

MASWALI NA MAJIBU

 . . . mengi itanibidi kuyapata, lakini nina . . . nilileta kamusi yangu ya maneno makuu. Huenda nikampa Leo hapa, au mtu fulani anayeketi karibu ili anisaidie mkipenda, tukilifikia.

² Sasa, kama bibi huyu aliyeko pale, kama kuna . . . kama yeye ange- . . . Wapi . . . Nani mume wake? Naam. Vema, ukitaka mke wako aje aketi pamoja nawe, wao—wao wangeweza, hakuna lo lote lisemwalo kwa ndugu ila lile lingesemwa kwa dada, pia. Sisi tu . . . wajua. Je, hilo . . . Ni sawa? Sasa, uwe huru kabisa kuwa pamoja naye. Je, ye—yeye ana joto pale nje, Doc? Vema, sawa, lakini ana ukiwa.

³ Na hakuna lo lote—lo lote ndani humu . . . wakati mwingine sababu yangu ya kutaja “Wanaume,” ni kwamba kuna wakati mwingine wanaume wanaweza kuuliza swali kati ya wanaume ambalo halingejibiwa wanawake walipo. Lakini hakuna ndani mle ila yale yangejibiwa tu papa hapa katika kanisa la kawaida, kwa sababu zaidi sana yanahusiana na wahudumu, na kadhalika, na nini agizo la—lao na yale yawapasayo kutenda.

⁴ Sasa, naamini haya yananaswa kwenye kanda. Kama . . . Sina hakika. Ndugu Goad, yuko wapi, je, haya yananaswa kwenye kanda sasa? Vema. Sababu ya kufanya hivi ni kuchunguza, ndugu, nini muhimu, se—sehemu gani, ile . . . nini yaliyo kwenye nia ya watu, mambo yetu ni—nini.

⁵ Ina—inatupasa sote kunena jambo lile. Sasa, kwa mfano, mtu fulani alingia na, tuseme, labda wanahudhuria kanisa la ndugu hapa, (jina lako la kwanza ni nani ndugu? Willard. Ndugu . . . Sasa, kuna Willard wawili humu, yanipasa niwapeni kitu kingine. Kama mimi . . . Jina lako la mwisho ni nani, sasa? Crase) Kanisa la Ndugu Crase, na Ndugu Crase angesema jambo fulani. Ndipo watoke Sellersburg hadi kwa la Ndugu Ruddell, la Ndugu Ruddell lingekuwa tofauti na hilo. Wanaenda kwa la Ndugu Junie, litakuwa tofauti, vivyo hivyo. Waje hapa Maskanini na bado tofauti. Ona? Inawafarakanisha watu.

⁶ Sasa, kama mtu fulani akisema, “Ee siamini unge- . . . inakupasa kweli kumpokea Roho Mtakatifu. Sidhani ni muhimu.” Kasema, kwa mfano, Ndugu Crase angesema hayo. Halafu uje kwa la Ndugu Ruddell, naye angesema, “Naam, ni muhimu.” Kisha uende kwa la Junie, aseme, “Vema, hamna tofauti sana.” Ona? Kama tungekusanyika hata . . . Laiti wahudumu wote wa Jeffersonville (katika hii jamii) wangekusanyika pamoja tupate kusema jambo lile lile.

⁷ Na hapo ndipo mara nyingi mashemasi na wadhamini . . . yawapasa watambue nini wajibu wao. Nami naona tuna mweka hazina wa kanisa na bawabu hapa usiku huu, kwa hivyo tutaona

wajibu wao ni nini. Lakini katika haya karibu yote (hapa) ni maswali ambayo yangeulizwa po pote na yangejibiwa po pote. Ni maswali rahisi tu, yakiwa kama wajibu wa wadhamini, wajibu wa... Sasa, kama ni wajibu hasa, nadhani hayo yamewekwa ubaoni hapa hivi sasa, kuhusu wajibu wa wadhamini na yale inayowapasa kufanya. Lakini nilidhani labda...

⁸ Na moja lilikuja pale, nami nadhani ni sawa, nitalijibu baada ya muda mchache, Bwana akipenda tulifikie, ni:

Katika mzozo fulani, shemasi apaswa kufanyaje? Yeye a... Nini wajibu wake mzozo unapozuka? Atafanyaje? Ona? Au mdhamini apaswa kufanyeje, mchungaji apaswa kufanyeje, kitu kama hicho, wakati wa mzozo? Tunajua utaratibu wa kawaida, lakini itakuwaje jambo fulani likitendeka nje ya utaratibu wa kawaida, ona, basi wao wapaswa kufanyaje?

⁹ Nasi twajua tu pa kuendea, ni kama tu mazoezi ya kijeshi, na kila mmoja wetu anajua mahali pake. Sasa, kama kundi kama hili, tungekaa hapa nusu usiku, twajua hilo, lakini ni... Sidhani inatupasa. Tatalijibu. Sasa nawatakeni kila mmoja...

¹⁰ Sasa, hakuna majina, mengine yana majina, lakini si—sitataja majina ya watu. Kwa sababu vyo—vyo vyote swali lilivyo, nitasoma tu swali. Kuna yapatayo mawili ndani mle yaliyo na majina. Naam, ngoja, huenda ningalipata lingine. Najua, ni mzee Daktari Ingleman, nilimpigia simu kule—kule upande wa kusini, pale 4-426 upande wa kusini. Hapo ndipo yule daktari mzee chini hapa tulipokuwa leo, kule Georgetown, aliponywa, au alipata fahamu baada ya kuzimia kwa muda mrefu na—na mengineyo. Sasa, nadhani hili linayo, sasa tutaendea maswali yetu ya kwanza niliyoyasoma kwanza.

Sasa, hebu tusimame kwa dakika moja hivi, tafadhalini.

¹¹ Baba yetu uliye Mbinguni, tumekusanyika hapa kama kundi la watu, Wakristo wanaokupenda, wanaokuamini Wewe, na waliojitolea maisha yao na kukutumikia Wewe katika ibada Yako. Kunao wahudumu hapa, vijana, wenye umri wa makamu, wana makanisa, wanahusika mbele za Mungu. Kunao mashemasi hapa wanaohusika katika huduma zao katika haya makanisa mbalimbali. Kunao wadhamini, wajibu wao. Wachungaji, wainjilisti, wo wote wale, Bwana, tunahusika Kwako. Na hiyo ndiyo sababu tunakusanyika, ili sisi sote tunene jambo lile lile kama vile tulivyoagizwa kuwa yatupasa kufanya katika Maandiko. Yatupasa sote kunena mamoja.

¹² Pia, Baba, twadhani, katika kundi kama hili, twaweza kupata baadhi ya ndugu zetu au baadhi yetu tunatofautiana kidogo juu ya mambo haya, na baadhi yao walikuwa wanauliza ili wajue Ukweli wake. Nasi twajua kuwa hatutoshi, kila mmoja wetu. Kama ningeuliza ye yote wa ndugu hawa wengine aje hapa kwenye maswali haya, labda wangeyajibu vilivyo au zaidi ya vile ningeweza kuyajibu. Lakini pamoja tunategemea ufunuo

Wako, upate kutufunulia sisi kwa Neno na kwa...kwa Roho Wako, ili...ili tupate jibu la kila swali. Ili mioyo yetu...ili tujazwe majibu na tuondoke tukijisikia kuwa tumejivika vilivyo kwa ajili ya huduma Yako na kutumikia utume wetu kuliko—kuliko tulivyo sasa. Hilo ndilo kusudi letu la kuwa hapa, Baba. Tujalie sasa.

¹³ Basi jibu maswali yetu, Baba, tunapokungoja Wewe. Kusiweko kutatizika katika nia zetu, lakini na tukae na swali hilo hadi limejibiwa vilivyo na tumetoshelezwa na Roho, limekubalika kwa wote kwa sababu ya Uwepo Wake. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁴ Nataka tu kunukuu Andiko, kwanza. Kama Isaya alivyosema, yule nabii alisema:

Haya, njoni...tusemezane, asema BWANA:...

¹⁵ Nami nadhani hiyo ndiyo sababu yetu kuwa hapa usiku huu, ni kujaribu kusemezana, kufahamikiana. Na sasa ningeanza... na nina baadhi ya mambo yaliyoandikwa hapa kulingana na namba na mengineyo, ambayo huyu Ndugu Wood...walishika...walipata bahasha hii yenye majibu. Na sasa nawatakeni kila mmoja wenu, ndugu zangu wapendwa, kujua ya kuwa—kuwa majibu haya ya—yanatolewa kadiri ni juavyo, vema ni juavyo.

¹⁶ Na majibu haya si yasiyokuwa na kosa, ona, kwa sababu Maandiko ndiyo hayana kosa, na kwa kadiri ni juavyo yanalingana na Maandiko. Natumai hilo layafanya dhahiri. Na kanda zitawekwa sasa na ye yote ambaye angezitaka, vema, wanaweza kuzipata. Lakini sasa, najua Maandiko hayana makosa lakini majibu yangu si yasiyokuwa na makosa. Kwa hivyo nina hakiko kila mtu afahamu hayo. Na kama sivyo—kama si yasiyokuwa na makosa, basi una haki ya kuniuliza labda wakati wo wote.

¹⁷ Kama kuna swali la mtu mwingine, si lazima liwe swali lako, lakini kama ni swali la mtu mwingine, labda hujawahi kuliwazia, lakini ni jambo ambalo sisi tuko hapa kusaidia. Tuko hapa ku—kukusanyika kwa sababu sisi tuko katika siku za mwisho, na siku hi—hizi ovu, na—nasi twataka tupate mazoezi, kuelimishwa.

¹⁸ Ndugu Stricker, mwanajeshi; Ndugu Goad nyuma kule, mwanajeshi; na labda Ndugu Ruddell hapa, yeye alikuwa mwanajeshi; Ndugu Beeler; na wengineo mbalimbali ambao wame—wamekuwa jeshini; mnakaa pamoja, mna—mnashauriana, mna—mnajua vita kabla hamjafika kule, na maarifa ya adui, mpate kumkabili ipasavyo.

¹⁹ Nilipokuwa nikipigana ngumi. Wangechunguza mpinzani wangu, jinsi atakavyokuwa, yeye hupigana vipi, kama ilikuwa ni kugonga juu au kupiga mdukuo wa shoto, au kukata na mkono wake wa kuume, ama kama yeye hutumia mkono wa

kulia au wa kushoto, na jinsi alivyo na nguvu, na iwapo yeye alinua mguu wake, na jinsi yeye alivyotumia macho yake, na yeye alitokea pembe gani, na maarifa mbalimbali ambayo tungeweza. Nao wangeona ni nini...wale—wale wakufunzi walikuwa wameshaona mtu yule akipigana hapo mbeleni. Kwa hivyo basi wangemweka huyo mtu pale pamoja nami kunipa mazoezi hasa jinsi mtu huyo alikuwa akipigana, ku—kujua yale yeye atafanya.

²⁰ Basi tuko hapa usiku huu kwa ajili hiyo. Tunajua pigo la adui. Twajua maarifa yake. Nasi tuko hapa usiku huu na Maandiko kumzingira ili asiweze kusonga, kwa sababu adui yupo kila mahali.

²¹ Ndugu Roberson, nilikuwa nikiwaza nyuma kule, nilipomwona, hakika yeye apaswa ajue mwanajeshi ni nini. Hakika yeye alishiriki vilivyo! Wanjeshi wangapi waliomo humu, hebu tuone, ambao wamekuwa askari jeshini? Tazameni hapa, ona, kundi lenu wanajeshi. Vema, sasa, mwajua ilivyo. Na hayo ndiyo msomeayo, sivyoy, Ndugu Roy, Ndugu Beeler, nanyi mashujaa wa vita na wengineo? Ni, kumpeleleza adui, “Yeye atafanyaje? Atatenda jambo gani?” Ndiposa utajua jinsi ya kukabiliana naye.

²² Na hiyo ndiyo sababu tuko hapa, kupeleleza mwenendo wa adui na—na kujua jinsi ya kukabiliana naye, kitu kitakachomshinda.

²³ Na kumbuka, hebu nisema hili, ndugu, kanisa hili ndogo limeanza kwa mlolongo wa karama, ona, karama zinaingia kanisani. Lakini kukiwamo karama au la, kama kusipokuwemo karama, nitawaambia, karama kila mara hazitamshinda adui, bali Neno litamshinda. Neno litakabiliana naye po pote.

²⁴ Na Yesu, alipokuwa hapa duniani, alithibitisha hilo. Yeye... Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Lakini Yeye hakutumia yo yote ya karama zake nzuri kumshinda adui. Twaona katika Mathayo... Naamini ni sura ya 2 au 3 ya Mathayo, Yeye alisema... La, sura ya 2 ya Mathayo, Yeye alipokabiliana na adui, alikabiliana naye kwa msimamo wa Neno, “Imeandikwa.”

Na yule adui alijibu, “Imeandikwa.”

²⁵ Kisha Yeye alisema, “Pia imeandikwa,” hivyo, hata akamshinda adui. Na hilo ndilo tuko hapa kufanya, ni kukabiliana na adui kwa zana ambazo Mungu alitupea sisi ku—kukabiliana naye.

²⁶ Sasa nina karibu maswali manne hapa yaliyo kwenye kile... yaliyo kwenye—kwenye karatasi moja, nami niliyatia nambari: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita... nane, kumi, na kuendelea hivyo. Na mara tu nimalizapo haya, ndipo nitarukia hayo pale. Linasema:

107. Ndugu Branham, kama maswali haya hayafai basi yaache, nami sitaudhika, nitajua haikuwa mkono wa Bwana. Si wali la kwanza:

Ndugu Branham, nimekusikia . . . kuwa ya—yapasa nirudi katika ile . . . ni—ni—nimesikia ukisema yanipasa nirudi hudumani, nami nimewaza kuhusu hilo, bali nimengoja neno dhahiri toka Kwake kuhusu hilo. Hata wa leo halijaja. Sasa, kwa kuwa najua mwisho u karibu sana, je, nizidi kumngoja Bwana Yesu ani—anzungumzie? Au, Yeye angependezwa kukwambia wewe ya kuniambia, kwa kuwa najua wewe ndiwe msemaji Wake kwa wakati huu?

²⁷ Vema, sasa, ndugu ninge- . . . nimeandika hapa jibu langu kwalo. Mungu anamwita ndugu huyu, wito maishani, sasa, kuna jambo moja kuu tungechukua tu hilo kama somo na kuhubiri usiku kucha juu yake, ona, jambo hilo moja, “wito.” “Fanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu,” ona. Hatutaki kushangaa kama tumeitwa. Yakupasa uwe umeitwa au utashindwa, tunapigana vita. Ona? Na kama una hakika kabisa, ndugu, kuwa wito wako ni wa Mungu, na umeitwa na Mungu kufanya kazi fulani. . .

²⁸ Sasa, kuna hila kubwa ambayo adui aweza kukufanyia. Yeye aweza kukufanya udhani hujaitwa hali umeitwa, ndipo yeye aweza kugeuka na kukufanya udhani hujaitwa; au akufanye u—udhani umeitwa hali hujaitwa; na vinginevyo, mojawapo. Na yakupasa uchunguze.

²⁹ Sasa, yakupasa kufanya hivi. Chunguza. Vema, sasa, huu ni wosia, jambo pekee niwezalo kusema ni wosia. Ona? Lakini hakikisha kuwa wito wako watoka kwa Mungu, na ndipo chunguza nia na makusudi yako. Ona? Sasa, mwajua lile ninalomaanisha kwa hilo. Nini nia yako katika kuhubiri? Je, ilikuwa tu. . . Je, ulidhani ilikuwa kazi rahisi kuliko uliyo nayo? Basi inakupasa usahau, haikuwa wito.

³⁰ Wito wa Mungu unachoma ndani yako hata usiweze kutulia mchana na usiku. Huwezi kuuondokea, daima unakuchomachoma.

³¹ Na—na kama ilikubidi uhubiri. . . Unasema, vema, sasa, kusudi lingine, “Ninaamini, kwa kazi niliyo nayo, kama ningekuwa mwinjilisti au mchungaji aliyefaulu, niwe na mshahara mzuri, niwe na nyumbani ambamo ningeishi na mengineyo, na niishi, basi ni—ninaamini hilo lingekuwa jambo zuri, rahisi sana kuliko hili ninalofanya sasa. Nami nadhani hakika ingekuwa. . .” Sasa, ona, kusudi lako kwanza ni baya. Ona, si sahihi. Ona? Ume—umekosea pale kwa hilo.

³² Ndipo ungesema, “Vema, labda kwa sababu mimi ni . . . nawaza kuwa labda nitakuwa mashuhuri sana kati ya watu.” Ona, utatambua uko tu tayari kuanguka kwa mshindo mkuu. Hakika, ona!

³³ Lakini, sasa, kama nia yako ni kuwa “Sijali kama itanilazimu kula biskuti na kunywa soda, nitahubiri Injili haidhuru.” Kitu fulani kinararua-rarua ndani yako. “Au nitahubiri Injili au nife.” Ona? Ndipo uta—utaenda mahali fulani, kwa sababu Mungu ndiye anayekushughulikia wewe. Mungu anajitambulisha Mwenyewe kwako, kwa sababu ni Mungu halitakupa utulivu. Na, kila mara, mtu aliyeitwa na Mungu hataki kamwe kuitenda hiyo kazi. Je, uliwahi kuwazia hilo? Mtu ye yote. . .

³⁴ Hivi majuzi niliulizwa na ndugu wapendwa sana, waliosema, “Sasa kwa kuwa tayari tumekuja katika Njia ile, Ndugu Branham, sasa kwa kuwa tumempata Bwana na kumpokea Roho Mtakatifu, tutafute karama kwa ajili ya huduma yetu itupasayo kutenda.”

³⁵ Nilisema, “Msithubutu kufanya hilo.” Ona? Usiwashauri watu wafanye jambo kama hilo, kwa sababu kawaida mtu anayetaka kufanya, huyo ndiye mtu asi—asiyeweza kulifanya.

³⁶ Mtu anayejaribu kuitoroka ndiye Mungu humtumia. Ona? Kama yeye anajaribu kuitoroka, “Ee, ndugu, nakwambia, mimi. . . wito umo ndani yangu lakini mimi. . . Whiu! Jamani, nachukia kujaribu hilo.” Vema, naam, mwaona. Huko—huko ni kujaribu kuikimbia.

³⁷ Kama yeye—kama yeye ataka kuifanya sana, muda si muda yeye anajikuta amejaa “majivuno.” Kama unavyosema, “Mungu, nipe nguvu kuhamisha milima, nakwambia, nitakufanyia kitu fulani ukiniiruhusu nihamishe milima.” La, yeye hawezi, hata ameshindwa kuwa na nia njema, ona, kwa hivyo yeye hangeweza kamwe kumhamishia Mungu milima.

³⁸ Hebu chukua, kwa mfano, kama Paulo. Unadhani Paulo angetoroka wito wake? Ee, ndugu! Yeye hangeweza. Ulikuwa tu unamchoma-choma mchana na usiku hata yeye akaliacha kanisa lake, akaacha kila kitu na—na kuenda chini kule katika. . . Naamini ilikuwa Asia, sivyo? Na kukaa miaka mitatu kule, akichunguza Maandiko, kuona kama ulikuwa sahihi au la, ona, kuona kama Mungu alikuwa amemwita kweli.

³⁹ Kwa hivyo kama Mungu anakuita wewe, ndugu, na unaendelea kuchoma-choma moyo wako, ndipo nitasema “Weka kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ikuzingayo kwa upesi.” Mwaona? Kama. . . Lakini kama haukuchomi, basi si—si—singeuwazia sana basi. Hebu acha tu ufikie mahali pake.

Sasa, yeye alisema, ndugu huyu alisema ndani humu:

Ndugu Branham, yapasa. . . Wadhani kuwa Mungu angekwambia. . . (eti mimi nimwambie yeye.)

⁴⁰ Naamini Mungu angemzungumzia yeye moja kwa moja. Kwa sababu, mwajua, Mungu. . . Sisi si watu wakubwa sana eti Yeye

asiweze kutuzungumzia. Na Yeye—Yeye—Yeye atazungumzia sisi, vema. Ona, Yeye tu. . . Yeye atatuzungumzia.

⁴¹ Nami nawaambia, kama Yeye aliniambia mimi, ndipo huyu ndugu aweza kusema, “Vema, Yeye alimwambia Ndugu Branham hivyo, Bwana asifiwe!”

⁴² Lakini, mwaona, si Ndugu Branham anayekupa wito ule, ni Bwana Yesu anayekupea wewe huo wito. Ona? Na kama ni Bwana Yesu anayekupa wito ule, Yeye atakuzungumzia. Ona? Ningekezungumzia masikioni mwako, lakini Kristo akuitapo hudumani hiyo huwa moyoni mwako. Ona? Hapo ndipo kitu kile chapaswa kutia nanga na huwezi kukiondokea.

Sasa, naamini kwa swali la pili. . .

⁴³ Sasa kama kuna swali lo lote juu ya hilo, swali lo lote juu ya hilo, ona, kwamba wito wa mtu yapasa uwe moyoni mwake, ukitoka kwa Mungu. Na—na ndugu mwingine. . . Lo, najua huyu ni nani aliyeandika hili. Ona, namjua aliyeandika hili, ndugu mpendwa na mwema, mtu aliyejaliwa ambaye ninaamini ana wito wa Mungu. Lakini mimi tu. . . Singetaka afanye hivyo (hiyo ndiyo sababu nilijibu jinsi nilivyofanya), ona, juu yangu juu yangu kusema; “Vema, ndio, Ndugu *Fulani* anapaswa kuingia katika huduma.” Ona?

⁴⁴ Sasa unasema, “Ndugu Branham aliniambia inanipasa kufanya hivyo.” Ona, na labda itakuwaje kama kitu fulani kilitendeka kwa Ndugu Branham, nivawe, au nife, au—au niondoke? Basi, ona, wito wako umekwisha basi. Lakini Yesu akikuita, ndugu, kwa kadiri kulivyo na Milele utakuwa bado una mlilo. Ona? Na ndipo unajua pale unaposimamia.

Sasa kwa la pili. . .

⁴⁵ Au kitu fulani kama hiki, “Tukijua kuwa ni siku ya mwisho.” Hakika nathamini hilo toka kwa ndugu huyo. Hakika nathamini hilo toka kwa huyu ndugu nikijua kuwa sisi tuko katika siku za mwisho, na unyofu wa moyo wake, akitaka kumtendea Kristo jambo fulani.

Linalofuata ni:

108. Sasa, kama Bwana wetu wa thamani akinijalia kumtendea jambo fulani ndogo, yanipasa nirudi kwa ile jamii ya wale ambao nimehudumia kwa sehemu. . . kwa makosa (ambalo nasikitikia). . . yeye ameyaweka hayo katika paradesi. . . na kujaribu kuwaamia Kweli? Wamekuwa—wamekuwa hivyo moyoni mwangu sana.

⁴⁶ La, ndugu; singedhani ni muhimu kwako kurudi katika jamii hiyo hiyo. Nami naamini, ndugu mpendwa, Bwana akuitapo huenda asikukubalie uende kama vile ulivyokuwa katika jamii hiyo, na wewe labda ulifundisha vitu au ulikuwa na vitu ambavyo havikuwa. . . ambavyo hakika unaviona vinginevyo sasa, ona, ambavyo huenda ukaviona tofauti na vile ulivyoona

wakati ule. Sasa, pia Bwana, Yeye alipokuita wewe, huenda . . . kama Yeye akikuhakikishia, huenda akakutuma mahali po pote. Ona? Si lazima uende kwa jamii fulani yo yote wala cho chote.

⁴⁷ Ulipokuwa kule ulikuwa mnyofu. Namjua ndugu, kama ninavyosema, aliyeandika maswali haya. Kwa unyofu sana, na nia ya Kikristo halisi hasa, ulifanya vema kadiri ulivyojua na kufanya yote uliyoweza, na hayo tu ndiyo Mungu anayohitaji. Ona? Sasa, Mungu akikuita urudi kwa jamii hiyo, nitarudi kule tena. Lakini kama Yeye hakufanya hivyo, ni—ninaamini ningeenda po pote Yeye anitumapo. Kuna swali?

La tatu:

109. Mtu anajua mahali pake halisi katika Mwili wa Kristo?

⁴⁸ Hilo ni zuri, zuri sana, “Anajua . . .” Hilo lingekuwa swali lenyewe kati ya wengi wetu hapa usiku huu, “Unajua hakika?” Sasa, ninabahatisha kuwa ndugu huyu ataka kujua, “Mahali gani, *wapi* katika Kristo, ninatumikia sehemu gani ya Kristo?”

⁴⁹ Sasa, kwa mfano, ningesema hivi, ndugu, kukupea wewe jibu bora sana nijualo. Mahali pako ni . . . katika Kristo panafunuliwa kwako na Roho Mtakatifu. Ndiposa ukitaka kujua kama ni Roho Mtakatifu au la, chunguza uone kama Yeye anabariki unachofanya, au la. Na kama Yeye anakibariki, basi ndiye Huyu. Kama Yeye hakibariki . . .

⁵⁰ Kama mtu fulani alivyoniambia mimi si muda mrefu umepita, kasema, “Bwana aliniita nihubiri.”

Nikasema, “Vema, hubiri basi.” Ona? Na kwa hivyo yeye—yeye . . .

⁵¹ Nadhani ndivyo ilivyo . . . Shetani, kama yeye aweza tu kumpata mtu fulani ku—kutenda hivyo ndiposa awadanganye wao, hilo ndilo analotaka kufanya. Ndipo ulimwengu wote huelekeza kidole chao papo hapo. Mtu fulani adhani wana karama ya kunena kwa lugha na kufasiri; wengine wana karama ya uponyaji wa Kiungu; wengine wana vitu kama . . . Wakati mwingine wanakosea katika vitu hivyo, ona. Na wakati mwingine wanadhani hawana hali wanazo. Kwa hivyo inahitaji uangalifu.

⁵² Kwa hivyo kila mara fanyeni hivi, ndugu zanguni, po pote mnajojisikia kuwa mnapaswa kufanya lo lote, kwanza chunguza kama kufanya hivyo kunalingana na Maandiko (kama kuko Maandikoni). Sio tu kuandikwa mahali pamoja, lakini namaanisha liwe la Kimaandiko katika Biblia yote kwako kulifanya, mahali pako, tuseme kama ungekuwa mwinjilisti, mchungaji, mwalimu, nabii, cho chote kile ambacho huenda Mungu amekuitia. Mwaona? Au kama una karama ya lugha, karama ya kufasiri, karama ya aina yo—yo yote kati ya hizo karama tisa za Kiroho kanisani, na zile afisi nne za Kiroho

za kanisa, mahali po pote, kwanza tazama uone kama Mungu alikuita.

⁵³ Ndiposa, kwa kawaida, jinsi niitazamavyo mimi mwenyewe, . . . huyu ni mimi, ninatazama hali ya mtu yule na kuona anakiri karama ya aina gani. Ona, Mungu atafanya kazi na viumbe vyake jinsi Yeye ameviumba. Ona? Yeye atamfanya kiumbe kimoja. . .

⁵⁴ Ukimwona ni kigeugeu sana na anaendelea, una . . . anasema, “Bwana aliniita mimi kwa *hiki* na *kile*, kuwa mchungaji.” Sasa, mchungaji hawezi kuwa mtu wa kigeugeu. Mchungaji ni mtu imara, thabiti. Ona?

⁵⁵ “Mungu aliniita kuwa mwalimu.” Basi mtazame jinsi afafanuavyo Neno. Ona? Iwapo yeye analichanganyisha sana na kadhalika, basi unaweza kutambua. Ona?

⁵⁶ Lakini, basi, jambo ni kwamba, mahali pako kwa kawaida hujulikana iwapo unaweza kufanya hayo au la.

⁵⁷ Sasa, Mungu aliponiita mimi kuwa mwinjilisti, nilitaka kuwa mchungaji. Nami nilidhani kukaa nyumbani hapa kungekuwa sawa. Kisha Bwana aliniita. Hatimaye watu walikusanyika. . . Hakuna mmoja wao aliyesalia usiku huu ndani humu, nao walilia na kuenda nje kule kwenye Barabara ya Spring 1717. Na bibi yule, Bi. Hawkins kule, alikutana nami na kusema (akilia, katika ule wakati wa shida, wakati jirani mmoja angepika maharagwe nasi sote tungeingia na kula hayo), naye alisema, “Nitawakubalia watoto wangu mezani kama tu utajenga maskani.” Ona?

⁵⁸ Na wito wangu ulikuwa muinjilisti. Asubuhi ile. . . Ikiwa papa hapa kwenye hili jiwe la pembeni, kama tungelipasua ndani mle usiku huu, mngeona ukurasa wa kwanza wa Biblia yangu ambapo Yeye aliniambia mimi niwe mwinjilisti. Ona? Nami sikuwa mchungaji aliyefanikiwa, singeweza kuwa kamwe, kwa sababu sina saburi na masharti ya mchungaji. Ona? Kwa hivyo basi kama nilijaribu kuwa mchungaji, ningekosea sana tu kama mchungaji anapojaribu kuwa mwinjilisti.

⁵⁹ Mwaona lile ninalomaanisha? Waweza kuona jinsi Bwana akuitavyo wewe, mahali pako katika Mwili ule. Kuna swali?

110. Je, watu wote waliojazwa Roho Mtakatifu watanena kwa lugha siku moja?

⁶⁰ Hilo ndilo swali la kwanza, “Je, wote waliojazwa Roho Mtakatifu. . .” Ndiposa, yote yako katika swali moja, nimeliandika hapa kama swali la nne. Lakini nita—nitasema hili kwanza, mwaona:

Je, watu wote waliojazwa na Roho Mtakatifu watanena kwa lugha siku moja? Nilipata pale Paulo alisema yeye “alinena kwa lugha kuliko wengine wote.”

Vema, swali nambari nne: **Je, wote hunena kwa lugha wanapompokea...** Au, la, lasema: **Je, wote hunena kwa lugha...** La: **Je, watu wote waliojazwa na Roho Mtakatifu watanena kwa lugha siku moja?**

⁶¹ Sasa, ndugu, mimi... Hili ni swali la kindani. Sasa, pale, labda ume-... Labda nitarudia tena majibu ya hili.

⁶² Roho Mtakatifu, sehemu moja ya Roho Mtakatifu ni kuhesabiwa haki. Hapo ndipo kwanza unapo... Mungu hana budi kukuita au hutaitwa kamwe. Ona? hakuna lo lote uwezalo kufanya mwenyewe. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Sivyoy? Kwa hivyo sehemu moja ya kuhesabiwa haki ni Roho Mtakatifu.

⁶³ Mmenisikia nikieleza yule mkuu wa chuo cha Kilutheri wakati ule kuhusu lile shamba la mahindi? Ona, "Mahindi, mtu aliondoka akapanda mawili... akapanda shamba lake la mahindi. Asubuhi iliyofuata yeye alienda na 'hamna kitu.' Baada ya muda mchache alipata majani mawili yakiota, akasema, 'Mungu asifiwe kwa ajili ya shamba langu la mahindi!'" Nami nilisema, "Je, yeye alikuwa na shamba la mahindi?"

Na yule mwalimu wa chuo cha Kilutheri akasema, "Kwa kutazamia."

⁶⁴ Nilisema, "Naam, kwa kutazamia yeye alikuwa nalo." Lakini nilisema, "Kwa..." Nilisema, "Hiyo ilikuwa ninyi Walutheri."

⁶⁵ "Baadaye huo mche ulimea na ukafikia kishada. Hicho kilikuwa Methodisti. Hatua ya pili ya hindi, ni kishada." (Nafikiri hiyo ni kweli, ninyi ndugu mtokao mashambani.) "Na ndipo kishada kile kinatazama majani yale na kusema, 'Enhee! Mimi ni kishada, ninyi ni majani tu! Ona, siwahitaji ninyi tena.' Na ndipo kishada kile... Mbelewele inamwagika toka kwa kile kishada, kurudi katika jani tena; yapasa kuwe na jani."

⁶⁶ "Na ndipo toka kwa hayo kunatokea masuke. Hayo yalikuwa Pentekoste, kurudishwa kwa zile karama kama ilivyotendeka hapo kwanza, kurudia ya asili. Ndipo masuke yalipoota, kasema, 'Sikuhitaji wewe, kishada. Wala sikuhitaji wewe, jani.'"

⁶⁷ Lakini, hata hivyo, uhai ule ule uliokuwa katika jani li-lile la mahindi uliotesha kile kishada. Na ule uliokuwa katika lile jani na kile kishada uliotesha ile punje. Kwa hivyo Roho Mtakatifu anaponena kwa lugha ni nini? Ni kuhesabiwa haki kwa hali ya juu. Ona? Kanisa Pentekoste ni nini? La Kilutheri la hali ya juu. Ona?

⁶⁸ Lakini sasa kile cha hali ya juu kitakapokuja, swali lingekuwa hili, "Basi nibaki tu hivi?" La! la, punje imekomaa. Ona? Unaanzia kwa punje. Anza na Ne-Neno, ile mbegu, litazaa kuhesabiwa haki. Basi kaa katika kuhesabiwa haki hata kutakapozaa kutakaswa. Kaa katika utakaso hata utakapompokea Roho Mtakatifu.

69 Sasa unampokea Roho Mtakatifu, atafanyaje? Nini . . . Bado kuna swali, sivyo? Vema:

111. “Kunena kwa lugha ni nini?”

70 Kunena kwa lugha si kinelela ila ubatizo wa Roho Mtakatifu aliokuhesabiwa haki na kukutakasa. Umejazwa sana! Sasa, nimetaka . . . nilitaka swali hili. Mungu ajua sikujua kamwe huyu angeliuliza, jibu . . . au kuliuliza.

71 Basi, ni . . . kukiwa na joto jingi sana ndani humu, fungueni huo mlango mkisikia usingizi na kadhalika. Nawatakeni mlipate hili vema na likolee. Kwa sababu ni—ni joto kidogo, huenda ikawafanya mkasinzie.

72 Sasa tazama, tazama hili: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

73 Sasa tazama hapa, liko hapa. Hebu nilieleze kwa mfano. Sasa, mimi niko chini hapa, mimi ni mwenye dhambi, ninaelekea *huku*. Wakati mmoja, baada ya kitambo kidogo, kitu fulani kinizungumzie. Na hakuna kiwezacho kunigeuza ila Mungu. Sivyo? Nimeelekea *huku*. Sasa, ninapogeuka, huko ni kuhesabiwa haki kwangu. Sivyo? Sasa, ile picha ndilo kusudi langu la kwenda, ona, picha ya Kristo.

74 Sasa nataka kufikia mahali ambapo najisikia vizuri kote. Ona, nimehesabiwa haki. Sasa nafikia hatua hii hapa ambapo naweza kuongea Naye, kwa sababu . . . Bado najionea aibu. Bado ninavuta sigara, ningali ninasema uongo na kutenda mambo madogo-madogo kisirisiri ambayo sipaswi kufanya, na wakati wote *heri* na *shari* zangu, *heri* na *shari*, lakini namtaka Yeye anisafishe toka kwa mambo hayo yote ili nielekee aliko na kuongea Naye. Ona? Vema, liko hapa, ni kuta- . . . hatua ya kutakaswa. Sasa, ilifanyaje? Ilininyosha mimi. Ona?

75 Sasa ninaelekea kwa Roho Mtakatifu. Ona? Na nifikapo *humu* mimi niko katika Roho Mtakatifu kwa ubatizo. Sivyo? Roho Mtakatifu anafanyaje? Yuanipa uweza. Uweza wa kuhubiri, uweza kuwa mwimbaji, uweza wa kunena kwa lugha, uweza wa kufasiri lugha. Amejaa uweza, kwa maana Roho Mtakatifu ni uweza wa Mungu. Na uweza wa Mungu ndio ulionibadili. Uweza wa Mungu ndio ulionitakasa. Naam, uweza wa Mungu ndio ulionijaza.

76 Sasa, katika muhula fulani, ninasimama hapa na ninajaribu kusema kitu fulani na Uweza wa Mungu unanijilia juu yangu sana hata siwezi kunena tena. Ona? Nami nilianza kugugumiza. Kama kwamba nilitaka kusema, “Ndugu,” na natoa sauti . . .

77 Kama hivi, tuseme, nitaeleza kwa mfano hivi. Nitasema nanyi ndugu zangu ili muwe na hakika kulifahamu. “Washi—washi—washindaje, ndugu?” Ona, mimi bado nina hatia. “Enhee, ni—nina furaha kuwa mimi—kuwa mimi bado ningali mmoja wenu. Ni—ni—nina furaha tele, mwaona.” Vema. Sasa, baada ya

kitambo kidogo, nini? Najua mnanitazama moja kwa moja na kujua mimi bado natenda upuzi, bado nafanya vitu ambavyo vina uchafu wa ulimwengu.

⁷⁸ Baada ya muda mchache ninasafishwa. Sasa kitu fulani kimetendeka, nimetakaswa. Naweza kukutazama kwa uso, mimi ni mmoja wenu. Ona? Vema, “Ndugu, Mungu asifiwe! Nina furaha kuwa katika hili kundi la Roho Mtakatifu. Nina furaha kuwa kati yenu ndugu watakatifu.” Mbona? Hamwezi kunielekezea kidole, nimesafika. Lakini sasa Mungu ataniweka mimi katika huduma. Sasa, naam, bwana!

⁷⁹ “Ndugu Branham, ulihesabiwa haki?”

⁸⁰ “Naam! Nakumbuka wakati ambapo ilikuwa vigumu kuwatazameni ninyi. Ndugu, naweza kuwatazama usoni sasa.”

⁸¹ Ona, tuko hapa. Sasa, hii nyingine ni nini? Sasa nita-... Hii imesafishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi, hii nayo inaanza kutumiwa. Sasa sisi sote twajua kuwa neno *takasa* ni neno la Kiyunani, neno la Kiyunani lenye maana mbili ambayo ni “Kusafishwa, na kutengwa kwa ajili ya matumizi.” Vyombo vile vilisafishwa na madhabahu, na kutakaswa na madhabahu na kutengwa kwa *ajili ya* matumizi. Lakini kuwa *katika* matumizi ni kujazwa na kutumikishwa.

⁸² Sasa, napitia hapa na sasa naja *kutumika*. Sasa, ilikuwa Mungu aliyenigeuza mimi, kasema, “Nisikize. Nisikize! Nisikize!” Na Yeye akasema...

⁸³ Mwafahamu lile ninalomaanisha? Ona? Na hapa, [Ndugu Branham aeleza kwa kumwiga mtu akinena kwa lugha—Mh.] Ona, hapa, umejazwa sana una... Naam. Ndivyo ilivyo, huko ni kunena kwa lugha.

⁸⁴ Nami naamini hili sasa: siamini kuwa kunena katika lugha ni ishara kamwe ya Roho Mtakatifu. Sivyo! Kwa sababu nimeshaona wachawi, walozi, washika-nyoka, pepo, cho chote kile kikinena kwa lugha, na si tendo lisilokosea la Mungu (Unaponena kwa lugha) kwamba una Roho Mtakatifu. Lakini, kumbuka, Roho Mtakatifu hunena kwa lugha na Shetani anaweza kumwiga.

⁸⁵ I-ishara kuwa umempokea Roho Mtakatifu ni maisha unayoishi, ona, “Mtawatambua kwa matunda yao.” Na tunda la Roho si (hakuna po pote katika Maandiko upatapo) kunena kwa lugha. Tunda la Roho ni upendo, furaha, imani, uvumilivu, utu wema, upole, fadhili, uvumilivu. Ona, sasa, hilo ndilo tunda. Hilo ndilo unalopata kwenye mti kuonyesha huo ni mti aina gani. Ona? Hilo ndilo...

⁸⁶ Watu wanawatazama ninyi wahubiri, na ninyi mashemasi, na ninyi wadhamini, na ninyi wainjilisti. Mngenena kwa lugha nje hapa barabarani siku nzima, hawangewasadiki. Lakini ishi

unayonena, onyesha utamu, na mizizi yote ya chuki haimo ndani yako, ndipo watu watatambua kuna kitu fulani.

⁸⁷ “Kunena kwa lugha.” Sasa, naamini hili, siku moja, kuwa mtu aliyejazwa na Roho anayekaa mbele ya madhabahu ya Mungu atanena kwa lugha. Lakini nimewaona wengi wakinena kwa lugha ambao hawakumjua Mungu kamwe. Ona? Hawakujua lo lote kumhusu kwa vyo vyote vile, nao bado hunena kwa lugha. Kila moja ya karama hizo yaweza kuigwa. Ona?

⁸⁸ Lakini tunda la Roho linathibitisha ni Roho gani aliye mle ndani, wewe unatoa ushuhuda wa Uzima wa Yesu Kristo. Kwa sababu kama mna maji embe katika mtofaa, utazaa maembe bila shaka. Naam. Ona, kwa sababu ndio uhai uliomo ndani yake.

⁸⁹ Sasa, hilo ndilo jambo lile lile lililoko hapa. Lakini sasa, niwaeleze hili ninyi nyote kusudi tupate kujua jambo lile lile. Naamini kuwa mtu aliyejazwa Roho ambaye. . . Sasa yeye anaingia katika Kristo kwa ubatizo, na tu. . . hilo si. . . Kunena kwa lugha si ishara ya huo ubatizo. Ona?

⁹⁰ Ubatizo, ungebatizwa katika uweza wa Shetani, na unene kwa lugha kwa ubatizo wa pepo za upotevu za Shetani. Ni mara ngapi tumeona hili likitendeka? Ni mara ngapi nimeona hili likitendeka?

⁹¹ Hata nimewaona wakinywa damu kwa fuvu la kichwa cha binadamu na kunena kwa lugha.

⁹² Nimeshawaona wachezea-nyoka jangwani walipojizungushia huyu nyoka mkubwa na kuendelea kunena. Wachawi wakajitokeza hivyo, nao wangenena kwa lugha na kuzifasiri.

⁹³ Nimekuwa katika kampi za wachawi ambapo wangeweka penseli hivyo, na kuweka kitabu hivi, na kalamu ile ilienda juu na chini ya bomba la jiko, na kuandika, “*Nyolewa ndevu na nywele, kwa pesa nane,*” na kuandika kwa lugha sizizojulikana, kisha na mchawi yule akafasiri na kueleza hasa yale yaliyotendeka. Ni—ninajua hayo mimi mwenyewe. Ona? Kwa hivyo mimi. . . Ona, huwezi. . .

⁹⁴ Paulo alisema, “Zikiwapo lugha, zitakoma. Ukiwapo unabii, utabatilika. Palipo na karama hizi zote, zitabatilika hivi karibuni.” (Tuna swali hilo baadaye.) “Lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo sehemu itabatilika.” Ona? Kwa hivyo tunataka kitu kikamilifu, ndugu. Ona? Twaona vitu vingi sana bandia na kutoa maelezo mabaya Kwake.

⁹⁵ Na usithubutu kumwendea mtu na—na uamini kuwa wana Roho Mtakatifu kwa sababu wao hunena kwa lugha. Ona? Lakini unaamini wao wana Roho Mtakatifu kwa sababu ya matunda wayazaayo, maana Yesu alisema, “Mtawatambua kwa matunda yao.” Ona? Naam, “Kwa tunda lao.”

⁹⁶ Sasa, lakini sasa, hebu tu nisiache hilo sasa, kwa sababu sitaki kudharau karama kuu ambayo Mungu ametoa. Ona? Nami naamini kuwa mwanadamu au mwanamke au mtoto aliyejazwa na Roho, anayeishi chini ya madhabahu ya Mungu, hawataishi pale kwa muda mrefu kabla hawajanena kwa lugha. Ona? Naamini kuwa mwanamunme huyo atatenda hilo, au mwanamke huyo.

⁹⁷ Sasa, unaweza kumpokea Roho Mtakatifu na labda hukunena kwa lugha ulipompokea. Ona? Lakini ukidumu pale daima mbele za Mungu wakati wote, huku ubatizo baada ya ubatizo unakugusa wewe, kitu fulani kitatendeka. Ona? Utajaa sana wakati mmoja hata huwezi kunena lo lote lingine; ona, u—u—unajaribu kusema jambo fulani, huwezi tu kulisema tena, na huwezi kulisema. Na wakati mwingi kama watu walitambua kuwa huyo alikuwa Roho Mtakatifu wangeendelea na kufungua tu mioyo yao na waache Mungu awazungumzie.

⁹⁸ Biblia ilisema, “Bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa.” Isaya 28, ona, 28:18, “Basi, kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa.”

⁹⁹ Anayegugumiza maneno ni nani? Mtu asiyeweza kunena dhahiri, anena [Ndugu Branham aeleza kwa kuiga mtu akigugumiza maneno—Mh.] Una . . . unagugumiza, ukijaribu tu. Ona, umejawa tu na Roho! Yeye anajaribu kusema . . . Kama nilikuwa nataka kusema, “Ndugu Ja—Jack— . . . Ja— . . . Ndugu Jack— . . . Ndugu Ja—Ja—Jack—Jackson.” Ona, ni kama hivyo, unajaribu kusema, huwezi kulisema. Ona, hilo ni, umejazwa sana na Roho! Ni . . .

¹⁰⁰ Nataka kuwaulizeni ninyi ndugu, mmewahi kusikia Roho Mtakatifu akitikisa sana hata ikawa vigumu kusema lo lote, ungeketi tu umetulia wakati mwingine, unaketi tu pale na kulia? Umepata kufanya hivyo? Vema, huyo ni Roho Mtakatifu. Kama unge- . . . Sababu ya watu kutokuongea kwa lugha wakati mwingi, hawajui jinsi ya kujinyenyekeza wenyewe kwa Roho nao wanatazamia kitu fulani mbali kule hali kiko juu yao. Ona? Hiyo ndiyo sababu hawa . . .

¹⁰¹ Halafu watu wengine wanajichochoea katika kuwashwa na kusema mafungu ya maneno ambayo hayana maana, wala bado hawajampokea Roho Mtakatifu, na kujaribu kusema wanaye kwa sababu walinena kwa lugha. “Mtawatambua kwa matunda yao,” Ona.

¹⁰² Sasa, kuna swali? [Ndugu Junior Jackson asema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Naam, ndugu. [“Nina furaha swali hilo liliulizwa, kwa sababu bila shaka mtu fulani alikuwa akishangaa huenda nilikubali na kufundisha jambo lile kwa kosa. Lakini naamini ni kama tu ulivyolifundisha.”] Asante, Ndugu Jackson, [“Haidhuru huenda nikanena kwa lugha

mara ngapi, au lo lote lile, kama maisha yangu hayashuhudii yale Biblia isemayo basi mimi si bora kuliko mbwa mchafu anayetembea barabarani.”] Naam. [“Na hata sikunena kwa lugha isiyojulikana hadi baada miezi sita baada ya ubatizo wangu.”] Hivyo ndivyo nilivyofanya, pia, Ndugu Jackson.

¹⁰³ Nilipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kule katika kibanda changu, ona. Na yapata mwaka mmoja baadaye, au kitu kama hicho, nili—nilikuwa . . . nilinena kwa lugha.

¹⁰⁴ Na yapata mwaka mmoja au miwili baada ya hayo, nilikuwa nikihubiri tena kanisani, nami nilikuwa—nilikuwa nimesimama jukwaani hivi, nami. . . Nilipokuwa mdogo na sikuwa nimekauka na mzee kama nilivyo sasa, ningezunguka-zunguka vema sana nami nilikuwa mwenye mwasho sana katika kuhubiri. Nilikuwa nimesimama pale nikihubiri nami niliruka tu juu ya dawati. Ilikuwa katika kanisa la Kibatisti, Kanisa la Baptisti la Milltown, nikaenda katika marefu ya kanisa, nikihubiri kwa nguvu tu kama nilivyoweza hivyo. Na mara tu nilipokoma kuhubiri, kitu fulani kilinipeperusha na nilisema maneno kadha, manne au matano, au maneno sita, katika lugha sizizojulikana. Na kabla sijajua yale niliyokuwa nikitenda, nami nikajisikia nikipaza sauti “Mwamba katika nchi ya uchovu, Kimbilio katika wakati wa tufani.” Ona?

¹⁰⁵ Kisha siku moja huku nikipita katika barabara ya reli, nilikuwa nikitembelea kufuata barabara ya reli, upande huu wa Scottsburg, nikifuata barabara ya reli, nikiilinda. Upepo ukivuma kwa nguvu, ee, jamani, na theluji imejaa kote njiani, nami nikavuka nipate kutembea zangu elfu thelathini na tatu; sitini na sita zilienda juu upande mwingine, nilienda nikifuata sambamba barabara ile. Nami nilikuwa nikitembea barabarani, na kwa ghafula. . . Nilikuwa natembea kule, na nilikuwa nikiimba. Mimi kila mara niliimba. Nilikuwa na mahali mbalimbali ambapo nilienda kuomba. Nami nilikuwa nikipitia pale, nikiimba, na kwa ghafula nikatambua nilikuwa nanena kwa lugha, ona, pasipo kujua yale niliyokuwa nikifanya.

¹⁰⁶ Kunena kwa lugha kunakuja kwa nguvu sana hata mtu yule ni vigumu kwake kujua yale wanayotenda. Wana-. . . Hawajui yale wanayosema. Na kufasiri ni vivyo hivyo. Hawajui yale watakayosema. Hawana habari watasema nini, kwa sababu ni ya kimbinguni. Ona, mradi unatia ya kimwili ndani yake basi hu-. . . u—u—unapata ya kimwili, mwaona. Lakini kama kitu fulani kinakushika tu na kukuzingira, na unafanya hilo. Ona?

¹⁰⁷ [Ndugu Neville asema, “Ndugu Branham, naweza kusema kitu fulani papa hapa?”—Mh.] Hakika unaweza, Ndugu Neville. [“Sasa, wewe katika kusema hivyo, hukusudii kusema, hata hivyo, kuwa—kuwa lugha ni sawa ibadani kama mtu hangeweza kujizua? Kwa sababu yeye. . . Mtu aliye na karama anapaswa kuizua.”] Yeye aweza kujizua. Naam. Kama tu. . . [“Yapasa

afahamu kutosha kuwa yeye yuko karibu kunena kwa lugha “] naam, ndivyo [“au yeye kwanza hana utarabibu.”] Naam yeye husikia. Ona? Sasa kama Biblia ilivyosema “Kama—kama kunaye mmoja anayenena kwa lugha na asikuwepo wa kufasiri basi na anyamaze.” Naam, bila shaka.

¹⁰⁸ Tuseme, kwa mfano, ninasimama hapa, mtu ye yote, unapoanza kupaza sauti, jambo lile lile. Je, uliwahi kusikia uweza wa Mungu ukikushukia ulipoanza kupaza sauti? Je, wangapi waliwahi kufanya hivyo? Vema, sisi sote. Ona? Unaketi tu pale, na unausikia ukija. Sasa, kuna wakati ambapo unaweza kuzuia hayo, ona. Unaweza kuizua, ona, si sahihi.

¹⁰⁹ Vipi kama ulikuwa umesimama, ukiongea na—na Rais wa Marekani, au ulikuwa umesimama nje hapa ukiongea na meya wa mji, na ulikuwa unaongea jambo fulani na kadhalika, papo hapo barabarani, ukiongea na kundi la watu, na kwa ghafula unajisikia tu kama ungeruka juu na chini, na kupaza sauti na kupiga shangwe “Utukufu! Haleluya!” na kugonga kila kitu na ukimbie huku na huko barabarani hivyo. Wangesema una kichaa. Ona? Wangesema, “Mtu huyo ana kichaa.” Ona?

¹¹⁰ Vema, ona, unajua vema kuliko kufanya hilo wakati huo. Unajizua, ijapokuwa inakuchomachoma ndani yako huwezi kujizua. Unasema, “Naam, bwana. Naam, bwana. Enhee, Enhee. Naam. Naam, bwana. Enhee.” Wee, inakuchomachoma na kukuvunjavunja lakini unajua kujituliza wakati huo. Unaona?

¹¹¹ Kwa mfano mahakamani hapa muda mchache uliopita, wao waliwashika Wapentekoste kule kwa—kwa kufanya jambo fulani na kadhalika, kupaza sauti sana au cho chote kile, ambayo ni. . . Walikuwa halali kabisa, mwaona, ni sawa. Lakini kila wakati hakimu alipowazungumzia au anataka kuwaambia jambo fulani, wangenena kwa lugha. Ona? Hakimu yule akasema, “Ondoa hawa wenda wazimu hapa.” Ona?

¹¹² Sasa, kama kungekuwa tafsiri kwa lugha hizo na yule hakimu aambiwe “BWANA ASEMA HIVI,” jambo *fulani na fulani* ambalo lingekuwa kweli, “BWANA ASEMA HIVI! Hakimu, unaketi hapa kunihukumia nini hapa hali usiku uliopita ulizini na kahaba? Jina lake ni Sally Juma, anaishi pale 44 mahali *fulani na fulani*, hivyo. Mbona wanihukumu? Hilo ni BWANA ASEMA HIVI! Sasa kana hayo na utaanguka ufe.” Sasa, ee, ndugu! Kuna jambo fulani tofauti pale.

¹¹³ Lakini unaposimama tu na kunena, na yeye alisema, “Wewe ni mjinga kwao.” Waona? Sasa unajua wakati upi wa kujizua na wakati upi usio wa kujizua. Ona? Sasa, hilo ni. . . Ona, ninaenda. . . Mnifahamu vizuri sasa, mwajua yale ninayomaanisha. Ona? Ndivyo. Bila shaka. . .

¹¹⁴ Tuna swali hilo papa hapa chini. Sababu ya kulishikilia hivi, tuna kitu kile kile, “Yawapasa kunyamaza?” Mwaona? Hiyo

ndiyo sababu sikulijibu zaidi ya yale uliyokuwa unasema. Lakini huo ndio wakati, kulijibu sasa, ona, sasa hivi. Na tutalifikia pia katika hili swali chini hapa, nami nitarejea kwake. Je, kila mtu afahamu hilo vema?

[Ndugu Fred auliza, **“Ndugu Branham?”**—Mh.] Naam. Naam, Ndugu Fred. [**“Je,—je mtu hunena katika—katika Roho, anapowajalia kutamka (tuseme yeye ni Mwingereza naye aweza kunena Kiingereza) na je, Roho angemjalia kutamka?”**]

¹¹⁵ Bila shaka. Naam, bwana. Ona, kwa sababu Roho Mtakatifu hunena katika kila lugha. Ona? Kwenye Siku ya Pentekoste kila lugha chini ya Mbingu ilikusanyika pamoja, ona. Kunena katika Kiingereza... Sasa, mimi daima nimejua hili, Ndugu Freddie, mimi binafsi, kuwa mimi... kama nimewahi kuhubiri mahubiri na kuna upako wo wote kwayo, ni Roho anayenijalia kutamka, mwaona. Ni... Ona? Kwa hivyo hayo yangukuwa lugha zisizojulikana kwa mtu ambaye hakufahamu Kiingereza. Bali hata hivyo...

¹¹⁶ Na kama tu vile lugha isiyojulikana si lugha “isiyojulikana,” ni... kuna mtu fulani pale... Kama kwenye Siku ya Pentekoste, wao walisema, wenye dhambi hawa wote, wao walisema, “Imekuware basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu wenyewe? Je, *tunawasikia* hawa Wagalilaya wakinena kwa lugha zetu wenyewe?” Hakukuwa na lugha “zisizojulikana” hapo kwa vyo vyote vile. Hamna kitu kama lugha “zisizojulikana” pale Pentekoste. Sasa, ona, hilo si kulingana na Maandiko kamwe. Ona? Hakukuwa na zisizojulikana... hazikuwa lugha zisizojulikana, ilikuwa lugha. “Imekuware basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyojaliwa nayo?” Hamna kutokujulikana hapo kamwe. Ona? Hilo... mna swali lo lote kwa hilo sasa, hivi sasa kabla hatujaliacha? “Imekuware basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu wenyewe?” Ona?

¹¹⁷ [Ndugu fulani asema, “Hapo—hapo ndipo kuna kosa ndogo kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu, na watu wata—watakaposhindwa kukubali lo lote, na kusema tu, ‘Sitaia mini vinginevyo, ila tu kulingana na Matendo 2:4!’”—Mh.] Vema, kama waliipata kulingana na Matendo 2:4 bila shaka hawangenena kwa lugha zisizojulikana. [“La, katika lugha.”] Enhee. Ingewapasa wanene ka—katika lugha ambayo watu wangekusikia, ona, kwa sababu “Kila mtu alisikia katika lugha yake.”

¹¹⁸ Sasa, nikipokea Roho Mtakatifu sasa hivi, kulingana na... ninasema... naamini kuna ndugu mmoja hapa anayetafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambaye ni—ni—ni Ndugu Wood. Sivyo, Ndugu Wood? Sikusudii, kukutaja, bali nyote... sisi hapa ni ndugu nasi tunataka kusema hili. Na yeye anatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, kama Ndugu Wood alipokea ubatizo

wa Roho Mtakatifu pale, kwa njia sahihi, kama alimpokea kulingana na Biblia, yeye angesimama pale, anene, yeye angenena katika Kiingereza, akisema, “Yesu Kristo Mwana wa Mungu amefufuka,” yeye alikuwa akiinena na unabii motomoto unaonena hayo.” “Najua kuwa Yeye ndiye, kwa sababu ameingia moyoni mwangu. Yeye ni Mwana wa Mungu! Dhambi zangu zimeondolewa, kuna kitu fulani kilichotendeka kwangu.” Ona? Naam. Huko ndiko kunena kwa . . .

“Imekuwa je basi sisi kusikia kila mtu kwa lugha zetu wenyewe?”

¹¹⁹ Tuseme, vipi kama sisi watu wa Indiana tuliongea lugha tofauti na watu wa Kentucky, na Ndugu Banks ni Mkentucky? Nao walinena lugha tofauti basi, nasi hapa twajua kuwa yeye hangenena lugha ya Kiindiana. Kisha yeye aamke pale na kunena katika—katika lugha ya Kiindiana, na twajua kuwa yeye haijui. Ona? Nasi tumsikie katika lugha ya Kiindiana, yeye anadhani ananena lugha ya Kentucky. Yeye anashuhudia tu, “Bwana asifiwe! Yesu amefufuka toka kwa wafu. Haleluya!” Lakini tunamsikia yeye katika lugha ya Kiindiana.

¹²⁰ Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste. Ona? “Imekuwa je twasikia kila mtu,” ona, “tazama, si hawa wote wanaonena ni Wagalilaya,” ona, Wa-Kentucky? “Na imekuwa je sisi Wa-Indiana, Wa-Ohio, na Wa-Illinois, na Wa-Maine, na Wa-Massachusetts, na Wa-California, twamsikia katika lugha zetu tulizozaliwa nazo?” Mnaelewa? Ona, ni kutiwa pumzi. Ona, ni kutiwa pumzi na Mungu. Ona wametiwa pumzi na Mungu kusikia, ni kutiwa pumzi kwao.

¹²¹ Ona ujumbe ule . . . ukweli ni kwamba, ni ushuhuda wa kufufuka kwa Yesu Kristo. Ona, naam. Sasa, kama Mungu haishi maisha hayo ndani yako, haijalishi utashuhudia mara ngapi juu Yake, bado hutampata. Ona? Naam. Hata u . . .

¹²² Kuna swali lingine sasa? [Ndugu Roy Roberson asema, “Vema, Ndugu Branham, nadhani kuwa tuliona hayo yakitendeka kwenye mstari wa—wa maombi, yule msichana Mhispania.”—Mh.] Naam. Sawa kabisa, Ndugu Roy. Ilikuwa kule—kule ninakoenda sasa, kule Beamont—Beamont. Je, ilikuwa Beamont? Naam, bwana.

¹²³ Sasa, mstari wa maombi ulikomeshwa. Msichana mdogo Mhispania alikuja jukwaani. Vema, kusema kweli, naamini nilikuwa naondoka, sivyo? Howard alikuwa akinipeleka nje, na—na huyu . . . Ni—ni—nikasikia mtu fulani akilia, alikuwa msichana mdogo Mhispania pale, ee, mwenye umri wa miaka kama kumi na mitano hivi, kumi na sita, vema . . . mtoto tu. Na—nami nikatazama, naye alikuwa na kadi ya maombi inayofuata kama ningeendelea. Nilikuwa na kundi kubwa pale, naye alikuwa na kadi ya kuombewa inayofuata. Nikasema,

“Mlete.” Kwa hivyo wakamleta. Nilikuwa naenda kwa mkutano mwingine, nami nilisema, “Mlete humu.”

¹²⁴ Kwa hivyo nikapata kutambua, nilimwambia jambo kama hili, “Sasa, utaniamini? Kama Yesu atanisaidia kukwambia nini shida yako, utaamini kuwa—kuwa Yeye atakuponya?” Naye aliinamisha tu kichwa chake. Nilidhani hapana budi yeye ni kiziwi na bubu pia. Ona?

¹²⁵ Kwa hivyo, nikapata kutambua, nilisema, “La, yeye hawezi kamwe kuingea Kiingereza.” Kwa hivyo walimleta mkalimani aje pale, nami nilisema “Utaamini?” Yeye akanipungia mkono... Basi yeye angesikia kupitia kwa mkalimani, bila shaka. Ona?

¹²⁶ Vema, ndipo nilisema... Nami nilitazama na kuona ono. Nikasema, “Nakuona wewe umeketi katika meko ya zamani na birika kubwa likiwayawaya, pamejaa mahindi ya manjano.” Ninyi wazee... Unakumbuka hayo, Ndugu Roy? Nilisema, “Ulikula mahindi mengi kupita kiasi. Na ulipofanya hivyo, ukawa mgonjwa sana na mama yako alikulaza kitandani kisha ukashikwa na kifafa.” Nami nilisema, “Umekuwa nacho tangu wakati huo.”

¹²⁷ Na ndipo msichana yule akamgeukia mkalimani na kumwambia kwa lugha yake, “Nilidhani yeye hangenena Kiingereza... au kunena Kihispania!”

¹²⁸ Naye mkalimani akanigeukia na kusema, “Hukunena Kihispania, sivyo?”

¹²⁹ Nikasema, “La.” Kwa hivyo tulichunguza kwa kinasa sauti, tukasimamisha kinasa sauti, ilikuwa Kiingereza kabisa.

¹³⁰ Lakini basi mkalimani akasema, “Uniambie yale yeye alisema.” Ona, ilimpasa apate tafsiri yake. Kasema, “Wewe niambie yale yeye alisema.” Naye alirudia maneno yale yale kwake, naye akayafasiri tena.

¹³¹ Sasa, yeye alinisikia katika lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo, nami nilikuwa nikinena Kiingereza. Yeye alinisikia katika Kihispania. “Imekuwa basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyojaliwa nayo?” Kisha mtoto yule akaponywa. Ona, ndivyo ilivyo, hizo ni kazi za ajabu za Mungu.

[Ndugu fulani auliza, **“Basi chombo kilicho na Roho Mtakatifu hakita... kitakuwa tu chombo na Yeye yule akijazaye aweza kukijaza yale Yeye...?”**—Mh.]

¹³² Cho chote Yeye atakacho, hiyo ni kweli, kweli hasa. Haya basi, chunguza kile umejazwa nacho, ndipo utajua kama una Roho Mtakatifu au la, wakati huo. Ona? Chunguza kile kilichojazwa humo. Kama—kama chombo kile kimejazwa taka, basi si chombo cha Mungu. Bali iwapo kimejazwa usafi, basi ni chombo cha Mungu. Mwaona ninayomaanisha? [Ndugu yule asema, “Na chombo kile, kuna wakati ambapo chombo kile

kitatumiwa na isijulikane, isijulikane, isijulikane wakati ule nini. . . wakati kilipotumiwa?”—Mh.] Ee, Bila shaka. [Ndugu atoa ushuhuda.] Enhee. Enhee. Naam hasa, bila shaka. Ee, sisi wote, twaona hilo. Nimeona hilo mara nyingi. Naam, bwana. Naam, bwana. Sisi sote. . . Tunajua tunafahamikiana na mambo hayo.

Naamini hilo lilikuwa nambari nne: **Je—je, watu wote waliojazwa na Roho Mtakatifu watanena kwa lugha siku moja? Nalipata ambapo Paulo alisema, “Ninanena kwa lugha kuliko—kuliko wao wote.”**

Sasa, lile ninalodhani sasa, kumalizia swali la ndugu:

Paulo akinena kwa lugha kuliko wao wote.

¹³³ Paulo alikuwa mtu mwerevu, yeye alijua lugha nyingi, yeye mwenyewe. Ona, yeye angenena kwa. . . yeye. . . Kumbuka wakati alipoingia majaribuni, yeye angenena kwa lugha hii au lugha ile, au yo yote ile. Na hizo ni lugha zisizojulikana kwa watu, lakini hizo hazikuwa zimevuviwa. Hizo zilikuwa lugha za kuzungumziana, mwaona. Lakini. . . halafu. . .

¹³⁴ Lakini naamini kuwa mtu aliyejazwa na Roho anayeishi chini ya madhabahu ya Mungu, bila shaka, hakuna budi, atapata na ujuzi wa kunena kwa lugha, kwa sababu hicho ndicho kitu cha chini sana na kitu kidogo sana kilichoko kulingana na maelezo ya Paulo. Kama ungeviweka katika orodha, ni kitu cha mwisho miongoni mwa karama, ona, ni kunena kwa lugha.

¹³⁵ Lakini sasa, kwanza, unabatizwa. . . Hapa, kila mmoja wenu nyote ni karama. Mimi niko nje. Sasa, “Kwa Mlango mmoja, Roho mmoja,” mlango mmoja unaingia katika chumba *hiki*. Sivyo? Sasa, siwezi kuingia *hivyo*, siwezi kuingia *hivi* na kurudi *hivyo*. Ona? Naingiaje ndani humu? Kwa kupitia kwa Ndugu Roberson? La, bwana. Kwa, vema, tuseme Ndugu Leo? La, bwana. Enhee. Vema, naingiaje? “Kwa Mlango mmoja, kwa Roho Mmoja.” Roho si lugha pekee. Ee, la. Jamani! Ona? Ona, “Kwa Roho mmoja nimebatizwa kuwa Mwili huu.”

¹³⁶ Sasa, *hii* ni Roho, *ninyi* nyote ni karama. Mwasema, “Vema, Mungu ahimidiwe!” Nitaenda kule na, tuseme, kuna—kuna Ndugu Wood, yeye ni miujiza. Ona? “Lo, nilitenda miujiza. Ninajua nina Roho Mtakatifu kwa sababu nilitenda miujiza.” Si kwa “muujiza” mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili ule.

¹³⁷ Mwendee Ndugu Junie basi, yeye ana maarifa, “Vema, vema, nina maarifa ya Biblia! Wee, nakwambia, ninajua nina Roho Mtakatifu kwa sababu ya hilo.” La, hiyo bado sio njia ya kuingilia.

¹³⁸ Vema. Si kwa Ndugu Leo, si kwa Ndugu Wood, si—si kwa Ndugu Junie. Ona? La. Bali kwa nini? [Makutano wasema, “Roho!”—Mh.] Vema. Nimebatizwa kuwa katika huu Mwili mmoja, sasa niko ndani yake, sasa Baba atanitumia wapi?

Ona? Jambo ni kwamba Leo yuko karibu na mlango; bila shaka hili lingekuwa mojawapo wa jambo la kwanza ambalo lingetendeka, au huenda lisiwe. Huenda nikajazwa sana Roho, hata Mungu angeenda moja kwa moja hapa kwa Ndugu Wood, awaruke wengine wote. Huwezi kuniambia mimi sasa sina Roho Mtakatifu, kwa sababu mimi niko katika Mwili huu kwa ubatizo. Lakini Mungu hakunileta hapa kamwe kusema, “Vema, Mungu ahimidiwe, nadhani nitaketi kitako sasa, nikastarehe, ninaenda Mbinguni.” Enhee! Mwaona ninalomaanisha?

¹³⁹ Lakini ningerudi moja kwa moja nyuma toka kwa hii hapa, nirudi moja kwa moja nyuma kwa ile. Mwaona ninalomaanisha? Ningetoka upande mmoja hata mwingine, au huenda nikaenda katikati, au po pote. Lakini kitu fulani kitatendeka, kitu fulani yapasa kitendeke. Na ni nini? Ubatizo wa Roho wanionyesha mimi kuwa niko katika Mwili ule, “Kwa Roho mmoja.” Mwafahamu hilo, ndugu, hapa? Vema! Naam? Vema.

112. Lugha na unabii vinapaswa kutumiwa vipi katika ibada... (Havipaswi kutumiwa kwa vyo vyote vile katika ibada! Ona?)...**kumtukuza Mungu...** (si kwa vyo vyote vile!)...**na kujenga kanisa? Najua watu husema roho ya nabii... najua lile... Ni—ninajua...** (p... nadhani kuwa... La, samahani, limekuwa “ni Biblia,” B-i-b-1-i-a nilianza p-i-p-i-l-i-a au kitu kama hicho. La)...**Bi—Biblia yasema, “Roho ya unabii inamtii nabii.”** (hakika)

¹⁴⁰ Kunena kwa lugha kwa kiroho na kutoa unabii ni kujenga kanisa, lakini vina huduma yake zenyewe. Ona? Si kusumbua mradi tu nabii wa kanisa ni... mkutano unaendelea katika utaratibu. Ona? Hazipaswi kuharibu mkutano.

¹⁴¹ Sasa, ona, “roho za manabii.” Tuna—tuna swali lingine sasa, hebu hilo lipite kwa dakika moja hivi. Ona njia halisi iliyo sahihi kwa hizi... kutumia karama hizi... Hili linajibia karama nyingi, mwaona. Tukiyafikia tutasema tulilijibu katika hili la kwanza, mtu huyu mwenye hili hapa. Ona? Hilo ni nambari tano:

Je, lugha na unabii vitumiwe katika ibada kumtukuza Mungu?

¹⁴² Mwaona, sasa, mhudumu yule... kama mhudumu ana upako wa Mungu, na kanisa liko katika taratibu, sasa njia sahihi... Wengi wenu mwajua jinsi nime—nimeongea nanyi kuhusu “kuweka utaratibu.” Karama hizi zapaswa... Sasa, hayo ndiyo tutakayofanya katika Maskani, Bwana akipenda. Sasa, ninatazama, ninaona kitu fulani, nitamwacha Ndugu Neville na ndugu hawa wengine katika utaratibu. Sasa mna... Na wengi wenu ndugu ni ndugu vijana.

¹⁴³ Sasa, mimi—mimi ni shujaa wa kale kwe—kwenu nyote katika Njia hii. Nimekuwa miaka thelathini na mmoja Humu. Ilikuwa yapata miaka thelathini iliyopita nilipoweka jiwe lile pale. Nimekabilia kila kitu kilichokuwepo kukabiliana nacho,

heri ujue yale unayonena, pia, uifikiapo. Heri usijue hilo tu pekee, heri kuwepo Mungu pale kuliunga mkono ufikiapo—utakapomaliza hayo.

¹⁴⁴ Sasa njia iliyofanikiwa sana ya—ya kufanya hili sasa, mngefanya mkutano maalum. Naamini hilo ndilo walilofanya katika I Wakorintho 14 pale, “Kitu fulani kikifunuliwa kwa mmoja anayeketi kando pale, na mwingine atulie basi.” Naamini ulikuwa “mkutano maalum wa karama,” ambapo ungekuwa sawa. Kama walitaka kuwa na mkutano maalum ambapo watu wote wenye karama walikutana mara moja kwa juma, wale walio na karama, na kuja kanisani, hilo lingekuwa sawa. Basi wafanye mkutano huo, hakuna . . . hakuna mahubiri, ni kwa ajili ya karama za Roho.

¹⁴⁵ Si kwa walio nje na wasioamini. Wangeingia, waketi, tuseme . . . Mmoja ainuke na kuenda, “ahaa-ahaa,” anene kwa kugha; mmoja aseme, “waa-aa.” “Nini jamani!” Wangeingia na kusema, “Kuko wapi kuimba? Mengine yako wapi?” Ona?

¹⁴⁶ Lakini, sasa, hawa wanaonena kwa lugha, wengi wao (na kufasiri, na kadhalika) ni watoto katika Injili. Ona? Usi—usiwaudhi, acha wao—acha wao wakue hadi karama ile . . . Baadhi yake, unaweza kuona jinsi Shetani hujaribu kuzua katika zingine. Hakika, mashujaa, sisi—sisi—sisi tunaona hilo. Ona, tunaweza kujua hilo, na utalichunguza.

¹⁴⁷ Hapa si muda mrefu uliopita mhudumu fulani, anayeketi papa hapa sasa, alinijia na kuniambia mimi na akanialika nyumbani kwake, ndugu mpendwa sana.

¹⁴⁸ Silisemi hilo eti kwa sababu yeye anaketi hapa, lakini ninyi nyote ni ndugu *wapendwa*. Kama singewaza hivyo, ningewaambia, “Hebu mimi na ninyi tunyoshe jambo hili kati yetu, kwanza.” Ona? Naam. Ona? Nawapenda ninyi nyote, nami nataka kulisikia katika roho wa uvumilivu kwa Biblia, mwaona, ku—kusaidia. Ona?

¹⁴⁹ Ndugu huyu alinialika nyumbani kwake ku— . . . mwanamke fulani, na mwanamke huyo alikuwa amekosea. Na hili . . . Sikuwa nimewahi kumwona mwanamke yule lakini nilisikia tu kwenye kanda, akifasiri lugha, akieleza jambo fulani. Ungeitambua papo hapo basi.

¹⁵⁰ Siku moja, mhudumu mwingine, nami . . . au mtu yule yule, tulikuwa tumeketi kwenye gogo, tukiwinda kuchakulo, alinena juu yake. Na wahudumu wote wawili, walioko sasa, wajua jinsi hayo yalivyokuwa. Ona, hebu, tazama.

¹⁵¹ Wakati ninyi wahudumu mnapomsahihisha mtu fulani kuhusu karama, mnapowasahihisha, mnapowasahihisha Kimaandiko, nao wanaudhika, kumbuka, haikuwa Roho wa Mungu, kwa sababu Roho wa Mungu hawezi kuudhishwa na Neno Lake. Yeye huja kwa Neno Lake. Ona, yeye kila mara

yuko tayari. Mtakatifu halisi wa Mungu anataka kufanya alivyoamriwa. Naam, bwana.

¹⁵² Nataka kusahihishwa. Nataka Roho Mtakatifu anionye katika mambo mabaya ninayotenda. Sitaki badilisho lo lote. Ni—ninataka jambo lililo sahihi au nikae bila, niache peke yangu, usi—usiniache niwe na lingine liwalo lote. Ona? Kwa sababu heri nifanye hilo kuliko kumfedheni Kristo.

¹⁵³ Nami singefundisha lo lote na singenena lo lote isipokuwa Maandiko...

¹⁵⁴ Na kama ndugu fulani, ndugu fulani Mkristo angeniona nikifundisha kitu fulani kwa kosa, ningefurahia kama ungeniita kando baada ya ibada, useme, “Ndugu Branham, ningetaka kuja chumbani mwako niongee nawe, umekosea kwa jambo fulani.” Ona? Ninge—ningefurahia hilo hakika, ndugu, kwa sababu nataka niwe sahihi. Naam.

¹⁵⁵ Sasa, sisi sote twataka tuwe sahihi, hiyo ndiyo sababu tunataka ku—tunataka kunena mambo haya. Nayo yanapaswa kupitia kwa Maandiko, mwaona, kufanya Maandiko yafungamane pamoja.

¹⁵⁶ Sasa, kunena kwa lugha yapasa... Sasa, baadaye kidogo... Sasa, hebu iendele sasa, kwa muda mfupi. Ona, ningewashauri mwache tu iendele na mwiache iwe hivyo. Kweni wahudumu sasa, ninyi wachungaji, acheni tu iendele hata watoto hawa wakomae kidogo. Sasa, labda, hakuna budi, kama ni adui anayejaribu kumdanganya mtu huyo, atajionyesha. Hatuna hakika sana.

¹⁵⁷ Sasa baada ya haya kabla hujaanza hili, pata roho wa hekima ndani mle kupambanua roho, mwaona, kuchunguza. Punde si punde, unaanza kuona kwamba mtu fulani ameanza kuona kuwa kuna kasoro kidogo, huo ni upambanuzi. Basi, lea hiyo kitambo kidogo. Ona? Ndipo uonapo upambanuzi ukikosea, basi sahihisha hilo. Na kama kitu kile... kama ni ya Mungu, itastahimili maonyo ya Neno. Ona?

¹⁵⁸ Tuseme, kwa mfano, nitasema tulineni kwa lugha, mtu fulani, tuna... hili ni kundi la watu waliokarimiwa. Na Leo aliinuka na kunena kwa lugha; ndipo, ndugu fulani hapa Willard, afasiri. Vema. Sasa, nataka kusema Ndugu Neville na Ndugu Junie na Ndugu Willard Collins walikuwa wapambanuzi, ona. Sasa, kwa sababu Leo alinena... Naam, sisi tuko tu hapa ndani kama katika mkutano mdogo wa watakatifu, mkutano wa karama, na Leo alinena naye Willard akafasiri hapa, naye alisema, “BWANA ASEMA HIVI! ‘Jumatano usiku atakuja mwanamke ndani humu naye ata—atazusha ujeuri. Mwambie Ndugu Branham asimkemee, kwa sababu yeye ana kichaa. Lakini mwambie yeye ampeleke pembeni, kwa sababu pembeni ndiko alikofanyia jambo ovu wakati mmoja na jambo fulani likatendeka.” Ona? Hilo laonekana zuri sana, siyo? Ona? Vema.

159 Sasa, lakini kwanza, mwajua, katika Maandiko ya kale, haidhuru nabii alisema nini au alilosema mtu ye yote, ilipimwa kwa Urimu Thumimu, kwanza. Ona, lilienda kwa Neno. Na kama nuru hizo hazikuangaza, waliitupilia mbali. Ona?

160 Na jambo la kwanza, sasa, hebu tulirudishe kwa Neno. Sasa, mtu *huyu* alinena kwa lugha, ilionekana sawa. *Huyu* akafasiri, ilionekana sawa. Lakini Neno lilisema, “Na ipambanuliwe na watu wawili au watatu, kwanza.” Ipeleke kwenye Urimu Thumimu.

161 Sasa, kwanza, Willard Collins asema, “Ilikuwa Bwana.” Junie asema, “Ilikuwa ya Bwana—Bwana.” Hao ni wawili kati ya watatu. Vema, inaandikwa kwenye karatasi, inatangazwa papa hapa katika kanisa hili. Ndipo watu wanaoiona ikisomwa kabla haijatangazwa, kisha waone ikitendeka, wao watasema, “Ndugu, huyo ni Mungu! Ona, huyo ni Mungu!”

162 Lakini vipi isipotendeka, basi itakuwaje? Ona? (Sasa, tayari tunafikia kwa jambo lingine ningeligusia papa hapa, “Je, unabii wote ni . . . tafsiri zote na ujumbe ni unabii?”) Sasa, hebu kidogo. Sasa, vipi isipotendeka? Basi *Leo* amenena kwa pepo wa uongo; *yeye* alitoa tafsiri ya uongo; *nanyi* mkatoa uamuzi wa uongo. Basi ondoeni kitu kile kwenu. Hamtaki hicho. Hicho ni kibaya. Kiacheni. Huyo ni Shetani. Ona? [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] “*Mimi* si mhubiri, lakini mimi ni—mimi ni mkalimani. Ona, mimi ni mkalimani, Bwana, mimi—mimi si mhubiri. Mimi. . .” Ndugu *Leo* asema, “Bwana, mimi si mhubiri, bali ni—nina karama ya lugha na Shetani alinihangaisha kwake. Mungu, kiondoe kitu kile toka kwangu.” *Wewe* unasema, “Bwana, *Wewe* umenipa roho wa upambanuzi, nami nimekuona *Wewe* ukifanya hivyo mara nyingi, imekuwaje? Baba, nisafishe! Nini kilitendeka?” Mwaona, naam, ndipo mmefanya sawa.

163 Ona, huo ni mkutano wa kawaida wa watakatifu. Nafikiri hivyo ndivyo ilivyokuwa katika Biblia, kwa sababu Paulo alisema, “Mmoja akitoa unabii na jambo fulani litabiriwe, jambo fulani li-. . . na jambo fulani lifunuliwe mtu aliyeketi basi na atulie hata huyu amenena kwa lugha kwanza, ndipo yeye aweza kunena. *Nanyi nyote* mwaweza kuhutubu zamu kwa zamu.” Sasa, hilo halingekuwa katika mkutano wa kawaida, mwajua hilo, kila mmoja hangeweza . . . karama zile.

164 Sasa, iweni na hakika kuwa ni ya Mungu, ona, kwa sababu kama ni upumbavu tu si ya Mungu. Isipotimia, si ya Mungu. Ona? Yapaswa itimie. Na—na kwa hivyo katika makanisa yetu, mwaona, ndugu, tuna kanisa imara basi, ona, ambapo hakuna mtu awezaye kusema kuwa lo lote limewahi kusemwa au kutendwa. . .

165 Tazama linakoniweka, ninapokuwa kule mbele ya umma. Tazameni hilo! Na kosa moja je la hayo? Ona? Kwa sababu namtumaini. Ona? Namtumaini. Mtu fulani anasema,

“Unaogopa kosa, Ndugu Branham.” La, la, enhee, siogopi kosa. Namwamini Yeye. Yeye ndiye Ulinzi wangu. Nimechaguliwa kufanya hivyo kwa hivyo nitakaa papo hapo.

¹⁶⁶ Kama Mungu amekuchagua wewe kufanya kitu fulani, basi Yeye ndiye Mlinzi wako. Ona, Yeye atakulinda. Kama Yeye alikutuma, Yeye atalidhihirisha neno lako. *Wewe* ni balozi aliye na karama ya kufasiri, *wewe* ni balozi aliye na karama ya upambanuzi; nyote watatu. Mwaona yale namaanisha? Ndipo mna nini? Mna kanisa imara. Hungeogopa kusimama tena kama ilivyokuwa hapo jana.

¹⁶⁷ Hapa, nilikuwa mkutanoni chini kule. Kijana mdogo toka Uingereza alikuja hapa, alikuwa anajaribu kujinyonga. Ndugu Banks alikuja pale na kusema, “Yeye amekuwa kule kwa siku nne au tano.” Nilikuwa na shughuli nyingi, lakini yeye alisema, “Kijana yule atajinyonga.” Hotelini mwa Waterview kule chini walikuwa wakiniambia mimi kuhusu hali ya mvulana yule.

¹⁶⁸ Nami niliingia chumbani kumwombea. Nikatoka nje na kusema, “Sasa, Ndugu Banks, sijawahi kumwona mtu yule au kujua lo lote kumhusu, lakini nitakwambia shida yake kabla sijafika pale.” Sivyo, Ndugu Banks? Na tulipofika pale, Roho Mtakatifu alishuka na kumwambia yeye kile kilichosababisha hayo na yote kumhusu, na pale alipokuwa na kuhusu maisha yake yote. Nusura aanguke.

¹⁶⁹ “Unaogopa kosa, Ndugu Branham, kumwambia mtu kitu kama hicho?” Vipi jukwaani, ukimwambia mtu kwamba haishi mwaminifu kwa mke wake, amepata mtoto kwa mwanamke mwingine? Yeye atakutupa korokoroni. Heri uwe sahihi! Ona? Ona? Usiogope, kama ni Mungu. Lakini kama huogopi... Kama—kama hujui kama ni Mungu, basi tulia hadi iwe ni Mungu. Sivyo? Kuwa na hakika u sahihi ndiposa uendele.

¹⁷⁰ Sasa, haya ni mafundisho magumu, ndugu, lakini ninyi ni ndugu zangu. Ninyi ni—ninyi ni—ninyi ni wahudumu vijana mnaoinuka, nami ni mzee, nitaondoka hivi karibuni. Ona? Na kwa hivyo hakikisha ni—ni sahihi.

¹⁷¹ Nilipokuwa chumbani mle mwa... Labda nitalishika hili badaye kidogo humu. Mvulana... Vema, nitasema sehemu yake sasa. Jana mimi pamoja na Ndugu Banks, tulikuwa na shughuli nyingi mno, tumekuwa (ee, jamani) kwa nguvu niwezavyo, nami nita—nitawaambieni yale niliyokuwa naenda kufanya katika mkutano huu. Leo na Gene na kundi letu tulikuwa tukienda kule, pamoja na ndugu, kisha tuseme sisi tulikuwa tunaenda kuwinda nguruwe, kuwinda nguruwe—mwitu. Walikuwa na siku tano za kuwinda aina ya nguruwe aitwaye Javelina, katika Arizona, baada ya mkutano ule kwisha, mkutano wetu ulipomalizika. Tulienda Phoenix siku moja, na ilitupasa kungoja siku tano kabla hatujawa na mkutano mwingine po pote, siku nne kabla wao hawajafanya mkutano mwingine ko kote.

Yatupasa kuwa papo hapo Arizona. Vema, wakati uo huo ndio wa majira ya kufunguliwa kuwinda javelina.

¹⁷² Kwa hivyo nilitaka kuenda kulenga bunduki yangu ndogo, kuona kama ilikuwa sawa. Banks alikuwa yuaenda pamoja nami. Tulianza kuondoka langoni, kuelekea langoni. Akaingia mtu moja kwa moja ndani, juu ya ubao ule (ona, uliosema, “Tafadhali msimwulize Ndugu Branham”).

¹⁷³ Ona, sababu ya kufanya hayo...si kwa watu walio wagonjwa. Yangu, nyumba hiyo, uliza Banks, yeye alikuwa jirani yangu. Watu huja, mchana na usiku na kadhalika, wakiwa na watoto wagonjwa, na kadhalika. Hatumkatai mtu kama huyo. Lakini...

¹⁷⁴ Nao wakaniita, Leo na wengineo, toka nje pale kwenye gari, Jim na wengineo, “Kuna mtu hapa aliye na mtoto mchanga. Pia kuna mtu hapa hawezi kansa.” Tuliachilia kila kitu tukamwendea yeye.

¹⁷⁵ Usiku ulipita niliitwa katika chumba cha hospitalini ambapo mtu fulani aliniita, na mtu yule hangeniruhusu hata niingie baada ya kufika pale. Ona, mtu mwenye shauku. Lakini hilo ni sawa, naenda haidhuru. Ona? Kwa sababu ni wajibu wangu kuenda, ona, na kujaribu kumsaidia mtu fulani.

¹⁷⁶ Vema, hilo silo kusudi la ubao ule. Lakini mtu huyu, tulipokuwa tu tunaingia garini, na Ndugu Banks ajua kuwa ilinipasa ku...Sijui kwa nini nilisubiri kwenye nyumba. Mtu fulani alikuja kwa Ndugu Banks akamchelewesha. Na punde tu nilipoingia mle, nikacheleweshwa. Ndipo mara tu tuliposhika bunduki zetu na kuanza kuingia garini, hapa akaingia mtu moja kwa moja ndani. Akaja pale.

¹⁷⁷ Nami nilikuwa tu najitayarisha kumwambia aondoke na apige simu kule (kule BUTler 2-1519) pale kwenye ubao ule. Nilisema, “Tuko na haraka.”

Kasema, “Nadhani uko na haraka, bwana.”

Nilisema, “Jina langu...”

¹⁷⁸ Kwanza nikamwendea, akasema, “Washindaje?” Nami nikaona kuwa yeye hakujua mimi nilikuwa nani.

Nilisema, “Jina langu ni Branham.”

Yeye alisema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nilisema, “Naam.”

¹⁷⁹ Naye akasema, “Mimi—mimi...nilitaka kuonana nawe, Ndugu Branham.” Kasema, “Naona unajitayarisha kuondoka.”

Nilisema, “Naam, bwana. Ninajitayarisha.”

Akasema, “Najua wewe una haraka.”

Nikasema, “Ninayo sasa hivi, bwana.”

180 Naye akasema, “Vema, nilitaka tu kuongea nawe kwa dakika chache.”

181 Nami nilitaka kumwambia; kisha Roho Mtakatifu akasema, “Mpeleke chumbani, unaweza kumsaidia.” Sasa, pale, hilo labadili kila kitu. Bunduki iliwekwa tu kando, na kila kitu hivyo, kazi ya Mungu kwanza. Ona? Naye alisema . . .

182 Nikasema, “Njoo, nifuata.” Nilisema, “Nitakuja baada ya muda mchache, Ndugu Banks.”

Yeye alisema, “Ni kuhusu nafsi yangu, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Vema, ingia.”

Nikapitia nyumbani, Meda akasema, “Hujaenda bado?”

183 Nikasema, “La, la, la, ni mtu fulani hapa.” Nikasema, “Waweke watoto katika chumba kingine.” Nilimpeleka katika chumba kidogo cha faragha, akaketi chini. Kabla tu hajatulia . . .

184 Mtu huyu alikuwa kanisani usiku uliopita. Au yeye hakuja, Banks? Je, uli-. . . Naam, vema, yeye alipaswa kuja usiku uliopita. Yeye alikuwa tu . . .

185 Kwanza, Roho Mtakatifu alianza kumwambia yeye alikuwa nani, kile alikuwa amefanya, kile kilichotendeka kote maishani mwake, kila kitu kuyahusu, ona, papo hapo, akimwambia kila kitu. Banks ni shahidi. Hakufungua kamwe kinywa chake na kunena ila tu yapata maneno mawili kwangu; na pale akaja akimwambia, kasema, “Umekuwa mhuni, wewe hakika unaishi kule Madison. Ulitoka tu kule Evansville, Indiana. Umekuwa chini kule katika hii shule ya Biblia, ya dini iliyojitenga, ukafarakanika. Umefika Louisville dakika chache zilizopita. Kulikuwa na mtu fulani, na mtu yule alikwambia (uliyeketi na kula naye), alikwambia uje hapa unione mimi na ‘yeye atakuondoa shidani.’” Nikasema, “Hayo ni BWANA ASEMA HIVI!”

186 Huyu mtu ameketi tu, akipepesa macho yake, akinitazama, akasema, “Naam, bwana!”

Nilisema, “Limekuduwaza, sivyo?”

Yeye akasema, “Naam.”

Nikasema, “Je, unamwamini Roho Mtakatifu?”

Yeye alisema, “Nataka kufanya hivyo, bwana.”

187 Basi nikasema, “Unataka nikwambie yale unayowaza?”

188 Yeye akasema, “Naam, bwana.” Nami nikamwambia. Yeye alisema, “Naam, ndugu, hilo ni kweli.”

Na nilisema, “Badili mawazo yako.”

Yeye alisema, “Vema, nimeyabadili.”

Nilisema, “Unawaza *hivi*.”

Yeye alisema, “Naam! Naam!”

¹⁸⁹ Nilisema, “Sasa, huhitaji ono, unahitaji tu kunyoshwa.” Nami nikamwambia jambo fulani pale hungenitaka mimi kulisema. Lingalikuhusu, hungalitaka. Ni jambo fulani baya lililokuwa la kuogofya, kwa hivyo hungelitaka niliseme kama lingalikuhusu. Nami siwaambii watu yale Bwana anionyeshayo. Kwa hivyo nilisema tu, “Vema, utalifanya?”

Yeye akasema, “Nitalifanya.”

Nilisema, “Nenda zako.”

¹⁹⁰ Tulikuwa ndani humo hazipiti dakika kumi, sivyo, Ndugu Wood? Yapata kati ya dakika saba na kumi. Tukaondoka, tukarudi barabarani, tukienda barabarani, yeye na mimi na Ndugu Banks na mvulana wangu mdogo, Joe, naamini ilikuwa hivyo, tukiendesha pamoja, tukielekea kwenye kituo cha ushuru. Yeye aligeuka kunitazama mimi, akasema, “Bwana, nataka kukuuliza swali fulani.”

Nikasema, “Vema.”

¹⁹¹ Yeye akasema, “Nimetatanishwa kidogo.” Yeye alisema, “Ulijuaje mambo hayo yote kunihusu mimi?” Ona? Banks alikuwa ameketi pale.

¹⁹² Nami nilisema, “Bwana, umeshawahi kusikia kuhusu maono yangu na huduma yangu?”

¹⁹³ Yeye akasema, “Sikuwa nimejua jina lako kamwe hadi yapata saa moja iliyopita. Mtu fulani aliniambia, aliniambia tu kule Louisville, aliniambia nije huku, nami nikavuka tu daraja.” Sivyo, Banks? Yeye alisema, “Sikuwa nimejua jina lako kamwe, kujua wewe ulikuwa nani.”

¹⁹⁴ Nilisema, “Katika huduma yangu, ni karama ya Mungu ambayo Yeye alituma.”

¹⁹⁵ Yeye alisema, “Basi kama hiyo—kama hivyo ndivyo ilivyo,” kasema, “Sasa nime- . . .” Kasema, “Nimekuwa tu. . . Nimepona sasa,” akasema, “kila kitu kimekwisha.” Ona? Akasema, “Hapana shaka, huyo alikuwa ni Mungu akinena nami kupitia kwako.”

Nikasema, “Sawa.”

¹⁹⁶ Yeye akasema, “Sasa, nafahamu katika Biblia kuwa . . . Wakati mmoja nilisoma katika Biblia na, kasema, Yesu aliwaambia wanafunzi Wake.” Ambalo alikusudia “watu,” mwaona. Kasema, “Aliwazungumzia wanafuzi Wake na kuwaambia mambo waliyokuwa wanawazia.” Ona, “kutambua mawazo yao” ndiyo aliyokuwa anafikia. Yeye alisema, “Na Yeye alisema ni Baba Yake aliyekuwa akinena kupitia Kwake.”

Nikasema, “Naam.”

¹⁹⁷ Alisema, “Sasa basi, Baba basi alikutumia tu wewe kunena nami kupitia kwako, kuniambia mambo haya na kunifanya niamini yale uliyoniambia ni kweli.”

Nikasema, “Yalikuwa kweli?”

Akasema, “Naam.” Kasema, “Basi haina budi kuwa Mungu.”

¹⁹⁸ Nami nikasema, “Ndugu, unajua mengi kuihusu sasa” (mimi na Banks tulikuwa tunasema) “kuliko wengine ambao wamekuwa mkutanoni kwa miaka kumi na bado hawajui.” Mtu huyo—huyo tu! Sasa, hivyo ndiyo hilo lilivyo. Ona?

Na Roho (kitaratibu) katika lugha je, unabii utumiwe wakati wa ibada?

¹⁹⁹ La. Yapasa vitumiwe *hivi*, kisha *ielezwe* katika ibada. Lakini kwa wakati huu, kwa wakati huu uliopo, waacheni wanene. Sasa, isipozuilika, basi siye, yapasa mtazame hilo. Sasa, wakati mwingine huenda ikawa ni Mungu. Halafu maskini watu hao, kama mtoto anavyojaribu kutembea, sasa, akianguka chini mara nne au tano. . . Sasa, nimeona hili tangu nimekuwa hapa kanisani, na—na, vema, nita—nitaliacha tu hivyo. Ona? Na, lakini, mwaona, lakini na hilo je, ungesema basi, “Ndugu Branham, mbona hukusahihisha hili?” La, la.

²⁰⁰ Billy Paul nyuma kule alipoanza kutembea, kwanza, yeye alikuwa akianguka na kuamka, na alianguka chini mara ningi zaidi kuliko alivyosimama juu. Lakini yeye hakujua kutembea. Lakini naamini yeye alikuwa na karama ya kutembea. Ona? Nilimwacha atembea kidogo. Na alipojikwaa miguu yake mikubwa, namwambia yeye hayo Sasa. Mwaona lile ninalomaanisha? Ona? Akitembea huku ametazama kitu kingine na kuanguka kwa kishindo na kadhalika, nasema, “Inuka, mwanangu. Uko wapi?” Ona? Sasa, hiyo—hiyo ndiyo tofauti, mwaona.

²⁰¹ Sasa, acha wao—acha wao wajikwae na wajikokote kwa muda mfupi. Sasa, inapokupasa kuwasahihisha, ikiwaudhi basi unajua mwenyewe haikuwa Mungu. Kwa sababu Roho wa Mungu ni mtiifu. Kama tulivyopata hapa kidogo, “Roho wa ‘Roho ya unabii humtii nabii.’ Ona? Naam.

[Ndugu Stricker anasema, “Ndugu Branham, ninataka kusahihishwa.”—Mh.] Vema, ndugu. **[“Wakati mwingi nimeketi katika ibada nami nimesikia kunena kwa lugha na kufasiri, na wakati mwingi nilijisikia vibaya sana kuhusu hayo. Nami huenda nyumbani na ingeonekana kama kwamba ningetubu yote. Je, ilikuwa sababu nilijisikia havikuwa vya Mungu, au je, ilikuwa sababu havikuwa katika taratibu?”]**

²⁰² Huenda ikawa, ndugu, labda ni mojawapo ya hayo mawili. Ona? Ningesema. . . Sasa, huyu ni—huyu ni William Branham,

ona; hadi niingie katika Maandiko, naam, bado ni mimi, mwaona. Sasa, ningesema hili, Ndugu Stricker, hilo lingekuwa mojawapo wa hayo. Huenda ikawa vilikuwa nje ya taratibu; huenda ikawa ulikuwa na walakin; huenda ikawa mtu huyo alikuwa na kasoro; kasoro fulani katika huu ujumbe; au lo lote laweza kukufanya wewe *ujisikie* vibaya.

²⁰³ Sasa, basi, hebu nikusaidie kidogo, Ndugu Stricker, hapa. Ona? Kila mara. . . Usihukumu kamwe cho chote kwa kujisikia, mwaona. Kihukumu kwa matunda yake, mwaona; matunda yo yote kizaayo, mwaona. Kwa sababu wakati mwingine. . .

²⁰⁴ Naam, twatambua kuwa kuna vitu unavyojisikia, huko kujisikia kwa kipepo. Mimi hukupata, na, wee, naanza kukuondokea upesi sa—sana, mwajua. Lakini sisemi lo lote. Nakuacha tu pekee kwa sababu sijui ingekuwaje, mwaona, hadi *nijue* ni nini.

²⁰⁵ Sasa, kama watu wengi wasemavyo, “Wee! Ndugu, najua nina Roho Mtakatifu! Haleluya! Mungu asifiwe!” Na bado wasiwe na Roho Mtakatifu. Wangenena kwa lugha, na kadhalika, na kupiga shangwe na kucheza katika Roho, na bado wasiwe na Roho Mtakatifu. Kwa sababu mvua hunyea juu ya wenye haki na wasio haki. Si kwa kujisikia, ni kwa *matunda* yao.

²⁰⁶ Tuseme kuna. . . Mwakumbuka ono langu juu ya hayo? Jinsi hayo. . . Waebrania 6, mwaona, “Mvua mara kwa mara inyeayo nchi ni kuipa maji, ambayo kwa ajili yake hulimwa, lakini miiba na magugu hukataliwa ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.”

²⁰⁷ Tafadhalini, nitaongeza hewa kidogo, najua ninyi nyote mnaanza kusinzia na kuchoka. Kwa hivyo sasa, ngoja, yanipasa kuharakisha kupitia kwa haya upesi kidogo au sitayamaliza. Hili lina- . . . Tuko karibu kwa msingi wa—wa haya yote, katika kundi hili hapa. Lakini yata- . . . Ona, ile. . .

²⁰⁸ Hapa kuna sha-shamba la ngano. Na katika shamba hilo kumepandwa makwekwe na makombe, au cho chote kile, magugu. Basi, kiangazi kimeshika. Naam, je, makombe hayaoni kiu kama ngano? Na ni mvua aina gani. . . mvua maalum hunyea ngano halafu mvua maalum ikanyea magugu? Hiyo ni kweli? La, mvua ile ile huyanyea. Sivyo? Roho yule yule anayewashukia manafiki ndiye yule anayewashukia Wakristo, jambo lile lile. Lakini kwa matunda “yao”! Je, hilo lilididimia, ndugu?

²⁰⁹ Ishara ya Roho Mtakatifu ni tunda Lake, tunda la Roho. Vema, ni. . . Vema, sasa, unasema, “Mimi ni ubua, mimi ni kwekwe. Mimi ni ubua jinsi ile ngano ilivyo ubau.” Bali ni aina gani ya maisha yaliyoko ndani yako? Maisha yaliyo ndani yake huzaa miiba, kila wakati kuzozana na kubishana, na machoyo sana na yenye madhara na kila kitu. Mwaona ninalomaanisha? Mwenye kiburi, ona hayo si tunda la Roho. Tunda la Roho ni upole, saburi, utu wema, ona, hayo yote. Ona?

210 Yeye aweza kusema, “Vema, naweza kupiga shangwe kwa sauti kubwa tu kama wewe. Mungu ahimidiwe, Roho Mtakatifu alinishukia!” Hilo huenda ni kweli kwa kila chembe, lakini maisha anayoishi hayaambatani na yale yeye anayonena. Ona? Yeye alikuwa gugu, yeye alikuwa gugu tangu mwanzo.

211 Sasa, tumefikia swali kubwa sasa, ona, kuhusu *kuchagua*, mwaona. Kwa hivyo hilo ni . . . Yakupasa uwe hivyo. Mwfahamu hilo.

212 Wao walikuwa kombe tangu mwanzo; *yeye* alikuwa ngano tangu mwanzo. Kwa hivyo ukame ukashika, mvua ikanyea wenye haki na wasio haki. Vema, mwalifahamu?

[Ndugu fulani auliza, “**Na matunda ya mhubiri je, hayo . . . hayo ni kuhubiri Neno?**”—Mh.]

213 Huyu, mhubiri, hata hivyo, kama alisimama juu pale na kuhubiri Neno kama Malaika Mkuu, ona, alifahamu siri za Biblia, na kuwa mchungaji mzuri sana, alienda na kuwatembelea watu na mengineyo kama hayo, yeye bado aweza kuwa amepotea. Ona? Ni tunda lake linalomtambulisha kila wakati, ndugu. Ona? Yeye, haijalishi ni mzuri jinsi gani au yeye yu nani yapasa yeye awe na Roho Mtakatifu maishani mwake. Ona?

214 Sasa, si Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo na kusema, ‘Bwana, sikufanya unabii (kuhubiri) kwa Jina Lako, na nimefanya miujiza kwa Jina Lako?’” Yeye alikuwa amenena kwa lugha, alikuwa ametenda miujiza, ametoa tafsiri, mambo ya siri za Mungu, na mambo hayo yote pale; Yeye alisema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, sikuwajua ninyi kwamwe.” Ona nina maanisha?

[Ndugu Taylor auliza, “**Vipi mtu atoaye u-ujumbe wa uongo? Namaanisha, yeye—yeye adhania yu sahihi bali anahubiri vibaya**”—Mh.]

215 Vema, naamini kuwa mtu huyo yu mnyofu, kama ndugu anayeketi hapa aliyetaka kurudia . . . kufuatilia mambo haya hivyo. Kama mtu huyo amechaguliwa na Mungu, naye daima amekuwa akiletwa mbele ya Kweli, yeye ata—yeye ataitambua. Ona, “Kondoo wangu wanajua sauti Yangu.” Mnafaha . . . Wafahamu ninalokusudia, Ndugu Taylor? Je, hilo ndilo unalonena? Ona?

216 Sasa, kwa mfano, tuseme Ndugu Crase—Crase—Crase, tuseme yeye alikuwa mhubiri Mbatisti naye hakujua lo lote kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, wala hakujua lo lote juu ya mambo haya, karama za Roho, naye alikuwa mhubiri Mbatisti mzuri, mwaminifu. Ona? Lakini punde si punde, hii imjie. Nami naamini kuwa kila mwana wa Mungu atakuwa . . . kila wakati utawavua hata Yeye ampate. Ufalme ule hauji hadi Mapenzi ya Mungu yametendeka. Naam. Na hakuna hata mmoja atakayeangamia, mwaona. Sasa, ona, hiyo ndiyo njia.

²¹⁷ Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu atupaye juya baharini na kulivuta pwani. Yeye alipofanya vile, akapata za kila aina. Yeye aliweka samaki, na ng'amba na kasa wakarudi majini. Yeye alilitupa tena, akapata zaidi, labda akapata samaki mmoja. Lakini Yeye aliendelea kuvua hata wote walipovuliwa. Mwafahamu ninalokusudia sasa?

²¹⁸ Lakini samaki huyo alikuwa samaki tangu mwanzo. Aliwekwa tu kwa matumizi ya Bwana, hiyo tu, wakawekwa kwenye kidimbwi kingine bora, kisafi zaidi. Lakini Yeye alikuwa bado anavua samaki katika hiki kidimbwi chenye vyura hata atakapowavua samaki wote toka humo. Mwaona ninalokusudia? Unafahamu ninalokusudia, Ndugu Taylor. Yakupasa ujue kwa yako pale.

Vema, sasa:

113. Je, yeye yule. . . Je, yeye kila mara huwa na mamlaka juu ya Roho kuhusu wakati wa kutenda na jinsi ya kutenda?

²¹⁹ Naam bwana. Naam, bwana, Roho Mtakatifu huongoza. Naam, bwana. Ana mamlaka juu yako nawe una mamlaka juu Yake, na hatakufanya kamwe utende cho chote kinyume cha Maandiko. Atakufanya. . . “Roho hana mazoea mabaya na kukosa adabu.” Naam. Vema.

²²⁰ “Toka kwa yeye akupendaye. . .” Naam, hilo, tutapata hilo. Vema, sasa tutarukia lingine hapa tuone tuliko.

²²¹ Sasa hilo lilikuwa na msingi. Sasa—sasa, ninapotaja haya sasa, iwapo kuna swali. . . Kulikuwa na swali zaidi juu ya hili? Sote twafahamu? Sisi tunafahamu jinsi tunavyoliamini sasa?

²²² [Ndugu mmoja asema, “Nina swali moja.”—Mh.] Endelea. Bado lahusiana na haya? Sawa. [“Naam, kwa hilo pale. Nilisitasita kidogo, lakini. . .”] Usisitasite, hili ni—hili ni. . . [“Ulikuwa unanena kuhusu mtu anayehubiri, na kama yeye hahubiri Ujumbe ambao Kristo alihubiri, na haijalishi nini chatendeka katika huduma yake. Yeye akutanapo na Kweli naye aikatae, nini basi?”] Yeye amepotea. Niradhi kwa dakika moja hivi kwa. . . [“Kuhusu kuchaguliwa asili na kumchagua aje ulimwengu?”] Naam. Naam. Ona? [“Basi jambo ni kwamba, yeye hakupaswa kuwa hivyo?”] Hakupaswa kuwa hivyo tangu mwanzo, ona, “Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu.”

²²³ Kwa mfano, hivi, ni jambo lile lile katika Waebrania 6. Ona? Watu hufasiri kwa kosa sana Andiko hilo, wao hudhani “haiwezekani.” Yeye alisema, “Haiwezekani kwa wale ambao wamepewa nuru na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, wakianguka.” Ona, hawampokei. Yeye asema, “Haiwezikani kwa wao waliokwisha kupewa nuru na washirika wa Roho Mtakatifu, wakaanguka baada ya hayo haiwezekani kuwafanya upya tena wakatubu, kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili na kumfedheni kwa dhahiri; wameihesabu

ile Damu ya agano ambayo Yeye alisulubiwa kama ‘kitu ovyo’ kuzifanyia jeuri kazi za neema.”

²²⁴ Vema, kwangu, ni ufunuo. Hakika. Ni kama tu Matendo 2:38, na Matendo . . . na Mathayo 28:19. Yawapasa tu mwiielewe, mwaona.

²²⁵ Sasa tazama, liko hapa, jambo lile lile. Vema, sasa, yeye anawaambia Waebrania. Ona? Sasa endelea kusoma sura ile yote, hata wanapoendelea na kusema, “Kwa kuwa ni jambo la kutisha kuanguka katika—kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.” Sasa, hapa kuna mtu kama tu mwamini mkwamia mpakani. Hapa, hapa kuna . . . Hapa, jambo lile lile lilikuwa hapa, mfano kamili niuonao niani mwangu.

²²⁶ Mungu aliita Israeli toka Misri. Watu hawa wote wakatoka, kila mmoja wao alikuwa amekombolewa, wakavuka Bahari ya Shamu wakaingia jangwani. Sivo? Bahari ya Shamu . . . walipojitayarisha, wakasikiza ujumbe wa Musa, wakaanza kupiga hatua, (kuhesabiwa haki) waligeuka, wakaanzia hapa.

²²⁷ Wakafika kwenye Bahari ya Shamu, (ile Damu), na wakapitia katika Bahari ya Shamu, na nyuma yao wale wasimamizi wamelala, wafu. Walikuwa tu umbali wa siku tatu toka kwa ile nchi ya ahadi wakati ule. Ona? Walibakiza hizo tu, haipati maili arobaini, ona. Kwa hivyo ndio hao, siku mbili tu zingewafikisha kule vizuri.

²²⁸ Hilo ndilo nakusudia kuhubiri kule Phoenix katika muda wa siku chache tangu sasa, kwa mkutano wa Wafanyi Biashara, *Kukaa juu ya Mlima huu*. Lakini Yeye aliwakawisha papo hapo kwa miaka arobaini kwa sababu wao . . . Enhee! Ona?

²²⁹ Kwa hivyo wao walifika hapa nao wakatazama nyuma, (wametakaswa), “Ee, haleluya! Bwana asifiwe! Mungu atukuzwe. Haleluya! Ndicho hicho kile kitu cha kale ambacho wakati mmoja kilinitatiza, kimekufa. Ile sigara ya kale ambayo wakati mmoja nilivuta imekwisha. Kileo cha kale nilichokuwa nikinywa chote kimo katika bahari ya Damu ya Yesu Kristo. Ee, Mungu atukuzwe! Haleluya!”

²³⁰ Kila mmoja wao akaja humu kumiliki Kanani sasa, wakavuka Yordani. Vema, yeye alichukua waakilishi toka kila kabila. Sivo? Naye akawatuma kule ng’ambo. Vema, wengine wao walisema, “Aaa, aa, aa, hatuwezi kufanya hilo. La, ni—ni . . . Naam, twaonekana kama panzi kando yao!” Ona?

²³¹ “Sasa, ningehubiri haya kwa kanisa aina gani kama nilifundisha huyo Roho Mtakatifu na upuzi huo wote hivyo? Naam, ningekuwa na viti vitupu. Wamethodisti wangu wangeondoka, Wabatisti, Wapresbiteria wangu.” Acha waondoke. Wao walikuwa mbuzi tangu mwanzo! Unataka kondoo, ona. Ona? Wewe huwachungi mbuzi. Wachungaji wa kondoo! Kuna faida gani kuwachunga mbuzi huku . . . ? . . . na kunao kondoo wa kuchungwa? Ona? Na hapa—hapa, mko ndani

humu, ona. Mimi kila mara nilisema ningehubiria vile vizingiti vinne na nihubiri Kweli, lile Kanisa. Naam, bwana, niye humu.

²³² Lakini ona sasa, alifanyaje? Walirudi, na Yoshua na Kaleb, asilimia mbili, au asilimia kama hiyo... wawili kati ya... wawili kwa kumi na wawili, mbili kwa kumi na mbili. Vema, walikuwa kumi na wawili, hao wangekuwa wawili kati ya kumi na wawili, wawili kati ya kumi na wawili walimwamini. Wakaenda moja kwa moja katika ile nchi ya ahadi, kasema, “Wee, hapa ni mahali pazuri kuishi.” Mzee Yashua na Kaleb, wee, wao walikuwa wakitumainia lile Neno; Mungu aliwapa, kasema “hiyo ni yenu.” Wakaenda kule, wakakata kichala kikubwa cha zabibu, ndio hawa wanakuja wakiikokota hivi. “Shime, wenzangu! Hapa ni mahali pa ajabu! Onjeni,” ona, zabibu karibu ukubwa *huu* mviringo.

²³³ Na, ee, jamani, walipoziona, kasema, “Aa, hatuwezi kufanya hivyo.” Waliporudi, walisema, “La, ndugu, huyu Musa ametuleta hapa jangwani,” huyu Roho Mtakatifu, mwaona, ambaye yeye aliwakilisha, “ametuleta hapa jangwani. Sisi hapa, huduma yetu imeharibika, nasi hatungefanya jambo kama hilo.”

²³⁴ “Kurudi nyuma,” ona, “wao waliopewa nuru, wakahesabiwa haki kwa imani, wakatakaswa.” Ona, walivuka haya madhabahu ya pili na wakaiona ile nchi ya ahadi. “Sisi tuliopewa nuru na tumekuwa... tumeonja karama za Mbinguni.” Ona, “kuonja” Hiyu. Wao wakayaleta. Twaona Hayo ni sawa. Sisi hakika tunayaona Hayo. “Kuonja karama za Mbinguni, kufanywa... au mshirika wa Kitu hiki, mwaona, huyu Roho Mtakatifu, wakamshiriki.”

²³⁵ “Hilo ni zuri, wee, mtazame mtu hu—huyo. Mbona, najua yeye alikuwa kipofu, sasa yeye aweza kuona. Tazama huyo mzee... Wee, nini kilimpata mtu huyo? Hamna mtu aliyefikiria kijana yule pale asiye kuwa na elimu... ndiye huyo pale amesimama na ule Moto ulimwenguni.” Mwaona? Ona? Ona?

²³⁶ Kisha wakaanguka, ona, na wana... kuwafanya upya tena, warudie tena kutubu, warudie kuhubiri toba badala ya hayo ambayo Yeye alisema kwanza, kuweka... hebu... Mwajua, kuhusu kuweka tena msingi wa matendo mafu hata wakatubu, na kadhalika. Tutaifanya hayo, Mungu akitujalia, mwaona. Ona, tutaifanya hayo. Tutarudi na kuweka msingi huu tena basi, lakini kurudia tena kutubu wenyewe, kutubu kwa ajili ya kuweko kule kamwe. “Nasikitika naliwahi kuwa kule kamwe,” na kuhesabu ile Damu ya agano ambayo yeye alitakaswa kwayo kama kwamba ilikuwa “jambo ovyo,” na kuifedhehi kazi ya neema. Yeye ameenda ndugu! Hivyo tu, Yeye amekwisha. Ona?

²³⁷ Vema, sasa, ona, haiwezekani kwa mwana mteule kufanya hayo. Yeye hatafanya hayo. “Kondoo wangu waijua Sauti Yangu.” Kama wanaitwa Kanani au po pote pale, wataenda. Ona? “Kondoo wangu waijua Sauti Yangu.”

[Ndugu fulani auliza, “Nao wanapaswa kuamini Matendo 2:38, pia, sivyo?”—Mh.]

²³⁸ Hao wangeamini hayo, kila fungu ndogo la Maandiko, wangelishika lote. Hiyo ni kweli kabisa, ndugu.

114. Kuna aina mbili, ku—kuna aina mbili za lugha za Biblia? Kuna tofauti kati ya lugha inayonenwa katika maombi ya kibinafsi, na kanisani ambapo kufasiri kwahitajika? Kwenye ile Siku ya Pentekoste zile lugha zilieleweka kwa watu wa mataifa mbalimbali; lakini katika I Wakorintho 14:12, lugha zisizojulikana zinanenwa kwa Mungu, si kwa wanadamu. I Wakorintho 13:1 inaonyesha mtu huyo... (W-a-k-o-r, nakisia hiyo ni Wakorintho 13, nini...)...kwa mtu kama huyo na zingine kwa malaika.

²³⁹ Ee, naam. Ona? Vema, ita...Sasa, ndugu, ye yote yule, ume—umejijibu mwenyewe hapa. Ona? Ona:

Je, kuna aina mbili mbalimbali za lugha? (Kuna lugha nyingi mbalimbali. Ona?) Je, kuna aina mbili mbalimbali za lugha katika Biblia, lugha mbili mbalimbali?

²⁴⁰ Kwenye Siku ya Pentekoste kila taifa chini ya Mbingu lilikuwa pale na lugha. Ona? Vema.

Pia, kuna tofauti kati ya lugha zinazonenwa katika maombi ya kibinafsi na makanisani ambapo kufasiri kwahitajika? Naam.

²⁴¹ Paulo alinena hapa pia katika Wakorintho ulikokuwa ukiuliza hapa, naye alisema, “Kuna lugha za malaika na kuna lugha za wanadamu.” Sasa, lugha za malaika ni mtu anapoomba yeye—yeye binafsi pamoja na Mungu, pekee. Lakini yeye anaponena lu—lugha, yapasa ifasiriwe kanisani, kwa kulijenga kanisa. “Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali yeye anenaye...yeye ahutubuye hujijenga kanisa.” Kwa hivyo yeye alisema, “Heri ninene maneno matano kwa akili zangu, kuliko elfu kumi katika lugha zisizojulikana, ijapokuwa, isipokuwa kuwe na tafsiri.” Ndipo ime—imenenwa basi kwa unabii ambao hujenga. Mwafahamu ninalomaanisha?

²⁴² Naam ile...Basi kuna lugha aina mbili mbalimbali za wanadamu na za malaika. Ona? Na Paulo alisema, “Ijapokuwa nanena kwa lugha za wanadamu na za malaika,” ona, zote hizo mbili, zile ambazo haziwezi...

²⁴³ Sasa, hapo ndipo Wapentekoste, watu wa ishara ya lugha wanaosema, waliniambia, yeye alisena, “Sasa, Ndugu Branham, umefarakanika kabisa.”

²⁴⁴ Kasema, nilisema, “Vema, ukimpokea kulingana na Matendo 2:4 ndipo kila mtu alikusikia ukinena kwa lugha walizozaliwa nazo.”

“Ee!” akasema kisha, “La! la!” akasema.

Nilisema, “Hakika, naam, bwana.”

245 Kasema, “Sasa, Ndugu Branham, umefarakanika kabisa.” Kasema, “Unanena kuhusu ile...” Kasema, “Ni lugha za ‘malaika.’ Huyu ni malaika wa Roho Mtakatifu anayeshuka na kukuzungumzia.”

246 Sasa, laonekana zuri, ona, laonekana kana kwamba lingekuwa na kweli nyingi, lakini si Kweli yote. Shetani alipomwambia Hawa, “hakika hamtakufa,” hilo lilikuwa... yeye alimwambia kweli nyingi, lakini hilo halikuwa Kweli. Ona?

247 Sasa, kasema, “‘Wanadamu na malaika,’ na malaika ambao yeye alikuwa ananena walikuwa...”

248 Sasa, hebu tuone jinsi haingetoa mdundo wa Maandiko. Ona? Sasa, haingeweza “kushirikiana,” nakusudia kusema. Samahani, sikukusudia kusema, “mdundo” wa Maandiko. Namaanisha “kushirikiana” na Maandiko, au “andamana, ambatana” na Maandiko ndilo neno bora.

249 “Sasa, mtu anayenena kwa lugha za malaika,” yeye asema, “hizo ni lugha za Roho Mtakatifu ambazo” yeye alisema, “sasa, wakati wewe, sisi, walimpokea Roho Mtakatifu.”

Nilisema, “Je, ... Lini, ulimpokea wapi?”

250 Vema, yeye akaniambia mahali hasa, dakika na saa. Sikushuku hilo. Ona? Sina ... Mimi si hakimu wake. Ona? Yeye alisema, “Hapo ndipo nilipoinena.” Yeye alijua mahali pale hasa. Kasema, “Kitu fulani kilitendeka kwangu.”

251 Nilisema, “Naamini hilo. Ona? Lakini hilo bado si ishara ya Roho Mtakatifu kwako, mwanangu.”

“Ee, naam!” Kasema, “Hiyo ndiyo!”

Kisha, “La.”

Yeye alisema, “Sasa, tazama, nataka kukwambia jambo fulani ndugu.”

252 Nikasema, “Je, wale watu waliokuwa wakikusikiza, kanisa hilo kule Indianapolis ambako ulisema ulimpokea, je, watu hao walikusikia ukinena Kingereza ukiwaambia kuhusu ufufuo na uweza wa Mungu na kadhalika?”

Yeye alisema, “Ati! la! Nilinena ka—katika lugha zisizojulikana.”

253 Nilisema, “Hukumpokea kulingana na Matendo 2:4, kwa sababu kila ... hakukuwa na neno moja lisilojulikana. ‘Twasikia kila mtu katika lugha yetu wenyewe.’”

254 “Ee,” yeye alisema, “Ndugu Branham, nimeona ambapo umefarakanika.” “Waona,” yeye akasema, “Kuna lugha zilizo za malaika, unapompokea Roho Mtakatifu,” kasema, “ndipo unanena kwa lugha na hakuna ye yote apaswa kufasiri hiyo,

hiyo—hiyo ni Roho Mtakatifu akinena. Ona? Lakini una karama ya lugha, basi hizo yapaswa zifasiriwe.”

255 Nilisema, “Basi umeweka gari mbele ya farasi. Kwenye siku ya Pentekoste waliweka gari nyuma ya farasi. Kabla hawajampokea Roho Mtakatifu, lugha zisizojulikana, wao walinena kwa lugha zilizoeleweka.” Ona? Kwa hivyo hakika ni

256 Kuna lugha aina mbili. Lugha za malaika, hizo ni mtu anayeomba binafsi kule mahali fulani akizungumza na Mungu, akinena na Mungu katika lugha za kimalaika. Ningewasimulia kisa kimoja sasa hivi, lakini sina wakati. Mwakumbuka mwanamke yule alipoingia katika ule ukumbi, anakotoka Daktari Alexander Dowie, Zion. Mwanikumbuka chini kule? Na Billy alinijia chini kule kuniarifu niende mkutanoni, nami nikasema, “Billy, rudi.” Nami. . .

Yeye alisema, “Unalilia nini? Kuna mtu aliyekuwa hapa?”

257 Nikasema, “La, bwana. Wewe rudi, mwambie Ndugu Baxter ahubiri usiku huu.”

258 Nami nikapiga magoti nikasema, “Bwana, imekuwaje kwangu?”

259 Na kwa ghafula nikasikia mtu fulani mlangoni, akinena kwa lugha zingine. Nilifikiri. . . Ilikuwa Kijerumani. Nikawaza, “Vema, mtu yule alikuja pale kumchukua. . .” Mwajua, nikakoma, mwajua, kuomba, nikamsikiza yeye nikisimama pale hivi. Nami nikawazia, “Vema, mtu yule atafahamuje hayo kamwe?” Kwa sababu nilimjua mwenye huo mkahawa wa wasafiri, yapata maili tano nje ya mji ule, mwajua. Ilinipasa kuenda nje kule (watu wengi sana kila mahali), mji mdogo. Nikasema, “Vema, hilo ni geni. Lo.” Nami nikasema, “Pale. . . Vema, jamani, umewahi kusikia. . . nini. . . Mtu huyo hata hapumui, ni vigumu.” Ona, nilikuwa nawazia hilo, “Jinsi yeye alivyokuwa akinena kwa nguvu!” Vema, nilisema, huyo, naam, ilikuwa ni mimi! Kwa hivyo nikatulia kabisa, yeye hakusema lo lote. . . akatulia kabisa. Baada ya muda mchache akamaliza kunena kwa lugha, na, ilipofanyika, ilionekana kama ningepitia katika kikosi na kuruka ukuta.

260 Nami nikaondoka na Bill alikuwa anapita lango lile na nikamwita, “Ngoja kidogo!”

261 Yeye akarudi, alikuwa akinywa soda. Naye akasema, “Baba, kuna nini?”

262 Nikasema, “Ngoja kidogo, kwa dakika moja hivi, tutaenda pamoja.”

263 Nikaanza kunawa uso wangu upesi sana. Yeye alisema, “Kuna nini?” Yeye hathubutu kunizungumzia, tunapoenda mkutanoni. Yeye alisema, “Kuna nini?”

264 Nikasema, “Hakuna, hakuna, hakuna jambo lo lote. Endelea tu mkutanoni.”

²⁶⁵ Tukaenda mkutanoni, Ndugu Baxter alikuwa ameketi pale akipiga wimbo, “*Hamna neno kati ya nafsi yangu na Mwokozi.*” Yeye akaja, akasema, “Whiu! Tulidhani hutakuja!”

Nikasema, “Shiii.” Nikaenda mle na kuanza kuhubiri.”

²⁶⁶ Nilipomaliza kuhubiri, yapata wakati nilipomaliza kuhubiri, vema, jamani, mtu fulani karibu abomoe upande wa nyuma wa lile jengo, nyuma kule katika ule ukumbi mkubwa. Maikrofoni ikapelekwa kule, na kulikuwa na mwanamke nyuma kule aliyekuwa akitembea juu na chini ya hayo marefu ya kanisa, akipaza sauti kadiri alivyoweza kupaza.

²⁶⁷ Ikawa, yeye alikuwa na TB, na alikuwa ameondoka Twin Cities, St. Paul, motokaa ya kubebea wagonjwa haingembeba kwa sababu waliogopa mapafu yake yangepasuka. Daktari alisema, “Lo lote, mapafu yalikuwa kama masega,” kasema, “kama yangepasuka angekufa. Hayo tu.” Na baadhi ya watakatifu wakachukua motokaa zee aina ya Chevrolet ‘38, na kuchukua kiti cha nyuma na kukitengeneza, wakamweka ndani mle nao wakashika njia wakaja. Nao wakagonga kilima au cho chote kile chini pale, naye akaanza tu kutema damu papo hapo, naye. . . nayo ilikuwa inapitia kwa mapua yake na mambo kama hayo. Akaanza kufifia kabisa, hatimaye. . . Yeye hakutaka kufia garini, akawaambia waisimamishe wamlaze kwenye nyasi.

²⁶⁸ Wakamtoa nje. Nao wote walikuwa wamesimama pale, wakiomba, na kwa ghafula yeye alisema kitu fulani kilimgusa naye akaamka. Ndiye huyo akienda, akipiga shangwe barabarani, kwa nguvu alivyoweza. Ndiye huyu kanisani, akitembea tu huku na huko kwenye marefu ya kanisa.

²⁶⁹ Nami nikasema, “Dada, ulikuwa wakati gani?” Wakati ule ule Roho Mtakatifu alipokuwa akinena kupitia kwangu. Ilikuwa nini? Karama.

²⁷⁰ Ilikuwa huyo—huyo komba mzee kulala pale langoni aombewe? Mnyama asiye na maarifa, hana hata nafsi, hajui mema wala mabaya; ona, hana nafsi, (ana roho), hana nafsi.

²⁷¹ Ilikuwa nini? Roho Mtakatifu akiombeana. Mungu alituma karama ulimwenguni, na Roho Mtakatifu hangengoja zaidi kwa hivyo Yeye alikuja tu akanichukua mimi hata pale na akaanza kunena Mwenyewe hivyo, Mwenyewe, akiombeana. Na tulipochunguza saa, katika dakika ile ile ambayo yeye. . . walimweka chini kwenye machela hivyo, walitaka kuona. . . Kwa sababu walijua yeye alikuwa yuafa, ingewapasa waseme alikufa saa, ngapi. Ilikuwa dakika ile ile ambapo Roho Mtakatifu alinishukia pale na kuanza kuombeana, usemi, maneno, ambayo huwezi kuyafahamu, ona, hivyo, akitoa usemi. Huyo alikuwa Roho Mtakatifu akinena.

²⁷² Haikunipasa kujua hayo. Ona, la. Huyo alikuwa. . . labda malaika wake. Tutafikia hayo katika dakika chache, ona, aliyekuja mle na kutoa huo ujumbe, mwaona.

²⁷³ Sasa—sasa, hiyo—hiyo ni sawa. Kuna lugha aina mbili, moja ku- . . .

²⁷⁴ Kuna swali? Vema, kujaribu kujua yale Mungu anasema, mwaona. Sasa, nina . . . ningesema, Ndugu Stricker, katika hayo, kuhusu hayo, usijaribu kuyawazia, ona, ujitolee mwenyewe tu zaidi kwa Roho. Ona? Kwa sababu unajaribu ku—ku—kusema, “Aisee, unasemaje? Ona? Aisee, wewe unanizungumzia? Enhee?” Mwaona, yeye ana . . . ona, yeye anajaribu.

115. Sasa, ni sawa mtu kunena kwa lugha anapoombea wengine madhabahuni?

²⁷⁵ [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] Hebu nione yale niliyoandika hapa, sina budi kutazama. Asipokuwepo mwenye kufasiri, na wanyamaze. Katika I Wakorintho, sura ya kwanza . . . sura ya 14 na kifungu cha 28. Nani ana Biblia? [Ndugu fulani asoma Andiko linalofuata—Mh.]:

. . . Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; . . .

²⁷⁶ Vema. Sasa, asipokuwepo mwenye kufasiri, wakati wo wote katika kanisa, po pote katika kanisa, anyamaze asipokuwepo mwenye kufasiri.

²⁷⁷ Madhabahuni, jambo pekee, kama mtu . . . Mara nyingi mnawasikia watu wakienda madhabahuni. Nilimsikia ndugu mpendwa hivi majuzi madhambhuni, akienda tu na kumtikisa mtu fulani mgongoni, ndiposa wao wenyewe wananena kwa lugha, wakinena kama waliokuwa wakijaribu kuwaonyesha hao la kufanya. Ona, hiyo ni njia ya kujibunia ya kumleta Roho Mtakatifu (kujaribu kumleta) kwa watu. Msifanye hilo. Ona? Jambo la kufanya ni kumwacha mtu yule pekee. Waache wainue mikono yao hata Roho Mtakatifu atakapoingia, mwaona. Ona? Kwa hivyo ni—ni—ni kosa. La, yawapasa wanyamaze katika kanisa, mwaona.

²⁷⁸ [Ndugu fulani auliza, “Ndugu Branham?”—Mh.] Naam, ndugu. [“Tuseme, mtu fulani alikuwa katika ibada na—na mwishoni mwa ibada, kwa kawaida kila mara ujumbe unapokuja, mtu aliye na karama, wataweza kutambua, au wao wanaweza kutambua tofauti kati ya—ya malaika . . . lugha za malaika au ujumbe unaokuja kwake?”]

²⁷⁹ Sasa, hebu tuone . . . [Nafsi tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mradi tu wao watakuja na kuandika jambo lile, waliweke kwenye dawati langu. Ona? Nami ningelisoma tu hivi. Lakini nilipoingia katika chumba kile pale, ndugu, imekwisha. Ona?

²⁸⁰ Na kabla wao hawajakuja humu, wangesimama nyuma pale na kila mtu anyamaze tu awezavyo. Na dada angekuwa pale, Dada Irene, pale kwenye—kwenye madhabahu, akipiga kinanda pale, akiimba “*Msalabani*.” Hatunge- . . . Mabawabu wakienda tu huku na huko. Wakimwona mtu ye yote akinena wangesema,

“Shii, shiii, shii.” Ona? Na kama watoto wana... wangeketi chini vizuri sana na wangesema, “Nyumba ya Bwana, kipenzi. Usifanye hivyo. Yakupasa uwe na adabu katika nyumba ya Bwana.”

²⁸¹ Na mwanamume na mkewe, na wengine wote, wanawaruhusu kuangika makoti yao na mambo kama hayo. Mtu fulani hapa mlangoni wa kuwalaki tu mara tu mlango ufunguliwapo. Wale... na kila kitu tayari kuanza, mwajua, kutengeneza kanisa. Kila mtu apate kiti aketi na wahakikishe kwamba wameketi.

²⁸² Nami nilikuwa chumbani mle, nikiomba, nimekuwa humo labda tangu saa nane au saa tisa alasiri hiyo. Hakuna ye yote aliyenisumbua. Nilienda chini pale na ujumbe wangu.

²⁸³ Ndiposa katika wakati wa kuanza, yule kiongozi wa nyimbo akaanzisha wimbo, “Hebu tufungue wimbo nambari fulani,” kama, “*Msalabani pa Mwokozi*,” na kuendelea hivyo, mwajua, na muendeleze huo hivyo. Ndipo mwimbapo yapata mbili maalum... Hatuweki kamwe wakati mwingi sana katika kuimba; ni Neno. Kama wana kuimba kwa nyimbo, hiyo ndiyo sababu wana nyakati hizi maalum za kuimba nyimbo. Tu—tuna... Neno ndilo jambo muhimu linalowaleta watu, ni nyumba ya maonyo.

²⁸⁴ Ndiposa labda mshirika, kama Ndugu George, Ndugu George DeArk asimame na kuomba. Kisha tungekuwa na ule maalum, kama wa kuimbwa na mtu mmoja au kitu kama hicho. Kisha wakati unafika, mtu fulani ataniarifu wakati wangu wa kuja umefika. Kama umefika, vema, nitakuja moja kwa moja chini ya upako. Ona?

²⁸⁵ Vema, labda juma hilo waliishakuwa na mkutano mahali fulani humu kanisani, walikuwa na mkutano wao wenyewe. Labda kabla ibada haijafunguliwa usiku huo, walikuwa na mkutano. Na hapa kulikuwa... Nilikipata hapa, na kusema, “Imeandikwa hapa kwenye kijikaratasi hiki kuwa kutakuwa na tufani kote nchini humu juma lijalo,” au cho chote kile, waza... mwajua, jambo kama hilo litatukia. “Iliandikwa, ilinenwa kwa lugha, na kufasiriwa na watakatifu wawili wa kanisa hili hapa, Ndugu *Fulani* na Ndugu *Fulani*. Mashahidi wawili walishuhudia hapo, wameandika majina yao hapa. Na iliandikwa, ‘Ingekuwa ni ya Mungu, ni *fulani na fulani*.’” Hiyo ndiyo sehemu yangu ya kwanza.

²⁸⁶ Ndipo nasema, “Vema, tutajitayarishia hili, kila mtu na aombe. Ona? Sasa kuna hitaji maalum, kila mtu?” Mwajua. “Hebu na tuombe.” Tusimame na kuomba. Moja kwa moja kwa Neno, moja kwa moja kwa Neno.

²⁸⁷ Ndipo mara baada ya ibada kwisha, wito wa madhabahuni ulitolewa. Ona? Wito wa madhabahuni ndio tulioutilia maanani sana, ule wito madhabahuni, kuwaleta watu madhabahuni.

Ndiposa baada ya wito wa madhabahuni, labda basi ningeombea wagonjwa.

288 Kitu tu kama hicho. Ibada ile yote ilitwaliwa kwa sababu roho wa manabii humtii nabii.

289 Hilo ndilo nililokuwa nawazia...Mwakumbuka usiku ule nilioona ono wakati malaika yule alinijia? Nilikuwa nimeketi mle chumbani, nikiwaza. Yapata, ee, usiku sana, nikisema, “Roho wa nabii hu-...’ Ingewezekanaje?” Nikatazama Nuru ile ikiangaza, kisha ndiye huyu akija kule hata nilipokuwa. Ona? Hapo ndipo Yeye aliponiagiza mimi papo hapa, ona, kwa mikutano hii.

290 Sasa, la, ni mtu yu—yule anayetoa ujumbe. Hilo ndilo swali lako, naamini, “Mtu anayetoa ujumbe, ange-...ni—ni... Mtu yule anayetoa ujumbe, je angejua ilikuwa malaika wa Bwana au la?”

291 [Ndugu fulani asema, “Sasa, swali lilikuwa, unasema kuna lugha za malaika...” Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Sidhani yeye angeweza. Sasa, ni jinsi tunavyofanya sasa. Lakini, ona, tukiwa vile itupasavyo, ambapo mna mkutano wa kila mara kwa ajili ya hilo, hebu...

292 Ona, kila mojawapo ni huduma. Tuseme, *wewe* unanena kwa lugha, *yeye* anafasiri, na *yeye* anena kwa lugha, *yeye* anatoa unabii; ninyi mu washiriki tu hapa, kanisani, bali mna huduma na mna kitu fulani. Ninyi mnajaribu kuusaidia Ufalme wa Mungu, kufanya jambo fulani kwa ajili yake, ona, na kwa hivyo ninyi ndugu kutanikeni pamoja. Hiyo ndiyo sababu wachungaji, hivi, tunakutanika pamoja, tuna jambo fulani linalotuhusu sisi sote. Ninyi ndugu kutanikeni pamoja, someni Maandiko, na mkanene kwa lugha na kufasiri, na mtoe ujumbe, mwoana.

293 Lakini, sasa, kama mtu huyu, basi, akitambua...Yeye amekuwa mkutanoni, yeye ana karama ya lugha. Vema, yeye afika mkutanoni, yeye anena kwa lugha bali hakuna tafsiri inayotolewa, yule mwenye kufasiri haipati.

[Ndugu fulani auliza, **“Je, ungesema basi kuwa watu wale wanajenga Mwili ule, lakini utume kama vile wachungaji, waalimu, na wengineo, huukamilisha Mwili?”**—Mh.]

294 Naam, hiyo ndiyo sababu yake, kukamilisha. Ona? Hizi zimetolewa kukamilisha, mwaona. Naamini, Ro—Ro—Roho hutolewa kwa kukamilisha, kukamilisha kanisa.

295 Sasa, wao, watu hawa wanaonena, wamejazwa na Roho, hakuna shaka. Sasa, hapa kuna mtu, labda yeye yuanena humu mkutanoni, naye anatoa...Sasa, yeye yuko mbele ya wale wenye kufasiri, ona, na hali hakuna ye yote apataye tafsiri, kuna kasoro. Mfasiri hawezi kujizuia, ona. Yeye—yeye yampasa afasiri kwa kutiwa pumzi kama tu yule anayenena hayo. Naye huenda

ana karama halisi ya kunena kwa lugha, lakini yeye hana karama ya lugha, lugha fulani. Ona, yeye . . .

²⁹⁶ Basi jambo limpasalo kutenda ni, yeye anapotumia lugha hii, ndipo anaona . . . Sasa, kile yeye—yeye hajaribu . . . Kama yeye anajaribu kujishindilia maneno tena, yeye yu mwenye kiburi anayejisingizia makuu. Yeye si . . . Yeye—yeye kwanza amekosea, mwaona, hatafaulu kamwe. Ona, mwadhani, “Vema, Mungu ahimidiwe, mtu yule hataki kufasiri lugha zangu. Ni hayo tu.” Sasa, ona, kwanza yeye amekosea. Papo hapo yeye ana—ana nia baya, kusudi baya. Ona?

²⁹⁷ Lakini kama yeye ni mwema na mpole aseme, “Vema, labda Bwana hakutaka kunitumia mimi katika ibada Yake. Lakini bado nita— . . . Yeye hubariki tu nafsi yangu. Yeye ataka kunitakasa mimi, kujua kuwa mimi niko karibu Naye ninaponena kwa lugha. Kwa hivyo nitaondoka niende katika bustani ya tofaa, ‘Ewe Mungu!’ Na nguvu zile zinaanza kunishukia nami naanza kunena kwa lugha. Nitarudi nimechangamka, mwaona.” “Lo, mwaona, unanizungumzia mimi, Bwana, unanifanya tu niwe mnyofu kwa kunena kwa lugha.” Ona? “Pia, Bwana, leo ingenipasa kuongea na mtu yule. Nisamehe hilo, Bwana. Ni—ni—niliruka jambo fulani ambalo haikunipasa. Baba, naomba unisamehe.” Na, moja kwa moja, aanza kunena kwa lugha. “Ahaa, wee, najisikia vizuri kuhusu hilo sasa!”

²⁹⁸ Mwaona, hilo ni sawa. Ona, karama ya—yako haipaswi kutumika kanisani, lakini ni kukujenga *wewe*. “Yeye anenaye kwa lugha zisizojulikana (zisizojulikana) hujijenga nafsi yake.” Ona? Sasa, kama hakuna mwenye kufasiri, basi . . . Mwaona ninalomaanisha? Ona, ndivyo ilivyo. Kwa hivyo yeye hangejifahamu mwenyewe. Yeye tu . . . Lakini yeye atajua wakati amekosea.

Sasa, basi yawapasa yaendeleo tu pamoja, mwaona, hilo ndilo jambo pekee mwezalo kufanya hadi mtakapoyatenganisha. Hiyoye ndiyo sababu nadhani ni . . .

116. Fafanua I Wakorintho 14:5.

²⁹⁹ Nani ameipata upesi sana? Mmoja wenu ameipata? [Nafasi tupu kwenye ukanda. Ndugu fulani anasoma I Wakorintho 14:5—Mh.]:

. . . ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kuhutubu; maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, kusudi kanisa lipate kujengwa.

³⁰⁰ Vema. “Ningetaka . . . Ningetaka ninyi nyote mnene kwa lugha.” Paulo alikuwa anajaribu kusema . . . Kama kanisa lile, ninyi—ninyi mwe kanisa langu. Baadhi ya makanisa ya Paulo hayakuwa washiriki wengi kama nilio nao papa hapa. Naam, wakati mwingine kumi au kumi na wawili. Ona? Ona? Sasa,

sasa, yeye alisema, “Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha.” Hilo linawaduwa ninyi?

301 Ona, kanisa li—li—lile kanisa ambalo...katika Matendo 19, naamini lilikuwa na wafuasi dazan moja. Ona? Wadogo sana misheni, mwaona. Kwa hivyo kila wakati imekuwa katika uchache, ona. Nami nadhani ilisema pia kulikuwa na idadi hiyo, wanaume na wanawake, dazan moja, mwaona, mle.

302 Sasa, mki—mkiangalia hapa, yeye alisema, “Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha. La—laiti nyote mngelinena, nyote mnene kwa lugha, mjazwe tu na Roho Mtakatifu hata mkanene kwa lugha. Lakini,” kasema “lakini zaidi sana mhutubu; isipokuwa ifasiriwe, kuweko tafsiri.”

303 Inasemaje pale? Nani... Umeipata pale, vema... ?... Hebu tulisome tena. Sasa sikizeni.

304 [Ndugu fulani aanza kusoma I Wakorintho 14:5, “Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha,...”—Mh.] Sasa simama hapo kwa dakika moja hivi, “Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha.” [“...lakini zaidi sana mpate kuhutubu:...”] “Nami nataka zaidi sana ninyi nyote mhutubu.” [“...maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha,...”] Sasa simama kwa dakika moja hivi.

305 Sasa kipi kilicho kikubwa kuliko kuhutubu? Hapo ndipo ulitaka nikomee? [Ndugu fulani asema, “Nilikuwa tu nasema, ‘Hiyo ilikuwa tofauti...?’”—Mh.] Naam. Ona? Naam. Ona? Sasa, hapa ndipo...

306 Sasa, unasema kwa mfano, sasa, tuna watu wawili wajinga kati yetu usiku huu. Hawajui lo lote kuhusu haya, nami niingie nanyi mlikuwa mna-...tulianza hapa katika mkutano huu, na—na mkaanza tu kunena kwa lugha, kila mmoja wenu akinena tu kwa lugha, akinena kwa lugha, na kunena kwa lugha, akinena kwa lugha. Basi, vema, ni nini? Ona, mtu mjinga asema, “Enhee! Wote wamerukwa na akili?” Ona? Lakini mmoja akihutubu, ona, ndipo yeye anasema jambo fulani analoweza kufahamu.

307 Sasa, endelea ukasome iliyobaki sasa. [Ndugu anaendelea, “...isipokuwa afasiri,...”—Mh.] Naam. Sasa, “isipokuwa,” Ona. Ni—ninge...wale ambao—wale ambao wanahutubu ni wakuu kuliko yeye anenaye kwa lugha *isipokuwa* haya yafasiriwe. Sasa, endelea, ona. [“...ili kusudi kanisa lipate kujengwa.”]

308 Sasa, kwa maneno mengine, naam, kanisa...Mtu huyu hapa...Hapa, kuna wengi *hapa* wajinga, mmekeki tu kati yetu usiku huu; tunafanya mkutano huu. Sisi sote tuko ndani humu tukitafuta...tukitaka kumjua Bwana, ninyi nyote mkaanza tu kunena kwa lugha. Hakuna mtu aliyesema lo lote, mkaanza tu kunena katika lugha. “Nami nataka ninyi...nataka... Hilo lingekuwa jema,” Paulo alisema. “Ninyi nyote mgalinena kwa lugha, ingekuwa sawa.” Lakini vipi kama baadhi yenu

wangehutubu, waamke na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Kuna mtu anayeketi hapa na yeye ni mgeni kati yetu. Jina lake ni *John Doe*. Yeye anatoka mahali *fulani*. Yeye amemwacha mkewe na watoto wanne pale. Yeye yuko hapa usiku huu kwa sababu anataka msaada. Leo alienda kwa daktari kule Memphis, Tennessee. Naye alisema. . . Daktari akamwambia alikuwa na ugonjwa wa kansa ya mapafu. Yeye yuafa.”?

³⁰⁹ Yeye alisema, “Wote wakinena kwa lugha na mjinga aje kati yao, yeye angesema. . . ndipo yeye atasema, ‘Si ninyi nyote mna vichaa au ni wenda wazimu? Lakini kama mmoja angehutubu na afunue siri za moyo, ndipo wataanguka chini, waseme, “Hakika Mungu yu pamoja nanyi!” Ona, hilo ni. . .

³¹⁰ Vema, sasa, hapa. Sasa mnanena kwa lugha, lakini mmoja afasiri, kasema, “BWANA ASEMA HIVI,” akifasiri, ‘Kuna mtu anayeketi kati yetu, aliyeacha mke wake, alikuwa kule Nashville lea,” au Memphis, au ko kote kule, “naye ana ugonjwa wa kansa ya mapafu. Amekuja humu, na jina lake ni *John Doe*,” *fulani wa fulani* hivyo. Ona?

³¹¹ “Isipokuwa ifasiriwe.” Ona, ndipo yeye ajenga. Ona? Ndipo wao watasema. . . Ndipo mtu yule ataondoka, asema, “Hebu niwaambieni jambo fulani, usiniambie Mungu hayuko pamoja na watu hao kule. Hakika! Watu wale hawanijui hata kidogo.” Ona?

³¹² Kwa hivyo tunataka karama za unabii pamoja na karama za kunena kwa lugha. Lakini, katika kunena kwa lugha, ona, yapasa kuwepo tafsiri. Ndiposa inapofasiriwa, ni unabii. Ona? Ni unabii. Sasa, nina swali hilo humu katika muda wa dakika moja hivi, kwa hivyo ni—nitalipata upesi iwezekanavyo. [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]

117. Mathayo 18:10. Mathayo

[Ndugu fulani asoma Mathayo 18:10—Mh.]:

. . . msidharau mmojawapo wa wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika—malaika zao mbinguni sikuzote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni.

³¹³ Vema. Sasa, ndugu yule, ye yote yule, kwa maana hakuna majina, vijikaratasi vidogo tu, mwaona, aliyesema hili. Nina hakika mimi. . .

³¹⁴ Sasa, ungechukua njia mbili yayo, mwaona. Lakini nafikiri kufasiri, kama uliniuliza mimi, “Fafanua hili,” ninafasiri hili hivi.

³¹⁵ Sasa, ninyi fungueni 2 Wakorintho, mtu mmoja, 5: 1, inasema haya, “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, . . .” Mwajua ilivyo, ona. “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunalo jengo.” Mwajua, “linalotungoja.” Vema.

316 Sasa, basi Yeye ange-... Ungalichunguza, katika Mathayo 18:10, Yeye alikuwa akinena kuhusu kuwachukua hawa “watoto” wadogo. Walikuwa watoto wadogo, vijitoto, vya umri wa miaka mitatu au minne, akawachukua. “Wakamletea watoto wadogo, mtoto.” *Watoto* linatoka kwa neno “mtoto.” Na mtoto ni mtu mdogo—mdogo—mdogo, si mtoto mchanga ila tu kati ya huyo na kijana mwenye umri wa kubalehe. Ona? Hajajua bado kujiamulia mwenyewe.

317 Sasa, Yeye alisema, “Angalieni *msidharau*.” Kama ungechukua hasa tafsiri halisi ya neno hilo, ni “msiwaudhi.” Ona, “Kuudhi mmojawapo wa hao.” Kumuudhi mtoto, haiwapasi kufanya hivyo kamwe. Wao ni watoto, hawajui. Ona?

318 Na sasa, tazama, kasema, “Kwa sababu wao... malaika zao sikuzote huutazama uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni.” Mwaona? Katika maneno mengine, “Malaika zao, wajumbe wa—wao, miili yao, miili yao ya kimalaika watakayoiendea wakifa, sikuzote huutazama uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni.” Ona?

319 Sasa, “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo tayari.” Sivo? Hilo ni mwili.

320 Tazama hapa. Laiti ngingekuwa tu na wakati wa kueleza haya! Hakika, najua ni—nitaupata. Lakini, hapa, hebu niwape tu ili iwe kwenye kanda, na mtaipata haidhuru.

321 Tazama, usiku mmoja Petro alikuwa gerezani. Walikuwa na mkutano wa maombi nyumbani mwa Yohana aitwaye Marko, ona. Na kwa hivyo Malaika wa Bwana akaingia, hiyo Nguzo ya Moto, Nuru ikashuka na Petro aliwaza yeye alikuwa akiota ndoto alipoona Nuru hii ikinijia. Ni... Biblia ilisema, “Ilikuwa Nuru.” Ona? Nami naamini ndiyo ile ile iliyo pamoja nasi, ona, Yeye akashuka. Na tukiingia katika shida ile ile, labda jambo lile lile litatendeka. Ona? Akaingia ndani mle, na kwa hivyo Yeye akasema, “Njoo, nifuate Mimi.”

322 Kwa hivyo Petro aliwazia, “Ninaota ndoto sasa, kwa hivyo nitaona tu nini maana ya ndoto hii.” Kwa hivyo yeye akaenda moja kwa moja kupitia kwa wale walinzi, na kuwazia, “Enhee. Sasa, tumepita hapo, mlango ukawafungukia wenyewe.” Wakatokea kwa mlango uliofuata, ukawafungukia wenyewe. Wakapitia kwenye milango ya mji, na ikajifungua yenyewe. Naye bado alidhani anaota ndoto. Kwa hivyo yeye aliposimama nje pale, na kusema, “Vema, niko huru, kwa hivyo nitaenda tu kwa nyumba ya Yohana aitwaye Marko kwa ushirika.”

323 Walikuwa nyuma kule, “Ewe Bwana, mtume Malaika Wako amwokoe Petro.”

324 Na yapata wakati ule kitu fulani kikafanya [Ndugu Branham abisha—Mh.]. Maskini msichana yule akaenda mlangoni na kusema, “Nani huyo?” Akainua kile kibao kidogo, kasema,

“Naam, ni Petro!” Kwa hivyo yeye akarudi, kasema, “Enyi, hebu—hebu acheni kuomba sasa, Petro yuko pale.”

Yeye alisema, “Ee, lo! Endelea,” kasema, “mme—mme—mme...” Ona?

³²⁵ [Ndugu Branham abisha tena—Mh.] Kasema, “Fungueni!” Ninataka kuingia, ona,” Na kwa hivyo yeye akasema...

Kwa hivyo yeye akarudi, kasema, “La, ni—ni Petro aliye mlangoni.”

³²⁶ “Ee” wao wakasema, “tayari wamekwisha kata kichwa chake, huyo ni malaika wake mlangoni. Ona, maskani yake ya Kimbinguni, yeye amekwisha kuipokea, kwa kuwa haya ya dunia hii yalikuwa yameharibiwa, kwa sababu yalikuwa yakimngoja aende Mbinguni.”

³²⁷ Yale niliyoona juzi katika ono hilo, mwajua, waliovuka. “Nyumba iliyo ya maskani ya dunia hii ikiharibika, tunalo jengo lingine.”

³²⁸ Na maskini watu hawa ambao hawajatenda dhambi bado, mwaona... Ona?

³²⁹ Mtoto mchanga—anapoumbika tumboni mwa mama, mara tu awekwapo mle... Ona? Ona? Lakini kwanza ni roho. Na roho yule anapoanza kuchukua mwili, chembechembe ndogo ya uhai inanza kuwa na mwili, na mara tu iangukapo toka kwa... Sasa, tumboni, kuna misuli midogo, inayotapatapa na kurukaruka. Twajua hilo. Hizo ni chembechembe hai. Kama tu unavyochukua unyoya wa farasi na kuuweka majini, utalea na kuenda, na ukiugusa utaruka. Hivyo ndivyo mtoto mchanga alivyo.

³³⁰ Lakini mara tu azaliwapo duniani na kupumua pumzi yake ya kwanza, anakuwa nafsi hai. Ona? Kwa sababu mara tu mwili wa duniani uzaliwapo ulimwenguni, kuna mwili wa Kimbinguni, au mwili wa kiroho, tayari kuuchukua. Na mara tu mwili huu wa kawaida unapoharibika, kuna maskani ya Kimbinguni yanayongoja. “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunalo jengo la Kimbinguni linaloingoa.” Mara tu mtoto a—azaliwapo duniani, katika mwili, kuna mwili wa Kiroho unaomngoja kumpokea. Na mara tu huo mwili wa Kiroho... ule mwili wa kawaida uharibikapo, kunao mwili wa kiroho unaongoja ng’ambo kule. Ona? Tunauita “mwili wa Kiungu.” Ona, mwili wa Kiungu.

[Ndugu fulani auliza, **“Vema, sasa, mwili huu ni... je, huo ni ule usiodumu, unaongoja kufufuka kwa mwili huu?”**—Mh.] Naam. Ona? Naam. Ee, naam. [**“Hiyo ndiyo hali tutakayoishi ndani yake hata tu—tutakapofufuliwa?”**] Naam. Ona? Ona?

³³¹ Haijafafanuliwa bado kwa wana wa Adamu. Naamini... Ni—najua niliiona. Ona? Lakini sijui ni mwili wa aina gani, lakini ningeusikia kama tu ninavyosikia mikono yenu au cho

chote kile. Bila shaka, haya yanaswa kwenye kanda nanyi huenda mkazisikiza miaka mingi baada ya kuondoka kwangu. Mwaona? Lakini . . . Na hayo, vyo vyote vile, nilikuwa—nilikuwa nikiwashika watu wale na kuwakamata, na ilikuwa tu halisi kama—kama mlivyo halisi, na hali haikuwa . . . Hawakula wala kunywa. Hakukuwa na jana wala kesho. Ona, ilikuwa Milele.

³³² Na sasa wakati nyumba hiyo ya maskani . . . waliondoka kule katika mwili huo, wakarudi duniani, na mwili wa aina hiyo ulipaswa kuvaa kutokufa. Ma—mavumbi ya ardhini yaliukusanyikia huo mwili wa Kiungu kwa njia fulani nao wakawa wanadamu tena, ikawapasa wakule kama walivyofanya katika Bustani ya Edeni. Ona? “Lakini nyumba hii ya maskani ya dunia hii ikiharibika, tunayo nyingine tayari.”

³³³ Kwa hivyo hawa watoto wadogo ambao hawana dhambi, ona, hawajatenda dhambi bado, *malaika* zao, “miili” yao (ule ambao Petro alirudi nao . . .) ona, ukingoja. “Huutazama uso wa Baba, Mbinguni,” siku zote wako mbele Zake; hiyo ni kusema “wanajua.”

³³⁴ [Ndugu fulani asema, “Lakini ni pagumu kidogo pale ambapo Yesu alisema, katika sehemu ya kwanza ya ufufuo Wake, Yeye alisema, ‘Usinishike,’ Yeye alikuwa bado hajapaa juu. Kisha alipoingia chumbani ambamo Tomaso alikuwa, anasema, ‘Njoo hapa na utie mkono wako ubavuni Mwangu.’”—Mh.] Hiyo ni kweli, Yeye hakuwa amepaa juu bado. [“Na to—tofauti kati ya hiyo miwili, ambapo mmoja Yeye—Yeye alimwambia asimshike, kisha huku Yeye akamwambia Tomaso aje pale.”] Yeye hakuwa amepaa bado, mwaona. Yeye . . . [“Kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba.”]

³³⁵ Naam, ona, hakupaswa kuguswa hadi . . . baada ya kufufuka Kwake. Yeye alikuwa ametoka ardhini, mwaona. Alitoka ardhini na alikuwa anatembea kati ya wanadamu, lakini Yeye alikuwa hajapaa bado. Yeye alisema . . . alimwambia Mariamu, akasema, “Usinishike.”

Yeye akasema, “Raboni.”

³³⁶ Akasema, “Kushika . . . Usinishike, maana sijapaa kwenda kwa Baba: Lakini napaa kwa Mungu Wangu Naye ni Mungu wenu, kwa Baba Yangu Naye ni Baba yenu.”

³³⁷ Halafu usiku ule, baada ya Yeye kupaa mbele za Mungu, na alikuwa amefufuka katika wafu, alienda mbele za Mungu. Aliporudi, Yeye akamwalika Tomaso aje aguse ubavuni Mwake. Ona, Yeye tayari alikuwa amepaa mbele za Mungu. Naam. Sawa.

118. Sasa, katika I Wakorintho 14, “Ufuateni—ufuateni upendo na kutaka sana karama za rohani, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu.” Webster, asema, “kuhutubu: kutabiri mambo yajayo, hasa kwa kutiwa pumzi ya Mungu.” Je, ujumbe waweza . . . Sasa wao . . . hivyo—hivyo ndivyo Webster alisema na vile ndugu a—aliuliza. Je, ujumbe

unaweza kuitwa “unabii” ambao hautabiri mambo yatakayokuja.

La, bwana. *Kuhutubu* ni “kutabiri”. Ona? Vema.

119. Sasa, I Wakorintho 14:27, naamini kuwa jumbe zote yapaswa zifasiriwe na kwamba hakupaswi kutolewa zaidi ya jumbe tatu katika lugha katika ibada moja.

³³⁸ Hayo ni Maandiko. Nimeyaandika hapa. Bila shaka, hatu-...Tumezoea hayo na tunajua hayo, mwaona. Hayo ni... Naam, bwana, ni... yapasa tu iwe zamu ya watatu. Hayo ni I Wakorintho 14, pia. Ona? Naam, “watatu zamu kwa zamu.” Sasa angalieni hayo katika mikutano yenu, ndugu. Sasa, mta—mtaona hayo yakitendeka sasa, mtaona ya kwamba watu wengi huingia katika hayo. Na msiseme hawajampokea Roho Mtakatifu, sasa. Lakini, mwaona, Paulo alienda chini kule kutengeneza kanisa la Korintho. Sote tunajua hayo, sivyo? Ilimpasa ayatengeneze. Kisha akasema, “Mambo yote na yatendeke kwa ustahifu na kwa utaratibu.”

³³⁹ Sasa, kama mlitambua, Paulo, aliposhuka, yeye sikuzote alikuwa na matatizo na kanisa la Korintho. Hukumpata hivyo kamwe katika... Yeye hakusema lo lote juu ya hayo kwa kanisa la Efeso, yeye angewafundisha usalama wa Milele. Hakuna lo lote juu ya usalama wa Milele katika—katika kanisa la Korintho. Wao walikuwa watoto wachanga daima, wakijaribu, “Mmoja ana lugha, mmoja ana zaburi.” Sivyo? Ona? Na ukiruhusu kusanyiko lako lianze hayo...

³⁴⁰ Kama vile Martin Luther, alijazwa sana na Roho hata akanena kwa lugha. Yeye alisema, katika maandishi yake ya kila siku, alisema, “Nilinena kwa lugha,” akasema, “lakini niki unaisna watu wangu nayo kasema “watatafuta karama lie badala ya Mpeanaji.” Naam, ona, watakuwa wakitafuta hiyo karama badala ya Mpeanaji.

³⁴¹ Hayo ndiyo watu wapatayo, nao ndipo wanaburugika na kujivuna wanapopokea kunena kwa lugha au vitu kama hivyo. Na kama si ya Mungu, basi haita... itakuwa bure. Lakini sisi...

³⁴² Sasa, makanisa ya kisasa hukataa jambo hilo lote, lakini sisi hatufanyi hivyo. Tunaaamini kuwa ni karama ya Mungu na inaweza kuwekwa ndani mle na Roho wa Mungu. Na hayo je, Ndugu Roy? Naam. Ndivyo, bwana. Weka katika kanisa! Ni cha kanisa. Kipawa kile cha kunena kwa lugha ni cha humo, ona, katika Kanisa la Mungu.

³⁴³ Sasa, hebu na tuone hasa swali lake lilikuwa nini hapa. Kasema kuwa:

Naamini kuwa jumbe zote... (naam)... yapasa zifasiriwe, na iwe watu watatu zamu kwa zamu.

³⁴⁴ Hiyo ni kweli, ona, kwa sababu ukiacha...Sasa hebu tuseme, kwa mfano, kama ulikuwa na mkutano nasi tulikuwa tumeketi ndani humu na—na...Sasa, ingefaidi nini kumwachilia *huyu* anene kwa lugha, *huyu* anene kwa lagha, *huyu* anene kwa lugha, *huyu*? Naam, sisi sote tungetatanishwa hata hatungejua tulilokuwa tukitenda. Ona? Watatu zamu kwa zamu, na...kama, Hollin, yeye yuanena kwa lugha, kama yeye ananena kwa lugha...

³⁴⁵ Na yapasa pia hapo kuwepo na mwenye kufasiri. Sasa, kwaweza kuwepo mwenye kufasiri mmoja isipokuwa wewe mwenyewe ufasiri lugha yako binafsi. Sasa wewe... “Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri.” Yeye anaweza kufasiri lugha zake binafsi ambayo ni—ni halali tu kama mtu mwingine anapofasiri. Lakini yapasa kuwepo mwenye kufasiri mmoja kabla lugha haija-...Kama mna kundi la watu wanaonena kwa lugha na kusiwepo mwenye kufasiri, basi wewe omba ili uweze kufasiri yale unayo—yale unayonena.

³⁴⁶ Sasa, usifanye hivyo tu kujiinua mwenyewe, kwa sababu unajijenga mwenyewe wakati huo, mwaona. Usifanye hivyo. Lakini nena kwa lugha ili umtukuze Mungu, upate kulijenga kanisa. Mwaona, yote ni kwa kusudi moja kuu, ndugu. Karama hizi ni za kumtukiza Mungu, kulijenga kanisa, kuwaleta watu kwa Mungu, kuwafanya wao wajue kuwa Mungu yuko pamoja nasi. Yeye si Mungu mfu, Yeye ni Mungu aishiye akitenda kazi kati yetu. Ona?

³⁴⁷ Nasi yatupasa tu tuchunguze hilo kwa makini sana kwa sababu, wee, Shetani achukia hilo sana, mwaona, kuona karama zilizo halisi. Kwa sababu karama ni dhaifu, naye anaweza kushughulikia karama hizo. Jamani, wee, jamani, yeye anaweza kuiga kabisa kila moja yazo. Kwa hivyo hiyo ndiyo sababu...

³⁴⁸ Sasa, tazama, tofauti kati ya karama ya unabii na nabii, zinaachana kwa maili milioni moja. Kabla unabii...Mtu aliye na karama ya unabii aweza hata kuambiwa mbele ya kanisa, watu wawili au watatu hawana budi kupambanua hayo na waseme “hayo ni kweli.” Naam. Lakini si nabii. Ona? Nabii ni huduma. Karama ya unabii ni kipawa. Nabii huzaliwa nabii, ana BWANA ASEMA HIVI, ndugu, na kadhalika. Hakuna cha hiyo, mwaona. Huyu ni nabii. Lakini karama ya unabii, hiyo ni karama, mwaona. Moja ni huduma ya Mungu, nyingine ni karama ya Mungu. Ona? Hiyu ndiyo tofauti.

³⁴⁹ Sasa, jumbe zile, tuseme, sasa, kwa mfano, ingekuwa hivi. Sasa, tutasema, kama Ndugu Junie, usiku huu, yeye hufasiri. Twajua yeye ni mwenye kufasiri. Ndugu Neville ni mwenye kufasiri, ona, hufasiri lugha. Vema, twajua hayo. Sasa, vipi kama tumeketi hapa usiku huu, ee, Roho wa Mungu a—aanze kunena kwa ghafula. Lo, salale! Nasi tume-...tuna haya. Tuna...Ngoja, kanisa litaanza katika dakika chache. Ona, si—

sisi tunakutana kabla tu kanisa halijaanza. Naliweka katika taratibu kama tuliyo nayo hapa.

³⁵⁰ Vema, basi, muda si muda, ndiye huyo Ndugu Ruddell amesimama pale akinena kwa lugha. Twangoja kidogo. Ona? Junie asimama, “BWANA ASEMA HIVI, *Jambo fulani*,” au mtu fulani hapa. Waandishi wanaaandika humu, ona, yo yote yaliyosemwa; enhee, hebu tuyaandike upesi, kwa sababu ni... anayapata moja kwa moja, yale hasa yeye aliyosema. Vema, wao... Yaki—yakikataliwa, basi yafaa uya—uyaachilie tu, ona, ipasue. Lakini yasipokataliwa, yanakubaliwa na watu wawili, basi yanaandikwa hapa, wanatia sahihi ya majina yao kwake. Ona? Hayo—hayo—hayo ni ya kanisa. Hayo ni... Nawaambieni ninyi nyote kwa manufaa yenu, ona, sijui kama walifanya hivyo mwanzoni au la.

³⁵¹ Na muda si muda, pale anaruka Hollin, anene kwa lugha. Sasa, mwenye kufasiri huenda akadai ujumbe ule ule, ona, huenda ni jambo lile lile, kitu fulani kitakachotendeka, unabii; ona, jambo ambalo liko karibu kutendeka, au kitu fulani kikupasacho kutenda. Pale anaruka Ndugu Roberson, nyuma, anena kwa lugha. Vema. Huenda ikawa ni ujumbe ule ule, atoe tafsiri ile ile, ona, au huenda ikawa ni jumbe tatu.

³⁵² Sasa, Mungu hatatoa jumbe hamsini katika usiku mmoja. Twajua hayo, kwa sababu ninyi—ninyi hamgezielewa. Mwafahamu? Lakini cho chote kinacholemea kanisa, kama... au kitu fulani linachofanya, ni kwa kujenga kanisa, ona? Ndipo si—singe—singeruhusu zaidi ya hizo, ona kwa sababu lilisema, “Na iwe watatu, zamu kwa zamu,” ona?

³⁵³ Kwa watatu tu zamu kwa zamu, ndipo—ndipo ningesema, “Basi, yaandikeni, mkayaweke mimbarani.” Ona? Ndipo kesho usiku tukutane tena. Ona? Na kama kuna cho chote kitakachotukia tangu sasa na usiku wa kesho, Mungu atakinena kwa mmojawapo wa jumbe hizo. Mwafahamu nipalomaanisha? Na iwe watatu. Nami nadhani sasa, Webster asema, unabii unaweza...

Je, swali...ujumbe waweza kuitwa kuhutubu kama hautabiri yatakayotukia?

³⁵⁴ La. Kama ni kuhutubu, ni kuhutubu, kutabiri jambo fulani litakalotukia. Hiyo ni kweli, pia.

³⁵⁵ Vema, nami nadhani...Sasa, hili ndilo la mwisho hata tutakapofikia haya hapa.

120. Ndugu Branham, je, yo yote ya haya yaweza—yaweza... Ndugu Branham, yo yote ya maswali haya...imepigwa chapa kwa mashine na karibu imefutika, Je, yo yote ya maswa-...Ndugu Branham, yo yote ya maswali haya ambayo hujisikii unaongozwa kujibu au kujishughulisha nayo...au kuyafafanua (naam), kuyafafanua, yaache,

sitaona vibaya hata kidogo: Kazi ya shemasi kulingana na Maandiko ni nini?

³⁵⁶ Vema, ni—ninaamini wana hayo nje pale. Kama ni... Najua ni mmoja wa mashemasi wa kanisa letu. Kwa hivyo wana taratibu ya hayo pale. Yatupasa tupate nakala zaidi yayo na kumpa kila mmojawao wa mashemasi kama hatuna. Nashangaa kama tungepata nakala ya hayo, Gene, moja... au, wewe au Ndugu Leo, au mmoja wao, yapata... chukua kama sita au nane ukawapatie mashemasi wetu. Hizo zinaeleza kazi ile Kimaandiko, yale shemasi anapaswa kufanya.

121. Iwapo tuna unabii au ujumbe katika lugha ambao si taratibu, tutaurekebishaje?

³⁵⁷ Sasa, hilo ni jambo nzuri la tahadhari, ona. Ona? Sasa, akubariki shemasi uliyetaja hili, kwa sababu hili ni jambo zuri. Unataka kulishughulikia kwa uangalifu sana. Sasa, ukitoa... Mtu akija makutanoni mwetu hapa na atoe ujumbe au unabii pasipo taratibu, wanajua wako nje ya taratibu na ita—ita... huenda ikaharibu ibada. Ona? Lakini, hayo yakitokea, jambo bora la kutenda, kwa mashemasi, ni kunyamaza tu. Ona? Kwa sababu nabii aliye jukwaani ndiye aliye... Wewe ni—wewe ndiwe ulinzi wake, wewe ni askari wake, ona, wewe u mlinzi wake hapa. Ona?

³⁵⁸ Sasa, kama ni mtu fulani katika ku-... Kama ni nje ya kusanyiko letu, mtu yule hajafunzwa, ona, hawajafunzwa. Hayo ndiyo tunayojaribu kuyapata ndani humu, ona, ambao tu—tunajua la kufanya. Twajua jinsi ya kufundisha watu wetu. Lakini kama ni—kama si kusanyiko letu, vema, hatujui jinsi maskini mtu yule amefundishwa.

³⁵⁹ Kwa mfano, kama... Billy akumbuka hili, kule Costa Mesa, California. Kila wakati nilipojitayarisha kutoa wito wa madhabahuni mwanamke fulani angeruka juu, akimbie huku na huku kwenye marefu ya kanisa, akinena kwa lugha, naye angeharibu wito ule wa madhabahuni kabisa. Ndiposa ingenibidi tu kutoka nje. Ungeona Roho amekwisha—amekwisha kuhuzunika, mwaona. Hakuna lo lote litakalomhuzunisha Roho wa Mungu kama limefanywa katika taratibu. Ona? [Nafasi tupu kwenyekanda—Mh.]... kabla tu yeye hajajitayarisha kuanza, jinsi angejitayarisha mwenyewe, kwa sababu nilimtazama. Mhudumu ye yote atafanya hivyo aonapo jambo lo lote nje ya taratibu. Ndipo mwanamke huyu alikuwa nyuma kule naye akamwambia Billy, kisha Billy akaniambia mimi nilipokuwa nikija usiku huo, kasema, “Baba, wajua mwanamke huyo aliyevunja u—ule wito wa madhabahuni, usiku muwili?”

“Naam.”

³⁶⁰ Kasema, “Yeye alikuwa ameketi pale,” kasema, “yeye kasema, ‘Mungu atukuzwe, Billy, nina ujumbe mwingine usiku huu!’”

³⁶¹ Vema, sasa, mnaona, nilimtazama kule makutanoni. Kulikuwa na maelfu ya watu pale; hapo ndipo *Reader’s Digest* walipoandika kuhusu kuponywa kwa Donny Morton, mwajua, *Ule Muujiza wa Donny Morton*. Kwa hivyo nilimtazama mwanamke yule, na karibu tu wakati nilipoanza kutoa wito wa madhabahuni, yeye... Sasa, yeye alikuwa hajafunzwa; bila shaka, mwanamke mzuri. Basi akatazama hapa na pale, akaanza kutengeneza nywele zake. Alikuwa amefupisha nywele zake, ona. Kwa hivyo, mwaona, yeye alikuwa wa Assembly au baadhi ya makanisa hayo—hayo yaliyoruhusu hayo. Alikuwa akitengeneza nywele zake. Akainama na kutengeneza soksi zake ndefu, akajitayarisha hivyo. Na yapata wakati huo nilipoanza kutoa wito wa madhabahuni... Nilisema, “Sasa, wangapi humu... wangapi waliomo humu sasa ambao wangependa kuja mbele na—na kuitoa mioyo yao kwa Bwana Yesu.”

³⁶² Yeye akaruka juu. Nikasema, “Keti chini.” Yeye akaanza. Nikasema, “Keti chini!” Ona? Naam, wee, kila mtu... Nilinyamaza tu. Akajifanya kama mwenye hakunisikia mimi, nami nikapaza sauti tena. Alinisikia wakati huo, kwa sababu nilikuwa karibu kutikisa jengo lile na hiyo maikrafoni kubwa iliyokuwa papo hapo. Naye akaketi chini.

³⁶³ Nilisema, “Sasa, kama nilivyokuwa nikisema, wangapi wanataka kuja madhabahuni na kumtolea Mungu mioyo yao?” Nami nikaendelea moja kwa moja na mkutano, ona.

³⁶⁴ Na usiku huo nilipoanza kuendesha motokaa, nikazungukwa. Na hapa kundi la wanawake lilionekana kama kundi la vifaranga, mwajua, “Wewe ulimkufuru Roho Mtakatifu.”

³⁶⁵ Nikasema, “Ati nini?” Nikasema, “Nawezake kumkufuru Roho Mtakatifu kwa kufuata yale... Yake... taarifa za Maandiko?” Ona?

³⁶⁶ Kisha huyu mwanamke akasema, “Nilikuwa na ujumbe moja kwa moja toka kwa Mungu.”

³⁶⁷ Nikasema, “Lakini wewe ulikuwa ukiutoa kwa wakati mbaya, dada.” Nilisema, “Mimi si... ”

“Unasema huo—huo haukuwa wa Mungu?”

³⁶⁸ Nikasema “Singekwambia, bibi.” Nikasema, “Ni—ni—ninaamini ulikuwa hivyo, ona.” Nilisema, “Nitasema hivyo kwa manufaa yako, kwamba, ‘Nasema naamini ilikuwa hivyo.’ Nami naamini wewe u mwanamke mzuri, lakini ulikuwa nje ya taratibu.”

³⁶⁹ Basi kulikuwa na mchungaji amesimama pale. Nilijua yeye alikuwa mchungaji wake, ona. Nami nikasema... Ni—nikasema,

“Kuna jambo moja tu naweza kusema, au ulikuwa katika mwili au una mchungaji ambaye amekufundisha asiyejua lo lote kuhusu Maandiko.” Nikasema, “Yeye apaswa aje akaongee nasi kidogo kuhusu Maandiko. Hilo ni kosa, uko nje ya taratibu. Ulipoteza watu nyingi, usiku wa juzi, na wengine wengi usiku uliopita tena, na ungefanya vivyo hivyo usiku huu.”

370 Na mtu huyu alisema, “Ndugu Branham,” kasema, “Kuniradhi.”

Nilisema, “Wamaanishaje?”

371 Kasema, “Yeye alikuwa na haki kutoa ujumbe huo, wewe ulikuwa umemaliza.”

372 Nikasema, “Mimi nilikuwa jukwaani, na roho wa nabii humtii nabii. Mimi bado niko jukwaani.”

Naye akasema, “Vema . . .”

373 Nilisema, “Mimi bado nilikuwa na Ujumbe. Nilikuwa natoa wito wangu wa madhabahuni, hiyo ni kuwakusanya. Nilitupa wavu, ninauvuta sasa. Usitupe seng’enge yenye miiba kule au kitu fulani kuharibu, ona.” Nikasema, “Nilikuwa navuta wavu wangu.” Na—nami nikasema, “Yeye aliingilia kati ku—kule kuwaleta watu. Ie . . . Ya nini kuhubiri au cho chote kile usipotoa wito na kuwaambia wenye dhambi waje? Ona?”

374 Na akasema, “Vema, ujumbe wake ulikuwa nyuma ya wako. Wake ulikuwa ni nje ya jukwaa . . . Wake ulikuwa moja kwa moja toka kwa Mungu.”

375 Nikasema, “Mtu akii iona kuwa ni mtu wa rohani au nabii na ayatambue yale ninayosema ya kwamba ni Maagizo ya Bwana. Lakini mtu akiwa mjinga, na awe mjinga. Sisi hatuna desturi kama hiyo, wala Kanisa la Mungu,” kumnukuu Paulo, mwajua. Nikasema, “La, bwana, hamna cho chote kipya! Yeye . . . Yesu alisema, ‘Neno la mwanadamu liwe uongo na Langu Kweli.’ Paulo alisema, ‘Lakini hata Malaika wa Mbinguni akija na lingine lo lote ila lile lililo Humu, na alaaniwe.’” Nikasema “Bwana, umekosea kabisa.” Nikasema, “Una kanisa aina gani? Nakuhakikishia ni kundi kubwa la mafarakano. Ona? Kama ungewaruhusu watu hao wafanye hayo unatoaje wito wako wa madhabahuni? Yeye ana huduma, wote wana huduma, lakini mna nyakati za huduma zenu, ona, mlizopewa.”

376 Kwa hivyo ndivyo ilivyo. La, na sasa kama *hilo* likitendeka kanisani mwetu hivyo, hivi, kwa baadhi ya ndugu au dada zetu humu kanisani wanaonena kwa lugha, naam, mashemasi baada ya kanisa, halmashauri nadhani yapasa kuwakuta wote pamoja, na kusema, “Hebu niwarejeshe kwenye kanda, kwa dakika chache, mwaona. Ona? Wewe una . . . Au mchungaji . . .” Au sema, “Ni—nina hakika mchungaji ataka kuongea nanyi. Je, mwaweza kukutana nasi hapa katika chumba cha kusomea kwa

muda mchache, ona, ndugu.” Nenda ndani mle, na uingie mle ndani na kuongea naye vizuri sana. Ona? Kisha useme. . .

³⁷⁷ Lakini, sasa, wote wakiwa nje ya taratibu na wakimsumbua mchungaji, ona, kama—kama wao wanamsumbua mchungaji wenu, basi ninyi wazee mwendeeni na kumwambia, “Hebu kidogo.” Na kama mchungaji akiwapungia mkono muwakomeshe, yeye amekwisha shika roho yule pale, kuwa ni. . . ya kwamba wanavunja roho ya mkutano, mwaona.

³⁷⁸ Kwa hivyo kama mchungaji amekoma na kuinamisha kichwa chake kwa unyenyekevu, msiseme lo lote. Ona? Msiseme lo lote; mpe mchungaji nafasi. Lakini mtazame mchungaji wenu. Akiwapungia mkono hivyo, kuwa mwapaswa kuyakomesha, basi enda pale kwa upendo wa Kikristo, mwambie, “Ndugu, dada yangu,” ye yote yule, “naamini uko nje ya taratibu, kwa sababu unamatiza nabii, waona. Yeye ana ujumbe toka kwa Mungu. Atakapoumaliza ujumbe wake, basi tutaona hilo baadaye.” Ona, kama linamatiza.

³⁷⁹ Lakini kama ni mgeni, naye mchungaji kwa heshima anatulia na kungoja kwa muda mfupi, basi yeye. . . labda yeye ataendelea, mwoana. Kwa hivyo. . . Na ukichunguza, tisini asilimia ya wakati kama huo, tafsiri ile, kila mara ni kunukuu tu baadhi ya Maandiko au kitu kama hicho, ambacho, labda ni mwili kabisa. Mwajua ninalomaanisha hivyo. Ona? Vema.

122. Je, kuna ruksa kwa watu zaidi ya mmoja kunena kwa lugha bila kufasiriwa?

³⁸⁰ La. Yapasa iwe zamu kwa zamu. Ona? Mmoja atoe. . . Mmoja anena, kisha atoe tafsiri. Ona? Ndiposa mwingine akinena, tafsiri; kwa sababu msipofanya hivyo, mwenye kufasiri hatajua yale anayotenda kwa sababu jumbe mbili au tatu hapa zinamjia yeye kwa wakati mmoja, mwaona, na hayo yangemtatanisha. Na Mungu si mwanzilishi wa farakano, mwaona. Kwa hivyo hebu mmoja anene, mwingine afasiri. Ona? Ndiposa. . . Toeni jumbe tatu, lakini hebu kila ujumbe ufasiriwe.

³⁸¹ Ndipo tutakuwa na. . . Tuseme Ndugu Ruddell ananena na Ndugu Neville afasiri, Ndugu Fred na anyamaze. Ona, tupate tafsiri hiyo. Kwanza, yapasa ipambanuliwe kwanza, kuona kama ni ya Mungu au la, kwanza. Ona? Na ni sawa. Sasa, kama Ndugu Rudell akinena, Ndugu Beeler anene, Ndugu Neville anene, maskini mwenye kufasiri ana jumbe tatu mfululizo; basi—basi, atajuaje la kufanya? Ona? Mwache pekee. Toa ujumbe kisha nyamaza, ngoja tu. Hebu jambo fulani lifunuliwe mtu mwingine anayeketi karibu naye; hebu yeye anyamaze, aketi tu hali ametulia. Ona? Ndiposa fasiri na ije.

³⁸² Basi unapofanya hilo andika basi, tazama yale wanaopambanua watasema. Ona? Wakisema, “Vema, ni—ni ya Mungu.” Vema, ndio huo ujumbe, uandike. Ndipo ngoja kidogo. Na punde si punde, vema, ndipo Roho yule anayemwongoza yeye

atanena. Kisha mwenye kufasiri angoja kwa dakika moja hivi, aone yale Roho Mtakatifu atasema. Huyu hapa anatoa ujumbe, mwaona. Halafu ataandika hayo, ona. Na iwe watu watatu zamu kwa zamu.

123. Ndugu Branham, twajua kuwa wewe u mjumbe toka kwa Mungu kwa wakati huu wa kanisa. Ishara zile zile zilizomfuata Yesu twaziona zikikufuata wewe, na sisi tuna... tunafahamu kwa nini wengine wakujuao sana hudhani wewe u Masihi. Je, waweza kueleza tofauti katika uhusiano wako na Mungu na ule wa Kristo?

³⁸³ Vema, najua, ndugu, hilo ni kweli. Ona, lakini tungoje, nina kitu fulani kilichoandikwa kuhusu hilo hapa, kwa mda mfupi. Ona, wakati mwingi imefahamika kwa kosa. Ona? Lakini, sasa, mtu wakati mwingine... Nami nataka baadhi yenu mfungue pamoja nami Luka, sura ya 3 na kifungu cha 15. Mnapofanya hivyo, huenda nikawaambia... Mnapoipata, hiyo ni Luka 3, ni... huenda... iko katika... Hebu tu... Mimi sitaufunga mlango, kwa sababu hakuna ye yote mle. Hebu—hebu niwaambieni hili, ndugu zanguni. Mmelisikia, limeenea kote. Lakini hebuni mimi niwaambieni, ona, haina budi kuwa hivyo. Yapasa iwe hivyo. Kama haingekuwa hivyo ningetubia ujumbe wangu.

³⁸⁴ Sikizeni, ndugu zanguni, nawasihini sana mbele za Kristo kuwa ninyi—ninyi—ninyi shikilia sehemu hii ya utulivu wenu, lakini kama mngekuwa wa kiroho mngefahamu. Ona? Je, hamjui jambo la kwanza kabisa Yeye alilosema chini kule mtoni? Je, hamkumbuki yale Yeye alisema? “Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako...” Ujumbe ndio utakaotangulia kule kuja kwa pili kwa kristo. Hayo ndiyo aliyosema Malaika wa Bwana.

³⁸⁵ Sasa, sasa tazama. Sasa, “Kama Yohana Mbatizaji...” Sasa, ninyi nyote mmesikia hayo. Mmeyesoma katika vitabu, na mmesikia watu waliosimama pale wakimsikiza, na kadhalika, wakati yule Malaika Mwenyewe aliponena ujumbe huo, “Kama Yohana Mbatizaji alivyotangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, wewe umetumwa na Ujumbe huu, utakaotangulia kule Kuja kwa Pili kwa Kristo.” Sasa, “Ujumbe ule.”

³⁸⁶ Sasa, ukichunguza, nami... Maskini Willie kule aliweka jina langu chini ya nyota ile pale, na hiyo ndiyo sababu niliyaruka, mwaona, kwa sababu si—sidhani... Sasa, nitakuwa mwaminifu niwezavyo kuwa, sidhani nina uhusiano wo wote na mjumbe yule, ona. Naam. Naamini kuwa huenda mimi nimetumwa kwa ajili ya sehemu fulani katika kanisa Lake, kusaidia kujenga huo Ujumbe mahali ambapo huyu mtangulizi atakuja, atakayekuja.

³⁸⁷ Lakini naamini, mimi nikiwa jinsi nilivyo, na... Naamini kuwa huu ndio Nuru ya siku hizi, nami naamini unatuelekeza kwa huo wakati unaokuja, mwaona, naamini kuwa huo ndio

Ujumbe ambao yeye alisema chini kule, “Ujumbe ulio nao.” Sasa, ukichunguza Nyota hiyo iliyoonekana nyuma kule, ilikuwa...

³⁸⁸ Hebu niifanye... Najua nina—ninachukua wakati wangu hapa nami nina haya mengine, maswali haya mazuri. Sitaki... Ime—imepita saa nne sasa, kwa hivyo, nami najua mnataka kuenda nyumbani. Ona? Lakini sikizeni hapa. Hebu niwaonyesheni kitu fulani. Je, mnaweza tu—mnaweza kunipa muda mchache zaidi? Sawa, sawa.

³⁸⁹ Sasa tazameni, sasa hebu niseme jambo fulani. Naam, ninyi ndugu wekeni hili kati yenu wenyewe. Ona? Sasa, wekeni hili miongoni mwenu wenyewe. Yanipasa kuwaonyeshea hili kwa sababu ninyi ni wachungaji wangu... ninyi ni wachungaji wangu na kadhalika, mwaona, na—nami yanipasa kutenda hili. Nanyi ni ndugu pamoja nami tukifanya kazi katika Ujumbe huu. Ona?

³⁹⁰ Sasa, kwangu mimi binafsi, kama mwanadamu, mimi niko kama ninyi na mwovu kuliko ninyi. Mi—mi—mimi... Wengi wenu nyote mna malezi ya Kikristo na kadhalika. “Mimi ni mwenye dhambi aliye mkuu,” kama ilivyosema wakati mmoja “kati yenu.” Maisha duni mno, nadhani, ambayo yangaliishiwa, kama asiyeamini na mwenye mashaka, ndivyo nilivyokuwa mimi.

³⁹¹ Lakini tangu utotoni nimejua daima kuwa Mungu yuko, na nilijua kulikuwa na kitu fulani kilichotendeka maishani mwangu. Na hilo, hilo halina shaka, ndugu yangu. Ona? Lakini hebu niseme haya, kuwa kutakuja—kutakuja Ujumbe, na kutakuja mjumbe. Naamini kuwa kama ni mwanadamu ata—atakuwa mtu fulani nyuma yangu. Ona? Itakuwa... Lakini Ujumbe huu ambao ninahubiri ni Ujumbe halisi wa siku hii, na ndio Ujumbe wa mwisho. Mnaona yale ninayofanya, ndugu? Nawawekeni ninyi nyote mahali pale pale nilipo, kwa sababu ninyi mu ndani yake kama nilivyo mimi. Ninyi ni wajumbe wa Ujumbe uu huu.

³⁹² Tazama hapa, nina mfano. Ni—ninafikiri naweza kueleza vizuri kwa mfano. Hebu nifunge mlango huu nusu kwa dakika chache. *Hii* ni Yesu, na *ile* ni Yesu; vema, nitaweka *hii* hapa, Gethesemane, na *hii hapa* na *pale*. Sasa, huwezi... Hata sijawahi kusema hili mbele ya kanisa nje kule. Sasa, kumbuka, ni nuru aina gani (nyota) iliyomwongoza yule mtu aliyekuwa akitafuta hekima, “*kutuongoza sisi kwenye Nuru Yako kamilifu?*”

³⁹³ Sasa nitakatiza hapa kidogo na kuwaambieni kitu fulani. Hebu tung’oe kitu kile... ambacho Willie alifanya pale, ndiposa tuseme ni sahihi. Hebu tukiseme ni sahihi. Siwezi kusema hilo, ndugu. Hayo ni majivuno. Hilo, singeweza... Hata kama

naliadini, singelisema hivyo. Ona? Mtu mwingine akisema hivyo, hiyo ni wao.

³⁹⁴ Lakini, hapa, kama tu nilipoulizwa tu, wavulana wengine, kama wangeshuhudia juu ya baadhi ya mambo yaliyotendeka. Sipendi kuingia mimbarani na kutoa ushuhuda juu ya jambo fulani lililotendeka mkutanoni. Hebu msimamizi au mtu mwingine afanye hivyo, mtu mwingine alifanye hilo. Sipendi kufanya hivyo.

³⁹⁵ [Ndugu fulani asema, “Hata walimjua Yohana na kusema, ‘Wewe u Kristo?’”—Mh.] Naam, ndivyo, ndilo ninalojaribu kufikia. [“Wewe u Nabii yule?”] Yeye alikana. [“Hakusema mmoja wa hao, yeye asema, ‘Mimi ni mtu aliaye nyikani.’”] “Sauti ya mtu aliaye nyikani.” Yeye alijiweka mahali pafaapo.

³⁹⁶ [Ndugu mwingine asema “Walimwuliza kama yeye alikuwa Nabii yule akasema ‘Mimi siye.’”—Mh.] Naam. Sasa... Maana Nabii yule alikuwa Yule Musa aliyenena habari zake. Ona, huyo ndiye Nabii yule, ona. Ona? Lakini alijua yeye mwenyewe alikuwa nani, ona. Lakini aliwaambia, sasa, kuwa... Yeye aliwaambia wao, ona, naye alisema, “Mimi ni sauti ya mtu...” Huyo alikuwa yeye. Yeye—yeye alisema jinsi alivyokuwa. Ona? Lakini alikuwa na...

³⁹⁷ Endelea. [Ndugu fulani auliza, “Kristo alipokuja wakati huo, akimfuata Yohana, walimjia kisha akasema... aliadini naye akawafundisha hawa kuwa Eliya angekuja kabla ya Masihi. Yeye alisema, ‘Na ikiwa mnataka kukubali.’”—Mh.] Huyo alikuwa yeye. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Na Yohana aliendelea kusema, “Mimi si kitu! Mimi si kitu! Sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu Chake!”

³⁹⁸ Lakini vipi Yesu aliponena juu yake? Yeye alisema, “Mlitoka kwenda kuona nani?” Naam. Naam. “Je, mlienda kuona unyasi ukitikiswa na upepo? Au mlienda kutazama nini, mtu fulani aliyevikwa mavazi mororo na anasa na kadhalika?” Kasema, “Kwao wamo kwenye majumba ya kifalme. Lakini mlienda kuona nabii? Nasema naam, na zaidi ya nabii.” Yeye alikuwa zaidi ya nabii, yeye alikuwa mjumbe wa agano. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Yeye alikuwa zaidi ya nabii. Yeye alisema, “Hakujawahi kamwe kuwa na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama yeye hata wakati huu.” Ona?

³⁹⁹ Hivyo ndivyo ilivyokuwa, ona, yeye alikuwa mjumbe wa agano. Yeye ndiye aliyejulisha na kusema, “Huyu ndiye.” Manabii wengine wote walinena habari Zake, lakini Yohana alisema “Huyo ndiye.” Ona?

⁴⁰⁰ Sasa tazama. Sasa tazama. Wale mamajusi walifuata nyota. Nitayarudia kifupi, ona. Wale mamajusi walifuata nyota, wakiuliza, “Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” Mmesikia wimbo ule. “Tumeona nyota Yake mashariki nasi

tumekuja kumwabudu Yeye.” Mmesikia hayo, yasomeni katika Maandiko. Vema:

Kuelekezwa magharibi, ingali inaendelea,
Tuongoze sisi kwenye Nuru yako kamilifu.

⁴⁰¹ Ona, nyota ile ilikuwa ikongoza hata kwenye Nuru kamilifu, kwa sababu nyota ile ilikuwa tu ikirudisha ule mwanga wa Nuru. Hapo ndipo tulipata hili hivi majuzi. Ona? Wangapi walikuwa hapa Jumapili kuona hayo? Mwaona, ndiyo kwanza nimalize kuhubiri hayo. Utukufu wa Shekina ukirudishwa na nyota ile, na nyota huurudisha. Hapa kulikuwa na yule Malaika wa Bwana amesiamama hapa jukwaani akiirudisha kule tena, toka kwa ule Utukufu wa Shekina. Kitu kile kile tu. Ilikuwa pale vivyo hivyo hasa. Kutazama hapa kwa kile halisi, kutazama pale na hiyo kurudishwa upande mmoja hivyo. Ona?

⁴⁰² Sasa tazama hili, sasa, hiyo nyota ilitoka mashariki. Sivyo? Ilikuwa nyota kuu. Vema. Na ni nani aliyekuwa nyota halisi ya kidunia katika wakati wa kule kuja kwa Yesu? Vema, Yohana. Yeye ndiye aliyewaongoza hata kwenye hiyo Nuru kamilifu. Sivyo? Hiyo ilikuwa mashariki Yesu alipokuja. Naam, sasa, kuna nyota ndogo nyingi zinazovuka upeo wa macho hata inapofikia ile nyota ya jioni.

⁴⁰³ Nayo ile nyota ya jioni huangaza jioni. Ile nyota ya asubuhi huangaza asubuhi. Nazo nyota hizo mbili zina ukubwa mmoja na ni za aina moja. Sasa ongeza mbili kwa mbili na umeipata, ona. Naam, basi. Kwa hivyo si. . . Ile nyota si Masihi, yeye anarudisha tu ile nuru ya Masihi.

⁴⁰⁴ Sasa, nyota ile hairudishi nuru yake yenyewe. Nyota inarudisha nuru ya jua. Sivyo? [Ndugu asema, “La.”—Mh.] Enhee? [“Kwa njia nyingine. Mwezi hufanya hivyo; nyota hurudisha nuru zao zenyewe.”] Naam, mwezi. . . Naam, hakika. . . Nakusudia kusema kuwa mwezi hurudisha tu nuru ile. Naam. Sasa, kama—kama nyota hurudisha nuru yake, ndipo nuru yake ingepasa ije toka. . . toka kwa Mungu kwa sababu ni mfano wa barafu fulani. Sivyo? [Ndugu yule asema, “Jua.”—Mh.] Enhee? Jua lenyewe, kutoka kwa jua. [“Jua zilizo mbali sana kuliko jua letu.”] Naam. Nao. . . Tunaarifiwa ya kwamba jua hizo zilitoka kwa jua lile kubwa. Jua lilitupa miali yake na hiyo ndiyo ile miali midogo inayowaka moto kama jua. Kwa hivyo ni jua ndogo kwetu. Sivyo? Nuru ndogo. [“Nyingine ni. . . nyingi ni kubwa kuliko jua letu.”] Namaanisha kwetu *sisi*, ona. Tunaongea kuhusu *sisi* wenyewe hapa. Vema.

⁴⁰⁵ Sasa, kama ni jua kwetu, au zinazotoa nuru, ni sehemu ya ile kuu inayotoa nuru. Ona? Lile jua kubwa hutupea nuru kubwa, ile nuru kamilifu. Jua ndogo, au nyota ndogo, ambazo tunaweza kuona katika miili yetu, huenda zikawa mbali sana kuliko jua li—lile liangazalo, lakini kile zinachorudisha kwetu ni nuru ndogo. Lakini ni shuhuda tu za nuru. Sivyo? Ndipo lile

jua kuu linapochomoza zile jua ndogo hutoweka. Sivyo? Hizo si jua kwe—kwetu sisi, ni za kurudisha kama jua. Mwafahamu ninalomaanisha?

406 Sasa, iliyo kuu zaidi ya zote (asubuhi) inayotangulia kule kuja kwa jua, machweo ya jua na kupambazuka kwa jua ni ile nyota ya asubuhi na ile nyota ya jioni. Sivyo? Mbili za nyota zilizo kubwa sana, ile nyota ya mashariki na ile nyota ya magharibi.

407 Sasa, basi mwaona lilipo? Eliya alikuwa mjumbe kuita, kutangaza kule kuja kwa ile nyota ya mashariki, na alitabiriwa kuwa mpiga mbiu wa ile—ile nyota ya magharibi, au kurudi tena kwa siku mpya baada ya siku hii kwisha. Sasa mnafahamu ilivyo?

408 Kule mashariki, “Kutakuwa nuru katika...” Ona, kabla tu jua lile halijatanguliwa duniani, ile nyota ya asubuhi hutoa ushuhuda kuwa “Jua linakuja.” Sivyo? Ona, hilo huleta ile nyota ya asubuhi. Vema, basi ile nyota ya asubuhi na ile nyota ya jioni ni nyota ya aina ile ile, na ni nyota ndogo kote. Je, hamwoni ninalomaanisha? Wajumbe wale.

409 Vema, basi, Yeye alionekana kama Alfa na Omega, Mwanza na Mwisho, Yaspi na akiki. Ona ninalomaanisha? Sasa, kule kuja kwa—kwa Kristo kunakaribia, ndipo Ujumbe ambao Eliya alipaswa kuhubiri katika siku za mwisho, kama kuna kujirudia kwa historia... Kama tu ile nyota ya asubuhi inavyotangulia kule kuja pale, ile nyota ya asubuhi hutangulia kule kuja kwa siku mpya, siku nyingine. Huku ni kule kuja kwa jua ndipo hilo hutangulia kule—kule kuondoka kwa—kwa jua ambako tumekuwa nako na kuja kwa jua mpya, ona, wakati mpya, wakati mpya unaokuja.

410 Sasa, sikiza basi. Kama Yohana alitoa ujumbe wake na akatangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, na Eliya yuaja katika siku za mwisho, nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Kwa maneno mengine, kungekuwa Nuru wakati wa jioni.

411 Ile nuru ya jioni, ile nuru kuu sana tuliyo nayo ni ile nyota ya jioni, nuru kuu sana tuliyo nayo. Vema, basi, ingepaswa kutangaza ujumbe ule ule uliotangazwa na nyota hii nyingine. Inatangaza jua, kunena habari za jua.

412 Vema, sasa sisi tuko katika wakati wa jioni, zile Nuru za jioni ziko hapa. Wakati huu umekwisha. Mwafahamu ninalomaanisha? Siku hii imekwisha, na kutakuwa na kutangazwa kwa siku nyingine inayokuja.

413 Maana, ona, hilo kweli ni... Mtu akiwa magharibi na aitazame nyota hiyo, ingekuwa mashariki. Ndiposa, mwaona, “tumeona nyota Yake mashariki,” lakini walikuwa hakika... walikuwa—walikuwa mashariki wakitazama magharibi kwenye nyota hiyo. Sivyo? Wale mamajusi walikuwa kule magharibi... kule mashariki wakitazama nyuma kwenye ile nyota ya

magharibi. Mwafahamu ninalomaanisha? Lakini ilikuwa nyota ya mashariki kwa wale waliokuwa magharibi.

⁴¹⁴ Ona, kama vile tungelisema... Mimi kila mara husema, “Chini ni juu.” Mnajua je kuwa hilo ni sahihi? Tunasimama katika Umilele, kwa hivyo ile pembe ya kusini ya dunia huenda ikawa upande wa juu na ile ya kaskazini huenda ikawa upande wa chini. Hatujui. Ona, njia ya kwenda juu ni kutelemka. Ona? Sisi tuna... Tunaacha hili; baada ya haya tunaingia Umilele. Inashangilia, inapiga mbiu ya kule kuja kwa Umilele, siku nyingine, wakati mwingine, kabisa,

⁴¹⁵ Sasa tuko katika wakati wa jioni. Tunaamini hilo. Tunaamini kuwa kule kuja kwa Bwana kumekaribia. Vema. Naam, kama ndivyo ilivyo, basi hapana budi kuwe na nyota ya jioni. Na ile nyota ya jioni, kulingana na Malaka 4, ilipaswa “kugeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao,” kurudia mwanzoni.

⁴¹⁶ Lakini yeye alipokuja mara ya kwanza, yeye alikuwa akigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao. Watoto walikuwa wale yeye alikuwa amewakusanya kwake. Ilimpasa kuwaleta watoto... mioyo ya baba (wale baba wa kale, wazee wa kiasili) wairudia nuru hii ambayo yeye alikuwa akitangaza hapa.

⁴¹⁷ Lakini yeye atakaporudi tena, hana budi kugeuka moja kwa moja (je, mlitambua, kabla Ulimwengu kuharibiwa, “ile siku ya Bwana, iliyo kuu na ya kuogofya”) na “kugeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao,” ile ya jioni—ile nyota ya jioni ambayo ilikuwa nyota ya asubuhi wakati huo. Amina.

⁴¹⁸ Natumai—natumai ninalipata sahihi, ona. Ile nyota ya jioni iliyokuwa nyota ya asubuhi, bila shaka ni nyota ile ile. Tuko magharibi, tukitazama mashariki. Wao walikuwa mashariki, wakitazama magharibi. Ni nyota ile ile. Mwafahamu ninalomaanisha? Inategemea uliko, ona, au ni ile nyota ya mashariki au ile nyota ya magharibi. Mwafahamu ninalomaanisha? Vema.

⁴¹⁹ Sasa, inaleta... moja inaelekeza imani ya baba kwa watoto wao; katika wakati huu ni “imani ya watoto iwarudie ya baba zao.” Mngenzunguka, mkarudi tena. Je, hamwoni ninalomaanisha? Mnaona ninalomaanisha? Ni nyota ile ile wakati wote. Jambo lile lile, Ujumbe ule ule, jambo lile lile likirudi tena. Limepita.

⁴²⁰ Na unajua je unapita njia gani? Naamini saa inakuja ambapo watatambua hakika kuwa ulimwengu hata hauzunguki. Naamini hilo kwa moyo wangu wote. Siamini... hata waithibitisheje kisayansi au cho chote kile. Wamefanya mathibitisho mengi ya kisayansi ambayo iliwapasa kuyaghairi. Mungu alisema ulimwengu ulisimama... jua. Namaanisha jua lilisimama badala ya ulimwengu. Ona, jua. Mimi hakika siamini jua... si—si—siamini jua hufanya yale wao wanayosema

hufanya. Najua mwezi hujongea, nami naamini jua huzunguka pia. Ona?

⁴²¹ Lakini baadhi yao husema, “Yeye aliutazama ujinga wa Yoshua, ona, na” kasema “Yeye akasimamisha...kasema lili-...” Vema, yeye alisema, “Yeye alisimamisha dunia.”

⁴²² Nilisema, “Basi uliniambia, ‘Kama—kama ulimwengu ungalisimama kwenye, ungerushwa kasi kama kimwondo angani kote.’ Ona?” Nikasema, “Basi, nini ilitendeka wakati huo?”

⁴²³ Nilikuwa nikiongea na Bw. Thiess hapa, yule mwalimu wa Biblia katika shule ya upili; mwajua alikuwa nani, lakini alisema hivyo. Nikasema; “Naamini hayo ambayo Bibia ilisema, kuwa ulimwengu ulisimama...” Nikasema, “Nakusudia, ‘jua lilisimama,’ Yoshua aliliambia jua, ‘Simama kimya!’ nalo likasimama pale.”

⁴²⁴ Akasema, “Vema, Yeye alisimamisha tu ulimwengu, Yeye aliona ujinga wa Yoshua.”

Nikasema, “Wewe fanya vivyo hivyo kwa werevu wako, basi.” Ona?

⁴²⁵ [Ndugu fulani asema, “Nadhani waweza kuthibitisha kisayansi muda—muda gani jua lilisimama.”—Mh.] Naam, pale wao...nimesikia hilo, pia. Naam, wao hudai...Nilimsikia mamajusi hapa wakati mmoja uliopita akinena kuhusu hilo, kuwa wangelithibitisha. Na wakati ule ule ambao wao...jambo fulani lilitendeka angani ambapo wangeona ambapo jambo fulani lilitendeka mbinguni na kuifungua ile Bahari ya Shamu wakati huo na kadhalika. Wao walithibitisha hayo yote. Vema, jamani, nawaambieni, nyota toka mbali kule mahali fulani ambazo zilitenda jambo kama hilo wakati huo. Ingawaje, hilo ni gumu sana kwetu.

⁴²⁶ Kwa hivyo, sasa, sababu ambayo Ujumbe huu...Ujumbe huu huna budi kuangaliwa hivi, kuthibitisha kuwa ndio. Sasa tunajua, ndugu, kuwa mwanadamu hawezi kuwa Mungu. Mwanadamu, bali yeye ni mungu, kila mmoja wenu ni mungu. Uliumbwa uwe mungu, lakini si unapokuwa katika maisha haya. Ona? Yesu alikuwa mwanadamu kama tulivyo sisi, lakini Mungu alikuwa ndani Yake. Utimilifu wote wa Mungu ulikuwa ndani Yake; tuna Roho kwa kipimo.

⁴²⁷ Lakini kwa kuwa Nuru hii imekuja, na kama ndiyo Nuru ya kweli inayotangaza ule Ujumbe ambao Yohana Mbatizaji alitangaza, kama yeye alivyosema alifanya hivyo kule mtoni... Basi tazama, ingekuware—ingekuware kitu kingine cho chote? Nitazame, ona, bila hata elimu ya shule ya sekondari. Yeye aliponiambia mambo ambayo yangetendeka, hakuna hata moja limekosa kutimia kamwe. Hakuna hata moja lilikosa kutimia. Tazama yale alitenda. Tazama, Yeye hata ono-...

428 Nami niliwaambia ndugu kule nyuma miaka mingi iliyopita, sijui nani angekuwa mzee sana kati yetu, lakini niliwaambia kuhusu mambo haya, kuhusu kuona Nuru hii na ilikuwa ya rangi gani, na kadhalika. Sasa picha ile inaonyesha kuwa ni kweli. Mambo haya mbalimbali yanathibitisha kuwa ni kweli. Sivyo? Verna, ndipo kama hilo ni kweli. . . Na ni Nuru.

429 Sasa, anzia karibu nne. . . [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] . . . iko juu ya kile kifungu cha 3 hadi cha 5 pale, au nakusudia. . . Hebu tuanzia karibu kifungu cha 14, ndugu. Nani ameifungua? Vema. Anzia karibu sura ya 3 ya Injili ya Luka pale. [Ndugu fulani asoma Luka 3;14-16—Mh.]:

Askari nao wakamwuliza, wakisema, sisi nasi tufanye nini? Akawaambia, Msidhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo; tena mtoshewe na mshahara wenu.

Basi watu walipokuwa wakingoja yatakayotokea, wote wakiwaza-waza mioyoni mwao habari za Yohana, kama labda yeye ndiye Kristo;

Yohana alijaribu akawaambia wote, kweli mimi nawabatiza kwa maji; lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto;

430 Vema. Ilikuwa nini? Watu walikuwa na taraja kuu la Masihi kutokea, walipoona hii huduma kuu iliyokuwa na upako, wa mtu aliyetoka nyikani akifanya mikutano yake na kurudi nyikani, watu wengi, hao walikuwa wafuasi wake binafsi, kasema, “Yeye ni Masihi.” Wao walikuwa wakitarajia, ona.

431 Basi kama huu ni Ujumbe wa kweli wa Mungu ukitangulia kuja kule, wa Yohana Mbatiptisti, ule ule. . . kama jambo lile lile, ujumbe wa Eliya, utawaziwa vivyo hivyo. Ona? Kwa hivyo hilo linajibu swali hilo, nafikiri, hivyo hasa. Ona? Hauna budi kuwaziwa vivyo hivyo.

432 [Ndugu fulani auliza, “Kuna cho chote tunachostahiliwa kufanya ili kujaribu kumsaidia ye yote ambaye ange—angeleta u—ubishi kama huo? Au tufanyeje?”—Mh.] Hamna cho chote, hamna lo lote unaloweza kufanya. [“Akili iliyoharibiwa. . . Je, hilo lingemfanya mtu aharibike akili?”] Vema, ingekuwa akili iliyoharibika ikifikia hili: kama mtu yule, yule aliyenenwa habari zake, angeshuhudia kuwa yeye alikuwa Masihi, basi sisi tunajua yeye angekuwa Kristo wa uongo. Ona?

433 Ona, mradi tu mtu yule mwenyewe angeshikilia mahali pake, mwaona. Kama walivyomwambia Yohana, Yohana haku. . . Haisemi cho chote pale kuhusu yeye kusema cho chote kuwahuu. Wao walikuwa—wao walikuwa wale—wale watu, wale—wale Wakristo ambao. . . au waamini waliokuwa wakimwamini Yohana.

434 Wao walisema, “Hakika mtu huyu ni nabii wa Mungu, hapana shaka.” Wao walisema, “Si—si—si—si wewe u Nabii yule?”

Akasema, “La.”

435 Alisema, “Naam, je, wewe—wewe si Masihi?” Ona, wao—wao walidhania yeye alikuwa vile. Ona?

Akasema, “La.” Ona?

“Si—si—sivyo? U na—nani wewe?”

Yeye akasema, “Mimi ni sauti ya mtu aliye nyikani.”

436 Ndiposa Biblia ilisema, “Watu walipokuwa wakingoja yatakayotokea.” Nani huyo? Wasikizaji wake, wale waliomsikia, wafuasi wake, ndugu zake. Ona? Sasa, hawakutaka kumwumiza, hawakuwa wakijaribu kumwumiza. Lakini, ona, wao—wao walidhani hakika mioyoni mwao kuwa yeye alikuwa Masihi.

437 Vema, sasa, historia haina budi kujirudia kila wakati. Tunajua hivyo. Haina budi Kujirudia.

438 Kama unachukua pale katika Mathayo 3, ilisema, “Ili litimie, lililonenwa na nabii, ‘Kutoka Misri nalimwita mwanangu.’” Sasa, hiyo haikuwa... Ilikuwa ikinena kuhusu Yesu, yule Mwana; lakini chunguza yale marejeo, ilikuwa Yakobo, mwana, pia. Ona? Ina maana mbili.

439 Kwa hivyo sasa kama hilo... kama—kama jambo hilo halikutukia, ningesema bado litatokea hivi karibuni, kwa sababu najua Ujumbe huu watoka kwa Mungu na ndio unaotangulia kuja kwa Kristo, na uko katika Roho ya Eliya, na nguvu zake, kwa sababu ni kurudisha mioyo ya watoto. Kila kitu kimethibitishwa kabisa, kwa hivyo haina budi kuumbika kuwa kitu kama hicho kwa watu wa kweli, ambao—ambao wameamini kabisa na ndugu zako na marafiki.

440 Sasa, nimekuwa... nina daktari papa hapa mjini. Naweza kuwaambia kuhusu daktari fulani... Sitawaambia yeye yu nani, rafiki yangu aliyenikumbatia, na kusema, “Billy, ingekuwa rahisi kwangu kukwambia, ‘wewe u Masihi wa Mungu wa siku za mwisho.’” Ona?

Nikamwambia, “Dak, usiseme hivyo.”

441 Yeye akasema, “Vema, sioni ye yote duniani aliyewahi kuwa na jambo lo lote kunena mambo na kufanya vitu unavyovifanya wewe, Billy.” Imemsaidia sana, ona. Yeye alisema, “Mimi huenda kwenye makanisa haya na kuona wahubiri hawa na kadhalika,” yeye alisema, “wewe ni tofauti nao nami najua wewe huna elimu.” Ona? “Nami najua kuwa wewe si mwana saikolojia, kwa sababu wewe... saikolojia, haitendi mambo hayo.” Ona?

Nami nilisema, “Hiyo ni kweli, Dak.”

442 Hakuna haja ya kunena naye kwa sababu hata hajui, hungefikia msingi wa kwanza naye, ona, kwa sababu yeye hajui la kufanya. Bali hivyo ndivyo, mwaona.

443 Najua mwanamke mweusi anayeishi barabara moja toka kwangu, naye humfanyia kazi mtu mwingine ninayemjua, na mke wa mtu huyu alipiga simu, kasema, “Mwanamke yule hakika angekuabudu wewe kabisa kama mungu, kwa sababu yeye alikuwa anakufa kwa ugonjwa kansa, nawe uliweka mikono yako juu yake na kumwambia yeye alikuwa...” Mwanamke huyu ambaye yeye anamfanyia kazi, mume wake na daktari fulani huyu (si daktari niliyekuwa nikinena habari zake, daktari mwingine) hucheza mpira wa vingoe na vinginevyo pamoja, naye alikuwa amemkatia tamaa. Na huyo alikuwa mjakazi wa rafikiye, na alikuwa amemkatia tamaa afe, naye aliponywa kabisa. Na daktari yule hata hangepata dalili yake, ya ule ugonjwa wa kansa. Na, ona, yeye angesema...

444 Sasa, hawalikusudii katika njia ile ninayodhani kuwa wao hulisema au jinsi sisi hulifahamu. Ona? Wao hukuudia kuwa wao wao... Wao humaanisha kuwa wanaamini Mungu yu pamoja nasi, ndani yetu, akitenda kazi kupitia kwetu; si kuwa mtu fulani ni Mungu, mwaona. Sasa, wao walijua kwamba Yohana alikuwa mwanadamu.

445 Vivyo hivyo Yesu alikuwa mtu. Yesu alikuwa mwanadamu tu, Yeye alizaliwa na mwanamke, ilimpasa afe. Sivyo? Yeye alikuwa mwanadamu, ilimpasa ale na anywe, alisikia njaa, alilia, alisikia kiu, na mengineyo, mwanadamu tu kama ulivyo wewe, mwanadamu tu kama nilivyo mimi. Lakini Roho wa Mungu alikuwa ndani Yake katika utimilifu wote, pasipo kipimo. Yeye alikuwa mwenye uweza wote katika mamlaka.

446 Walakini, Eliya alikuwa tu sehemu ya Roho yule; labda aliyetiwa upako zaidi kidogo ya ndugu zake, lakini yeye alikuwa tu sehemu ya Roho yule. Lakini watu wale walikuwa wakimtarajia masihi. Nao walipoona sehemu hii zaidi juu ya ndugu zao, wao wakasema, “Ee, lo, hapana shaka ndiye huyu!”

447 Lakini Yeye alipoanza kuangaza, hiyo nuru ndogo ya Yohana ikazimika. Ona?

448 Na hizi nuru ndogo zitafifia Yeye ajapo, yule Kristo mkuu wa Mbinguni aliyepakwa mafuta akija kutoka mashariki hata magharibi. Na ile... na... Ona? Lakini Yeye hatakuwa duniani sasa, Masihi hatakuwa duniani hata ule Utawala wa Miaka Elfu utakapoanza, ona, ona? Kwa sababu Kanisa, “tutanyakuliwa pamoja nao ili tumlaki Bwana hewani.” Yeye haji kamwe duniani. Yeye atanyakua Bibi-arusi Wake.

449 Yeye atachukua ngazi, mwajua, kama... Mchezo ule uliitwaje? Leo, ambapo mtu yule aliweka ngazi kando ya nyumba ile? Romeo—Romeo na Juliet. Naam, aliweka ngazi ile na kumwiba bibi-arusi wake wakatoroka.

⁴⁵⁰ Sasa Yeye yuashukia kwenye ile ngazi ya Yakobo, na kusema, “Shiii, Mpenzi, njoo hapa.” Ona, tunapanda juu kumlaki Yeye.

⁴⁵¹ [Ndugu fulani auliza, “Ndugu Branham, hili litaambata basi na hilo? Watu hawa walimjia Yohana mbatizaji nao walitaka kumwita yeye Masihi. Nami nilisikia wewe wakati mmoja ukisema Wayahudi wanadhani Masihi alikuwa Mungu.”—Mh.] Unasemaje? [“Nasema, watu hawa walimjia Yohana Mbatizaji, wakidhani kuwa yeye alikuwa Masihi, yule Kristo. Nilikusikia siku moja ukisema kuwa Masihi atakuwa Mungu, kwa Wayahudi.”] Naam, bwana. Ndivyo, yule “rabi.”

⁴⁵² [Ndugu asema, “Vema, Yohana aliwakemea, akisema, yeye ‘siye,’ kuwa Kristo alikuwa yuaja.”—Mh.] Naam. [“Lakini si ni kweli kuwa wanafunzi walimwita Yesu ‘Bwana’? Na Yesu alikubaliana na hilo, akisema, ‘Mnaniita ‘Bwana,’ na ndivyo nilivyo.”] Naam. [“Katika—katika Yohana 13, ambapo Yeye aliwatawadh...?...”] Naam, Yeye angekubali. [“Kuhusu kuwa Bwana, naam, Yeye alikubali.”] Yeye alikubali. [“Yeye alikubali.”] Enhee. Lakini ona, kuhusu Yesu kuwa *Bwana*, Yeye alipoulizwa kama Yeye alikuwa vile, Yeye alisema, “Naam, bwana, mimi ni Bwana na Mwalimu wenu. Mnaniita mimi hivyo, na mnasema vema, maana ndivyo nilivyo.” Lakini... [“Lakini hakujawahi kuwa na kiumbe kingine ambacho, ambacho...”] kingesema hayo. La.

⁴⁵³ Kama ikiwa... Kama mtu angesema kuwa mimi nilikuwa Mungu, vema, hebu niwaambie ninyi katika Jina la Bwana Yesu kuwa “Hilo ni kosa!” Ona? Mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, nikiwa na Ujumbe *toka* kwa Mungu. Ona? Ona?

124. Yapasa au haipasi kanisa la mahali pale kujishughulikia, wajibu—wajibu wake (lenyewe) wa mahali hapo kabla kujishughulisha na mahitaji ya kigeni katika nchi zingine? Hata hivyo, baada ya hilo...zake...Baada ya kutimiza mahitaji yake, ni ya Kimaandiko kwa kwa kanisa la mahali hapo kusaidia kazi za umisheni kama liwezavyo?

⁴⁵⁴ Naam. Vema. Fadhili huanzia nyumbani, mwaona. Sisi—sisi—sisi hushughulikia mahitaji yetu wenyewe hapa, kwa sababu tungekuwa na...hili ni kanisa la Mungu, au cho chote kile, kanisa lenu ndogo, kanisa la Mungu. Sasa, kama hamwezi hata kulipia mchungaji wenu, hamwezi hata kununua vitabu vya nyimbo, hampaswi kuzituma mahali po pote pengine. Ona? Lakini basi baada ya kanisa lenu kulipiwa, na kadhalika, madeni yenu yote yalipwe na kila kitu, yametimizwa na yako sawa na kadhalika, ndipo msaidie ndugu huyo anayehitaji msaada kidogo kule ng’ambo, mwaona. Twaa kidogo...

⁴⁵⁵ Naamini, hali...kama mnalipia kanisa lenu ningeanzisha pia hazina ndogo iwekwe mahali fulani kwa ajili ya sadaka ya umisheni kama hao watu walijisikia kama wanataka kutoa

kwa misheni. Kwa sababu watu wengi watatoa kwa umisheni hali hawawezi kutoa kwa makanisa yao ya nyumbani na kadhalika. Kwa hivyo wasipoitoa kwa misheni, wataitumia kwa kitu kinginecho. Kwa hivyo ningesema tu mwe na kijisanduku kidogo cha umisheni, na ninge- . . . Hivyo ndivyo tunavyojaribu kufanya.

125. Luka 1:17 tafadhali fafanua, Yohana katika akiya “yule roho wa Eliya.”

⁴⁵⁶ Vema, nadhani tuliona Luka—Luka 1:17, enhee, kuja katika “roho wa Eliya.”

⁴⁵⁷ [Ndugu fulani auliza, “Hapo ndipo wale watu wanaoamini kwamba mtu anapokufa huzaliwa tena katika mwili mpya, hupata mafundisho yao?”—Mh.] Kuradhi? [“Je, hapo ndipo wale watu wanaoamini kwamba mtu anapokufa huzaliwa tena katika mwili mpya hupata nadharia yao?”] Hapana shaka. [“Ona, wanaamini yeye alirudi katika. . .”] Naam. [“. . . yeye amerudi katika mwili mwingine.”] Naam, ona, ni kweli kuwa roho hafi kamwe. Hiyo ni kweli. Mungu huchukua mtu Wake ila si Roho Yake. [“Wao husema, ‘Kama umekuwa mzuri utarudi tena katika—katika mtu mzuri.’”] Naam. Naam. [“Kama umekuwa mbaya huenda ukarudi katika mbwa.”] Naam, wame- . . . Naam.

⁴⁵⁸ Vema, sasa, kule ka—katika—kule India, ilikuwa katika kundi la watu ambao tulikutana nao hivyo, nao wange—nao wangepangusa sakafu; wakikanyaga maskini mchwa au kitu fulani, huenda akawa jamaa yao au cho chote kile. Mwaona, hawangefanya hilo. Lakini, mwaona, hayo ni—hayo ni ukafiri. Ona? Huo ni ukafiri. Naam.

126. Paulo aliwaambia. . . Paulo alisema, “Takeni sana karama zilizo kuu, na hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.” Tafadhali eleza “njia iliyo bora” ni ipi.

⁴⁵⁹ Upendo, I Wakorintho 13, ona, “Takeni. . .” Kwanza fungueni. . . Sasa fungueni I Wakorintho 13 pale, ndugu. I Wakorintho, sura ya 13, na sasa hebu soma vile vifungu vitatu au vinne ya mwisho. I Wakorintho 13, mwisho. . . yapata vifungu vitatu vya mwisho vya sura ile—ya ile su- . . . [Ndugu fulani asoma I Wakorintho 13:11-13—Mh.]:

Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, silifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga, tokea hapa nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto.

Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami. . . kama mimi nami ninavyojuliwa sana.

Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo. [Ndugu Branham asema, “Lo, jamani, upendo”—Mh.]

127. Ndugu awezaje kulaumiwa ambaye udhaifu wake ni kuchukua nafasi kanisani bila kuulizwa afanye hivyo?

Ee, jamani! Vema, mvumilie, nadhani. Ona?

Ndugu awezaje kulaumiwa... Yeye hapaswi kulaumiwa!... ambaye—ambaye udhaifu wake ni kuchukua nafasi kanisani bila kuulizwa afanye hivyo?

⁴⁶⁰ Kwa mfano, kama yeye alitaka ku—kuwa shemasi. Ona? Naye hajaulizwa kufanya hivyo, bali yeye ataka kuwa shemasi, haidhuru, ona. Vema, kama ni mtu wa aina hiyo, mnajua kuna jambo fulani ndogo, mwajua, udhaifu mahali fulani, haidhuru, na kwa hivyo nitamshughulikia tu katika upendo.

⁴⁶¹ Na hakika, hutaki kamwe ku—kufanya jambo kama hilo isipokuwa unajua hakika. Weka mtu wenu bora sana mwezaye kwenye halmashauri yenu, mwaona, hivyo. Ndugu, msimweke ye yote ndani mle ambaye... Mchunguzeni mtu yule, kwanza. Shemasi ana wajibu mkubwa kuliko wa mchungaji. Yeye apaswa kuwa asiye na hatia, shemasi sharti awe hivyo. Ona?

128. Katika ibada moja ya ushirika, mtu fulani alikuwa madhabahuni kuomba. Ndugu Branham alikuwa amesimama nyuma ya—ya vitu vya ushirika vilipokuwa vikitolewa, yeye akasema, “hangeviacha aombe pamoja na yule mtu pale madhabahuni.” Tafadhali eleza.

⁴⁶² Nilimtuma msaidizi, mwaona, Ndugu Neville. Nakumbuka usiku ilipotendeka. Napaswa kukaa pamoja na hiyo meza ya ushirika, ona, hata wakati... Tazama hapa. Sasa, sina wakati wa kuingilia haya. Mtu fulani anayeketi hapa ambaye aliuliza, hakika. Iko hivi, ndugu. Mnapo—mnapokuwa na ushirika, huo unauwakilisha ule mwili wa Yesu Kristo. Ingekuwa... Yapaswa uwe chini ya ulinzi wakati wote.

⁴⁶³ Tazama, Eliya alipomwambia Ge—Gehazi, “Chukua fimbo yangu” (yeye alikuwa ameibariki fimbo hiyo), yeye alisema, “nenda zako. Na mtu ye yote akinena, usimjibu. Mtu ye yote akikusalimu, usimsalimu. Nenda zako, ukaweke fimbo hiyo juu ya huyo mtoto.” Sivyo? Kaa na hiyo fimbo! Ona? Na hilo ndilo nilikuwa nafanya.

⁴⁶⁴ Sasa, kama hakukuwa na mchungaji msaidizi hapa, amesimama pale... Nilikuwa nimemaliza kuhubiri. Nakumbuka ilikuwa lini. Nami... kama wao... kama Ndugu Neville hangekuwa amesimama pale, au mtu mwingine kumsaidia mtu yule madhabahuni... Nilikuwa tu nimemaliza kuhubiri, kwa hivyo nilikuwa nimesimama penye meza ya ushirika. Na walipokuwa wakijitayarisha kupokea ushirika,

nami nilikuwa ni—nikihudumu ushirika. Sasa, Ndugu Neville alikuwa amesimama pale.

⁴⁶⁵ Vipi kama tayari waliisha kuja madhabahuni na Ndugu Neville alikuwa bado katika kuhubiri kwake, naye alikuwa akihubiri? Ningeenda madhabahuni pamoja na mtu yule, kama yeye angeondoka nje ya mkutano hali yeye anahubiri, aende madhabahuni. Ningeliweza kuona kwamba ndugu yangu alikuwa . . . kuwa yeye alikuwa na upako wa Roho. Yeye alikuwa akihudumu. Yeye alikuwa mhudumu katika . . . yeye alikuwa katika huduma, mhudumu katika huduma.

⁴⁶⁶ Na msiwaruhusu wanene kwa lugha kamwe, kukatiza, au vyo vyote vile, mhudumu katika huduma yake. Naam, kama Roho Mtakatifu ananena na mtu fulani na akimbie madhabahuni akaokoke, acha mhudumu aendelee katika huduma yake; acha mchungaji, shemasi, msaidizi, kama kunaye msaidizi au mhudumu mwingine ye yote, hebu akamshughulikie mtu huyo upesi. Na msimsumbue mhudumu katika huduma. Ona?

⁴⁶⁷ Nami nilikuwa nyuma ya dawati katika huduma, nikihudumu ushirika. Na msaidizi wangu, Ndugu Neville, alikuwa amesimama karibu nami. Basi mtu mmoja akakimbia madhabahuni, nikasema, “Nenda, nenda aliko, Ndugu Neville.” Ndugu Neville akamwendea. Hiyo ndiyo sababu sikuenda.

⁴⁶⁸ Naam, kama hakungekuwa na msaidizi hapa, au mwingine ye yote wa kumwendea mtu yule, ningeondoka na kukomesha ushirika, na kuenda pale na—na kuhakikisha kuwa nafsi hiyo imeokoka. Mwaona? Lakini kwa kuwa kulikuwa na mtu wa kutuma, ingeniondoa katika ile huduma, mwaona, ambapo nilikuwa nikihudumu ushirika.

129. Mtu anaweza kufanya nini. . . Ni mambo gani yampasayo mtu kufanya kama msaidizi wa watu binafsi katika kumshughulikia mtu anayemtafuta Roho Mtakatifu, bila kukiuka Maandiko?

⁴⁶⁹ Vema. Endelea tu kumnukulia Neno, ndilo jambo bora la kufanya. Neno lina Nuru. Sema tu, “Ndugu, Yesu aliahidi. Kumbuka, ni ahadi Yake.”

⁴⁷⁰ Usimtikise, usimsukume, au kumsumbua-sumbua, au cho chote kile. Usijaribu ku- . . . Naam, usijaribu kumpea Hiyo, kwa sababu huwezi. Ona? Ona? Wewe. . . Mungu atampea. Wewe endelea tu kumnukuulia ahadi. Ona? Zidi kusimama pale kunukuu zile ahadi. “Mungu Mbinguni, namwombea ndugu yangu. Ahadi Yako ni kwamba Wewe utampa Roho Mtakatifu.”

⁴⁷¹ Ndipo kama unajaribu kumtia moyo. . . Yeye anasema, “Ee, ndugu, mchungaji, ndugu,” ye yote yule aliye karibu naye, “Ni—ninataka Roho Mtakatifu.”

⁴⁷² “Ndugu, ni ahadi. Mungu alitoa ahadi ile. Je, unaamini Yeye aliahidi? Sasa, usishuku hilo. Ukiamini ahadi ile, Roho Mtakatifu atakushukia wakati wote sasa. Uwe ukimtarajia. Jitolee Kwake kabisa, na useme, ‘Bwana, ninasimama kwa ahadi Yako.’”

⁴⁷³ Sasa, endelea kunukuu. Sasa, fanya mtu wa—wa—wa—wako, ona, mfaye aache. . . Endelea kunukuu. Sema sasa, “Mwambie Mungu. Sasa, umeshatubu?”

“Naam.”

⁴⁷⁴ “Sasa sema, ‘Bwana, Wewe ulisema kama nikitubu Wewe u mwenye haki kunisamehe. Wewe ulisema kama ningetubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zangu, ningepokea Roho Mtakatifu. Sasa, Bwana, nimefanya hayo. Nimefanya hayo, Bwana. Nimefanya hayo. Ninangoja, Bwana. Wewe uliahidi.’”

⁴⁷⁵ Ona, hivyo ndivyo, endelea kumfariji. Mweke humo kwenye Neno. Kama itakuja kamwe itakuja basi.

**130. Je, mhubiri au Mkristo ye yote afanya vema asiyeamini . . .
la: Je, mhubiri au Mkristo ye yote afanya vema asiyeamini
usalama wa Milele?**

⁴⁷⁶ Sasa, hebu tuone. Nawaza ile “. . . kufanya . . .” Ona kama utasoma hilo jinsi nifanyavyo. Lisome. [Ndugu fulani asoma swali, “Je, mhubiri au Mkristo ye yote afanya vema asiyeamini usalama wa Milele?”—Mh.]

Nilidhani huenda nilisoma hilo sahihi. Sasa, vema, mimi . . .

Je, mhubiri afanya vema asiyeamini usalama wa Milele?

⁴⁷⁷ Ningeamini kuwa mhubiri huyo alijuwa akifanya . . . kama yeye hakujua lo lote kuhusu usalama wa Milele. Lakini kama yeye aliujuu na kujua kuwa ni Kweli, halafu asiuhubiri, hana aibu; naam, au Mkristo ye yote. Sasa, Mkristo, sasa, ningewaambia Wa—Wakristo ambao hawafahamu hayo vizuri sana . . .

⁴⁷⁸ [Ndugu fulani auliza, “Hilo si fundisho dhahiri, sivyo, Ndugu Branham, kuhubiriwa watu ambao hawajawahi . . . ?”—Mh.] La, la, la. Sasa, hilo ndilo nilikuwa tayari nafikia. Naam. Ona? Ona?

⁴⁷⁹ Sasa, mwakumbuka yale niliyosema Jumapili iliyopita? Kama wewe u mhubiri, jipatie mimbara. Kama sivyo, ishi mahubiri yako. Ona, hiyo ndiyo njia bora sana ya kufanya hivyo, ishi mahubiri yako. Kama wewe ni mhubiri, jipatie mimbara, ona, kisha uanze kahubiri. La, sivyo, ishi mahubiri yako, hebu na maisha yako yawe mimbara yako. Ona? Nadhani hilo linashughulikia mengi, sivyo? Ona? Ona? Kwa sababu wakati mwingi twaona . . . Nanyi ndugu fanyeni hayo makanisani mwenu.

480 Kumbuka, washiriki wako wakati mwingine hujaribu kueleza mambo na kufanya mambo, ni heri kwamba uwashauri kutokufanya hivyo. Na kama mtu ye yote ataka kujua jambo fulani, hebu na waje kwa wale—wale waliofundishwa kufanya hivyo. Mwaona?

481 Tuseme, vema, sasa, kama mtu fulani angesema, “Heei, nawaambia... Wao huniambia, ninyi kule katika kanisa lenu mnaamini usalama wa Milele.”

482 Sasa, yakupasa uwe macho. Huenda ukaingia katika farakano kuu kuliko ulivyowahi kuwa, mwaona, na kumfanya kumpoteza sana kuliko alivyowahi kuwa. “Hebu nikwambie, ukija umuuliza mchungaji wetu, ona. Ne—nenda kaongee naye, ona. Sisi... Hilo ni kweli, najua mchungaji wetu, anaamini hayo. Naamini hayo pia, lakini siwezi kuyaeleza... mimi si mhubiri. Naamini tu hayo, hivyo tu ndivyo ni juavyo. Naamini kwa sababu nilimsikia yeye akiyaeleza hivyo kwa Biblia, hata hamna shaka kamwe.” Ona?

483 Lakini a—afadhali mshiriki amwambie mchungaji kuhusu hayo. Pia, huyo mchungaji, na awe na hakika kuwa yeye anajua jinsi ya kulijibu, pia. Kwa hivyo lisome kirefu barabara, kwa sababu mara nyingi watakufunga kwalo, mwaona. Jinsi...

484 [Ndugu fulani asema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Kaniradhi. [“Kama naweza...?... Lakini ni—ninajua wito wangu na nimefanya imara uteule wangu.”] Enhee. [“Umesema sasa hivi kuwa ‘kama wewe u mhubiri, unapaswa kuwa na mimbara.’”] Naam, bwana. Ndivyo. [“Mimi si mhubiri, mimi ni mwinjilisti.”] Naam, bwana. [“Lakini mimbara ya kila mtu ni yangu.”] Naam. [“Lakini hivi sasa nafanya kazi, kazi ya mikono. Si kazi ngumu, lakini ninafanya kazi, nami sina mimbara. Nami naamini kuwa muda huu wa kazi nilio nao ni mapenzi ya Bwana. Yeye aliniambia niifanye, kupitia kwa Neno na ushuhuda wa Roho. Nami naamini, baadaye, mimbara zitakuwa wazi.”] Bila shaka, hiyo ni kweli. [“Je, hilo ni sahihi?”] Naam, ndugu.

485 Ndugu, sasa, kama utarudi nyuma hapa na upate daftari kubwa ya kale ya kanisa, utaona kuwa nilikuwa mchungaji wa kanisa hili kwa miaka kumi na saba, na nilihubiri kila siku, nilihubiri kila siku na kufanya kazi kila siku. Ona? [Ndugu fulani asema, “Kama unafanya kazi, ni ishara nzuri kuwa wewe *umetwa*.” —Mh.] Naam. Paulo alifanya hivyo, sivyo? Paulo alitengeneza hema. [“Nilikuwa karibu kukata tamaa kwa sababu, kama ulivyosema, kila mhubiri hana budi kuwa na mimbara. Mimi... mimi hukata tamaa, lakini najua kuwa Mungu aliniita nipate kazi, kwa muda mchache.”] Bila shaka Paulo alienda na kutengeneza hema, sivyo? Alifanya kazi kwa mikono yake kusudi asi... Hiyo ni kweli kabisa. Bila shaka. [“Hapo ndipo nilipo.”] Ona? Hiyo ni kweli. Ona? John Wesley alisema, “Ulimwengu ndio mtaa wangu.” Kwa hivyo mimbara

yako bado i wazi, ndugu. Mwinjilisti huenda ulimwenguni kote. Sivyoy? “Enendeni ulimwenguni kote.” Kwa hivyo mimbara yako ni ulimwengu mzima. Naam, bwana.

Swali:

131. Je, sharti, s-h-a-r-t-i... Sharti shemasi au mdhamini adumu katika mafundisho ya kanisa lao? Naam. Hiyo ni kweli. Je, ni halali kwao kuongeza au kuondoa toka kwa mafundisho hayo kwa sababu ya maoni yao wenyewe au ufunuo wao binafsi? La, bwana. La.

⁴⁸⁶ Yampasa shemasi au mdamini yapasa kuambatana na—na mafundisho ya kanisa lao. Yawapasa kudumu kikamilifu na tafsiri ya Maandiko ya kanisa lao, kwa sababu, wasipofanya hivyo, wanapigana na jambo lile lile. Wana—wanajidhuru wenyewe. Ona? Mnapigana. . .

⁴⁸⁷ Ni, kwa maneno mengine, ni kama—kama—kama kusema napenda jamaa yangu na kujaribu kuwalisha sumu. Ona, jambo lile lile. Mwaona, huwezi kufanya hivyo, u- . . .

⁴⁸⁸ M—mdhamini au shemasi anapochukua afisi yake, au afisa ye yote wa kanisa anayewakilisha halmashauri fulani ya kanisa, ona, anayewakilisha kanisa.

⁴⁸⁹ Hiyo ndiyo sababu niliacha kanisa Batisti, ona, wakati wa kwanza kabisa. Nilikuwa tu nimekuwa ndani mle kidogo nao—nao waliniuliza kuwawekea mikono wahubiri wanawake. Vema, hakika singeweza kukaa kule. Nilisema, “Na—nakataa kufanya hivyo.”

⁴⁹⁰ Basi mchungaji akanifukuza, “Nini hii? Wewe ni mzee wa kanisa!”

⁴⁹¹ Nikasema, “Daktari Davis, kwa heshima yote inayostahili imani ya Baptisti na kila kitu ambacho nimetiwa mikono kufanya, sikujua ya kwamba hilo lilikuwa fundisho la kanisa Batisti kuwatia mikono wanawake. Hilo ndilo jambo moja lililoachwa.”

Naye akasema, “Hayo ni mafundisho ya kanisa hili.”

⁴⁹² Nikasema, “Bwana, naweza kuachiliwa usiku wa leo, au je, waweza kunijibu maswali kadha?” Ona?

⁴⁹³ Yeye akasema, “Nitajibu maswali yako.” Kasema, “Ni wajibu wako kuwa pale.”

⁴⁹⁴ Nikasema, “Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Napaswa kushiriki cho chote kanisa hili linafanya. Mimi niko hudumani, mmoja wa wazee wa hapa.” Naye akasema. . . Nikasema, “Waweza kunieleza kwa nini katika I Wakorintho 14 na 15 pale, ‘Naapo Paulo alisema, ‘Na wanawake wenu wanyamaze makanisani, hairuhusiwi kwao kuna.’”

⁴⁹⁵ Naye akasema, “Naam, bila shaka!” Akasema, “Kama. . . naweza kujibu hayo.” Akasema, “Mwaona, jambo ni kwamba,”

kasema, “Paulo alisema... Wanawake wote—wote walikuwa wakiketi pembeni, wakiondoka tu ghafula kama wafanyavyo mara ‘Msiwaruhusu akasema, ‘Msiwaruhusu wafanye hayo.’ Ona?”

⁴⁹⁶ Nami nikasema, “Basi nifafanulie 2 Timotheo, ambapo Paulo alisema, pia, mwandishi yule yule, mtum’Simpi yule, alisema, ‘Simpi mwanamke ruhusa kufundisha, wala kuchukua mamlaka yo yote, ona, lakini a—awe katika utiifu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza na Hawa baadaye, na Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa.’ Yeye amedanganyika. Sasa, sisemi yeye ataka kufanya jambo lo lote baya, lakini yeye hakika amedanganyika kwake.’ Yeye hapaswi kuwa mwalimu.”

Akasema, “Hayo ndiyo maoni yako?”

⁴⁹⁷ Nikasema, “Hayo ni mawazo ya Maandiko nionavyo mimi. Hayo ndiyo Biblia ilisema.”

⁴⁹⁸ Yeye alisema, “Kijana, unaweza kunyang’anywa leseni yako kwa hayo.”

⁴⁹⁹ Nikasema, “Nitawatatulia shida zao. Nitaitoa, Daktari Davis.” Nikasema, “Si kwa kutokukuheshimu wewe...” Naye hangefanya hivyo, hata hivyo. Yeye aliyaachilia, aliyaachilia hayo yapite hivyo.

⁵⁰⁰ Ndipo aliniambia kwamba angejadiliana nami wazi wazi. Nami nikasema, “Vema, wakati wo wote tu.” Lakini yeye—yeye hakufanya hivyo.

⁵⁰¹ Kwa hivyo basi mu—muda mfupi baadaye, basi, Bwana akanena nami, na kuhusu yule—yule Malaika wa Bwana akaja, ndipo—ndipo yeye akamfanyia mzaha, mwaona. Ndiposa ni—nikamwambia, nikasema. “Vema, Daktari Davis, ni heri kujiondolea hii sasa hivi, ona,” nikasema, “kwa sababu itakuwa mzigo. Nimetiwa mikono hivi majuzi, haidhuru, kwa hivyo itakuwa mzigo kwangu, kwa hivyo heri nijiondolee hii sasa hivi.”

⁵⁰² Kwa hivyo kama singekaa katika kanisa Batisti na kufundisha mafundisho ya Batisti na kukubaliana na imani ya Batisti. Kama nilifanya hivyo—kama nilifanya hivyo kwa sababu lilikuwa kanisa, basi nimekosea, ona, ninaficha kitu fulani. Na kama—kama mimi—kama mimi ni mwaminifu kwangu binafsi, nitawaandea Wabatisti (mchungaji wangu au ye yote awezaye kulieleza kwangu) na kuwauliza wao ne—neni la Uzima; kama yeye aweza kunionyesha sahihi iliko moja kwa moja Maandikoni, na kutosheleza ninavyojisikia, basi nitanena tu jinsi wao hulinena, ona, nami nitakuwa Mbatisti.

⁵⁰³ Hiyo ndiyo sababu mimi ni huru. Hiyo ndiyo sababu siko kwa madhehebu hayo, kwa sababu siamini katika madhehebu. Nami naamini haimo Maandikoni, kuwa na madhehebu.

504 Kwa hivyo, singekuwa mfuasi wa dhehebu lo lote na kujisikia mwenye haki kwa kufanya hilo. Ona? Kwa hivyo, siwaingizi watu ndani na kuwafanya washiriki, na mengineyo kama hayo, kwa sababu naamini *tumezaliwa* kuwa washiriki, tumezaliwa kuwa katika Kanisa la Mungu aishiye. Ona?

505 Hatuandiki majina ya watu kwenye kitabu na kuwafukuza, na mengineyo kama hayo, kwa sababu naamini huo si—huo si wajibu wetu kufanya hayo. Naamini Mungu ndiye anayewafukuza. Ona? Lakini naamini kuwa kanisa, kama kungekuwa na ndugu aliyekuwa akifanya makosa . . .

506 Kwa mfano, kama—kama walimshika Ndugu Neville, au Ndugu Junior, au Ndugu . . . ndugu fulani hapa, mmoja wa mashemasi au wadhamini, au ye yote yule, akifanya kosa, naamini jambo la kufanya ni kwa kanisa kukusanyika na kumwomba ndugu huyu. Kama yeye bado hawi mwaminifu, ndipo watu wachache wamwendee ndugu yule kumpatanisha. Ndiposa basi asipokubali, basi huo ndio wakati wa kanisa lote basi, ona, hilo ni kwa mchungaji, wazee, na kadhalika kufanya hivyo. Siamini kuwa halmashauri yo yote ya mashemasi ina haki kumfukuza ye yote kanisani au halmashauri yo yote ya wadhamini au mchungaji ye yote ana haki ya kufanya hilo.

507 Nafikiri kama ye yote angetengwa na ushirika, ingekuwa kwa ajili ya kuishi kizinz, au mambo kama hayo, ya kwamba yeye si mtu anayefaa, kama mtu kuja hapa na kuharibu wasichana wetu ama—ama kuwatukana wanawake wetu, na mambo kama hayo, na angali anakiri kuwa mmoja wetu hapa. Ona? Sasa, kama yuko nje mahali fulani akituingilia, naam, itatubidi tufanye jambo fulani, ila, mtu kama huyo, mtu mwasherati akijaribu kufanya mapenzi na wake zetu au—au kuwatukana binti zetu au, mwajua, mambo kama hayo, au kuwafanyia tendo fulani la kizinz, au kuwachukua nje wavulana wetu wadogo na kuwafanyia upotovu, ama kitu kama hicho.

508 Mambo hayo yapaswa kufuatiliwa, halafu mtu yule afukuzwe katika ushirika na asiruhusiwe kupokea ushirika pamoja nalo, kwa sababu hatupaswi kufanya hivyo. Haitupasi. “Ye yote akila isivyostahili, ana hatia ya ile Damu na mwili wa Bwana,” juu ya mtu huyo.

509 Lakini naamini kama mtu akisema tu, “Vema, basi yeye—yeye ni *hivi*, *vile*,” Mwombeeni.

510 Sitasahau kamwe, katika Stockholm, Sweden, Ndugu Lewi Pethrus, mtu mashuhuri wa Mungu. Tulikuwa tumeketi mezani, dakika chache tu kabla hatujarudi Amerika. Tulikuwa na mikutano mikubwa kule. Naye alisema, Gordon Lindsay akasema, “Ni nani msimamizi wa ushirika huu mkuu?” Wee, umeshinda Assemblies of God kwa mamia ya maili, mwaona. Kasema, “Ni nani anayeusimamia?”

Na Lewi Pethrus ni muungwana. naye alisema, “Yesu.”

Yeye akasema “Ni nani padre wenu?”

Akasema, “Yesu.”

511 Yeye akasema, “Najua hiyo ni kweli,” kasema, “tunaamini vivyo hivyo kuhusu Assemblies of God yetu.” Akasema, “Naam.” “Lakini,” kasema, “tuseme kwa mfano, ndu—ndugu aanguke,” kasema, “nani ana mamlaka ya kumfukuza?”

Kasema, “Hatumfukuzi.”

“Vema,” kasema, “mnafanyaje?”

512 Kasema, “Tunamwombea.” Nilidhani hilo ni zuri sana! Hilo lililonekana kama Kristo kwangu, “Tunamwombea.” Hakuna ye yote amfukuzaye, wanamwombea.

513 Kasema, “Vema, basi, vipi kama ndugu fulani wanakubaliana,” yeye alisema, “na wengine wao hawataki kushiriki pamoja naye tena? Kamleta, kama ni mchungaji, mwoana, anayeanza kuwa mtu wa wanawake kati ya... Mwajua ninalomaanisha, na mambo kama hayo, na baadhi ya wachungaji hawatamruhusu makanisani mwao. Mnafanyaje, mnamfukuza nje ya dhehebu lenu?”

514 “La.” kasema, “Tunamwachilia na kumwombea.” Kasema, “Bado hatujampoteza hata mmoja. Wao kila mara hurudi, sijui vipi.”

515 Yeye alisema, “Vema,” kasema, “sasa, vipi kama...” kasema, “Vipi kama baadhi yao wasema kuwa wao wanamtaka na wengine hawamtaki? Sasa, na hilo je?”

516 Kasema “Vema wale wanaomtaka, wanamchukua; wale wasiomtaka, hawalazimishwi.”

517 Kwa hivyo—kwa hivyo nafikiri hiyo ni njia nzuri ya kufanya hivyo, sivyo, ndugu? Basi kwa njia hiyo tunakuwa “ndugu.”

518 Sasa, ndugu zanguni, natumai kuwa mambo haya yameonyesha njia fulani kuelekea jibu au jambo fulani, ya kwamba mkutano wetu hapa usiku huu ume—umetufaidi kwa njia fulani. Najitayarisha kuondoka sasa kwa muda mchache, kuhudhuria mikutano kule Magharibi. Nina shauku sana ya maombi yenu.

519 Baadhi ya majibu yangu ndani humu, labda mengi yao, labda hakuna lo lote, lililokuwa sahihi. Sijui. Lakini ingekuwa bora sana kwangu kuyakusanya maoni yangu, mwaona, kujaribu kulieleza. Huenda ikawa haya yaliletwa humo nyumaye, sikuwa na wakati wa kuyachunguza. Nami sikufanya hivyo, yalikuwa... Nakusudia kusema, yalikuwa Maandiko tunayosoma hapa kila wakati, siku baada ya siku kanisani. Nilidhani labda ingekuwa jambo fulani kubwa la kufanyia bidii ambalo huenda likatufanya sisi kuchambua na kuliingilia hata

kufikia jambo fulani kuu, lakini inaonekana tu kama maswali ya makanisani.

⁵²⁰ Nina furaha kuwaona ninyi mmeshikilia hivyo, hamna kukosa taratibu, wala kutoridhika kwo kwote, wala farakano lo lote. Hakuna swali lililobishania na ikasemwa, “Ni kosa, Hili ni kosa, hatulitaki.” Ilikuwa tu ndugu waliotaka kujua kitu fulani kuimarisha misimamo yao, hivyo tu. Hilo . . . kuimarisha, kujifunga—kujifunga silaha na kuzikaza zaidi, kuziba pengo lingine humo. Natumai kuwa tutapata kukutanika mara nyingi zaidi hivi, kujivika silaha.

⁵²¹ Nanyi mkumbuke, ndugu, silaha yangu inatakiwa kukazwa, pia. Kwa hivyo mniombe Mungu kuwa Mungu atanisaidia na akaze silaha yangu zaidi kidogo, nipate ku- . . . nisiwe mlegevu sana kwa mambo. Na maisha ninayoishi na mambo nifanyayo, hebu nikayafanye kwa moyo mnyenyekevu, na kwa hamu kuu zaidi. Na Mungu anipe moyo wa kutenda kuliko nilivyokuwa hapo mbele. Nawaombea ninyi jambo lile lile. Mungu awabariki.

⁵²² Nimewakawisha ninyi hapa kwa muda mrefu, na hivi sasa ni saa tano kasoro dakika tano.

⁵²³ Na sasa, Ndugu Neville, huenda ni—nika- . . . Sasa, niliona, ni karibu tu maili mia tisa na kitu kule, sitaondoka hata Jumatatu asubuhi. Lakini nataka kuwa hapa Jumapili kwa ajili ya shule ya Jumapili, ninakuja kama mgeni kusikiza ukihubiri, mwaona, Jumapili. Ona? Lakini . . . Vema, ndugu, naam, ndugu. Ndugu Neville, sababu yake ndiyo hii, ndugu. Mimi . . . Nakupenda na umekuwa mkarimu kwa kunipa mimbara kama tu . . . kana kwamba nilikuwa mzee mkuu kwenu, au kitu fulani. Lakini sijajisikia hivyo, Ndugu Neville. Nimejisikia kuwa sisi tu ndugu.

⁵²⁴ Ndugu Ruddell na Ndugu Junie, na, ee, ninyi nyote ndugu zanguni na ninyi wote, sisi tu—sisi sote ni ndugu, mwoana.

⁵²⁵ Lakini vipi . . . Sababu yake, nimepwewa kidogo na sauti sasa, mwoana, na nimekuwa vitani majuma sita mfululizo, mwaona. Nami na—nataka tu labda kuanza nikiweza, wazo, baada ya mkutano huu usiku huu, ambalo litanipa ijumaa na Jumamosi na Jumapili kupumzika, kabla sijaanza mikutano ya kule nje.

⁵²⁶ Na Ndugu Junie, mara tu nitakaporudi, wakati mmoja nitakaporudi, sina budi kushuka kuja kuwaona tena, nataka kuja hako nje. Nilipitia kwenye kanisa lako ndogo pale, jana, naamini. Mke wangu akasema, “Nadhani kuwa . . .” Liko nje pale kando ya barabara ya reli karibu na Glenellen Park? Ningependa kuja huko na kuongea na hao watu wa Sellersburg, Vema.

⁵²⁷ Ndugu Ruddell, moyo wako ubarikiwe. Ningetaka kukutembelea, una kundi la watu wazuri. Uliketi pale usiku huu ukisikiza kama kwamba ulikuwa mzee wa zamani akisikiliza.

528 Ndugu Beeler pale, ni mmoja wa ndugu zetu wainjilisti. Natumai wakati mwingine naweza kukuta mojawapo wa mikutano yako mahali fulani, ndugu, nikatoe ushawishi fulani, kupata jambo fulani la kusema mahali fulani kukuinua njiani. Mimi kila mara huwanena mema kwa mtu ye yote, wewe pamoja na Ndugu Stricker hapa, na wainjilisti.

529 Ndugu Collins hapa, ambaye naamini siku moja atakuwa mhudumu wa wakati wote kazini.

530 Mashujaa, watu hodari, watu halisi wa imani, Mungu awe pamoja nanyi nyote, nanyi mashemasi, ninyi wadhamini, enyi ndugu zanguni.

531 Naamini una . . . Ndugu huyu hapa, siwezi kukumbuka jina lake. Wewe ni . . . [Ndugu Caldwell asema, “Ndugu Caldwell.”—Mh.] Caldwell. Wewe ni . . . Wewe ni mmoja wa wazee au cho chote kile, sivyo, au. . . [“Mhudumu.”] Mhudumu. [“Mimi ni mhudumu. Nilikuwa wa Church of God, singehubiri Injili nzima na nikae nao. Singehubiri ubatizo katika jina la Yesu na nikae nao. Nilikuwa na leseni ya huduma ya kiwango cha juu sana waliyo nayo, lakini nikawakataa. Tangu nilipokusikia wewe ukihubiri hizo jumbe kuu, niliwakataa na kuondoka dhehebuni. Sasa nataka kuwa mmoja wa wenu.”]

532 Asante, ndugu. Tunakukaribisha kwenye ushirika wetu. Na hati—hati zetu hutoka juu. Maisha yetu ndiyo hati zetu, mwaona. Hizo ndizo hati zetu. “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini mimi.” Ona? Hiyo ni kweli. Hizo ndizo hati zetu. Na kama mzee . . . Kama Howard Cadle alivyo zoea kusema, “Hatuna sheria ila upendo, hatuna kitabu ila Biblia, na—na hatuna—hatuna kanuni za imani ila Kristo, kitabu ila Biblia.”

533 Nasi ni—sisi ni, Ndugu Caldwell, tuna furaha kuwa pamoja nawe. Unatoka katika dhehebu kuu. Church of God ya Anderson, nafikiri. [Ndugu Caldwell asema, “Ya Cleveland.”—Mh.]. Au kanisa la Cleveland, Pentecostal Church of God. [“Na nilikuwa mchungaji kule. . . ? . . .”—Mh.] Bila shaka. Bila shaka, nimeshakuwa huko. Naamini nilikuwa huko na Ndugu Neville. . . au Ndugu Wood, wakati mmoja, tulimchukua mbwa au mbwa wa kuwindia kutoka kwa mtu fulani aliyehudhuria kanisa lako pale. Nami nilisimama vipandioni nje pale na kuongea, nao walikuwa wanaongea juu yako. Vema, nina hakika. . . [“Kanisani mwangu.”] Ee? [“Burns.”] Naam, Ndugu Burns. Naam [Ndugu Caldwell aeleza tukio fulani—Mh.] Ee? Naam. Ee, Bertha, hiyo ni kweli. Lo, ajabu hiyo.

534 Ndugu Rook pale, yeye ameshakuwa mchungaji? [Ndugu Rook asema, “Mwinjilisti tu.”—Mh.] Mwinjilisti. Nataka kotoa maelezo juu yako, Ndugu Rook, Ndugu Rook. Nimeshasikia kuhusu kazi kuu unayomfanyia Bwana. Wewe . . . nilisikia ulianda Indianapolis au ulikuwa ukianda Indianapolis, ukafanya ibada ukawaleta watu kwa Kristo. Mungu awe nawe, Ndugu

Rook. Hakika nina furaha kukuona. Nilikuona nje hapa kwa hizi tingatinga zee nje hapa, ukizunguka-zunguka hapo, ukitia bustani yako mbolea. Vema, nilikuona nje kule ukijaribu kumfanyia Bwana jambo fulani. Nafurahi Yeye alikuwa katika huduma, dumu ukimshikilia mbele yako, ndugu. Mungu akubariki. Usipatane kwa cho chote; bali ifanye kwa roho mwema sana uwezavyo. Na ujumbe wa—wako kila siku ukolee kwa uzuri wa Roho Mtakatifu.

⁵³⁵ Na Ndugu Stricker...[Ndugu fulani asema, “Twahitaji maombi yenu ninyi nyote. Tuna—tunajaribu kuanzisha kanisa chini kule Vernon Kaskazini.”—Mh.] Lo, natumai mtalipata. Tutawaombea. [“Linaendela vizuri sana, umbali huu.”] Sawa.

Billy, utaanza lini kufanya kazi ya uchungaji?

⁵³⁶ Daktari Goad na Daktari Mercier hapa, na—na—natumaini...huitana hivyo sisi kwa sisi. Na Ndugu Goad amefikia mahali hata mimi...yeye hakika anastahili kuwa na cheo, yeye aweza kushindilia magamba sasa. Naam. Na, Ndugu Leo, naamini sisi twaweza tu kumruhusu aende hivyo, na kumwita...kumwachilia aendeleo na cheo chake cha—cha “Daktari.”

⁵³⁷ Vema, “Daktari” Branham, nyuma kule, nyuma kule, mfundishe vilivyo, na nuru ziendeleo kung’aa vizuri sana. Na—na hebu niwaambieni, po pote tunapokuwa na mkutano maalum nitaongea na halmashauri na kuona kama hawawezi kukupa nyingine zaidi kwa hilo [Ndugu Branham acheka—Mh.], kwa kazi maalum inapokulazimu kufagia sana na kubeba-beba huku na huko na itakufurahisha.

⁵³⁸ Daktari Wood. Nilimwita “Daktari,” nakisia mnashangaa mbona hivyo. Sikosei kwa kumwita yeye hivyo, yeye hukata miti vipande-vipande, mwajua. Bwana ataufanya mti mzuri uote,” naye atakatakata na kuujengea nyumba. Sijawahi kuona mtu kama huyo bado, kwa hivyo nitamwita yeye “Daktari.”

⁵³⁹ Ndugu Taylor, wewe bado ungali mwaminifu mlangoni, kumpa mtu fulani kiti. Nadhani unapenda hili, “Ningependa kuwa jamvi mlangoni mwa nyumba ya Bwana wangu kuliko kukaa katika hema za waovu.” Hiyo ni kweli. Bila shaka.

⁵⁴⁰ Ndugu Hickerson, ndiyo kwanza uanze Njiani, nawe unasonga mbele. Nina shauku...mimi...Umeshika Njia, na unaendelea, hakika napenda unyofu wako na yale yote unayomfanyia Bwana Yesu. Mungu akubariki na akufanye shemasi halisi, ndugu, na ninaamini ndivyo ulivyo, ukiitisha nyumba yako na kadhalika kama vile umekuwa ukifanya.

⁵⁴¹ Ndugu Fred, haujakuwa pamoja nasi kwa muda mrefu sana, kutoka kule Canada. Hatujisikii kuwa wewe u mwenyeji wa Canada tena, tunajisikia kuwa wewe u msafiri na mgeni pamoja nasi, kama—kama mdhamini. Wewe pamoja na ndugu Wood,

nanyi mnaotumikia afisi zenu vizuri mkiwa na Ndugu Roberson, na wengine wenu; Ndugu Egan, yeye hayuko hapa usiku wa leo.

⁵⁴² Na Ndugu Roberson, umekuwa m—msaada mkuu kwangu, Ndugu Roberson na wengineo, katika hii kesi ya kodi iliyofanyiwa uchunguzi huu.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org